JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

TAARIFA YA MIAKA ISHIRINI YA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA 2001-2021

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora,
Mtaa wa Nyerere, Kitalu Na. 339, Kilimani,
S.L.P 1049, DODOMA.
Simu: +255 734 047 775; 734 119 978.
Barua pepe: info@chragg.go.tz.
Tovuti: www.chragg.go.tz.

Septemba, 2022

VIFUPISHO

AOMA	-	African Ombudsman and Mediators Associations
AZAKI	-	Asasi za Kiraia
BHR	-	Business and Human Rights
CHRAGG	-	Commission for Human Rights and Good Governance
CMIS	-	Case Management Information System
DANIDA	-	Danish International Development Agency
DIHR	-	Danish Institute for Human Rights
DIT	-	Dar es Salaam Institute of Technology
GANHRI	-	Global Alliance for National Human Rights Institutions
IFAD	-	International Peace Informations System
ILO	-	International Labour Organisation
IOI	-	International Ombudsman Institute
ISAWIMA	-	Igombe – Sagara Wildlife Management Area
IWGIA	-	International Working Group on Indigeneous Affairs
JMT	-	Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
JUWAUZA	-	Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar
LGBTI	-	Lesibians, Gay, Bisexual Transgender and Intersex
LSF	-	Legal Service Facilities
MOU	-	Memorandum of Understanding
NANHRI	-	Network of African National Human Rights Institutions
NEC	-	National Electoral Commission

NSSF	-	National Security Social Fund
OHCHR	-	Office of the High Commissioner for Human Rights
PGO	-	Police General Orders
PILPG	-	Public International Law and Policy Group
SMZ	-	Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
TAKUKURU	-	Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa
TAMISEMI	-	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
TAWA	-	Tanzania Wildlife Authority
TEHAMA	-	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
THBUB	-	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
TKU	-	Tume ya Kudumu ya Uchunguzi
TTCL	-	Tanzania Telecommunication Company Limited
UKIMWI	-	Upungufu wa Kinga Mwilini
UNA	-	United Nation Association of Tanzania
UNGP	-	United Nation Guiding Principles
UPR	-	Universal Periodic Review
USAID	-	United States Agency for International Development
VVU	-	Virusi Vya Ukimwi
ZBC	-	Zanzibar Broadcasting Cooperation
ZEC	-	Zanzibar Electoral Commission
ZSSF	-	Zanzibar Social Security Fund

MUHTASARI

Taarifa hii ya miaka ishirini ya THBUB pamoja na kueleza kwa kifupi historia ya kuanzishwa kwa Tume na uongozi katika kipindi hiki, imeelezea pia baadhi ya kazi zilizotekelezwa Tume katika kulinda, kutetea na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini. Taarifa inaonesha maeneo ambayo yamepewa kipaumbele na Tume ikiwa ni pamoja na:- kulinda na kutetea haki za binadamu kwa kushughulikia malalamiko ya wananchi; kufuatilia masuala ya haki za binadamu; kufanya tafiti mbalimbali; kukagua magereza na sehemu nyingine wanamozuiliwa watu; kuimarisha uhusiano na taasisi za ndani na nje; kueneza elimu ya haki za binadamu; na kuandaa taarifa za mwaka za utekelezaji na taarifa maalum.

Taarifa hii ina sehemu mbili ikiwa ni historia na utekelezaji wa majukumu ya Tume Tanzania Bara na Sehemu ya pili inahusu historia na utekelezaji wa majukumu ya Tume Zanzibar. Sehemu hizi zimegawanyika katika sura mbalimbali. Sura ya kwanza imeainisha kuhusu historia, uongozi na majukumu ya Tume. Kwa kifupi sura hii imeainisha kuhusu; uongozi, majukumu, ukomo wa majukumu, maslahi ya watumishi, mipango mbalimbali ya Tume na hali ya fedha na bajeti.

Sura ya pili imeelezea kwa kifupi kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Tume Tanzania bara ulivyoimarishwa kwa kuweka mikakati ya ushirikiano na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi katika kipindi hiki cha miaka ishirini. Shughuli zilizofanyika ni pamoja na:- kupokea na kuchunguza malalamiko mbalimbali ya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora ambapo jumla ya malalamiko **35,900** yalipokelewa na kufanyiwa uchunguzi ambapo kati ya hayo malalamiko **30,728** yalifanyiwa uchunguzi

na kuhitimishwa, malalamiko **3,648** yalibainika kuwa nje ya mamlaka ya Tume na malalamiko **1,524** yanaendelea kufanyiwa uchunguzi na Tume. Sura hii pia imeainisha kuhusu tafiti na ufuatiliaji, ukaguzi wa maeneo ya vizuizi, mapitio ya sheria mbalimbali, elimu kwa umma na namna ambavyo mashirikiano yaliimarishwa kati ya wadau na THBUB katika kipindi hicho.

Sehemu ya pili ya taarifa hii inazo sura mbili zinazoainisha historia na uongozi wa THBUB na utekelezaji wa kazi za Tume katika kipindi hicho kwa upande wa Zanzibar.Ofisi ya THBUB Zanzibar ilitekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuchunguza malalamiko ya wananchi ambapo katika kipindi hiki jumla ya malalamiko **724** yalipokelewa na kuchunguza. Kati ya hayo, malalamiko **553** yalihitimishwa na malalamiko **171** yanaendelea kuchunguzwa. Sura hii pia imeainisha kuhusu tafiti na ufuatiliaji, ukaguzi wa maeneo ya vizuizi na utoaji wa elimu kwa umma.

Sehemu ya tatu imeainisha kuhusu changamoto na mapendekezo. Tume imekabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo: Ufinyu wa Bajeti; uelewa mdogo wa wananchi kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora; ushirikiano mdogo kutoka kwa taasisi zinazolalamikiwa; kutotekelezwa kwa mapendekezo ya Tume; uhaba wa watumishi na vitendea kazi na taarifa za Tume kutojadiliwa Bungeni.

Katika kukabiliana na changamoto za utendaji kazi zilizojitokeza kwa kipindi cha miaka 20 Tume inapendekeza yafuatayo:

1. Serikali itenge bajeti inayokidhi mahitaji ya rasilimali fedha na pia fedha zilizotengwa zitolewe kwa wakati. Hali hii itasaidia Tume kutekeleza

majukumu yake ya kulinda na kutetea haki za binadamu na misingi ya utawala bora ipasavyo;

2. Taasisi za Serikali na binafsi zinazolalamikiwa zitoe ushirikiano kwa Tume na ziheshimu haki za binadamu na kuzingatia misingi ya utawala bora ili kuepuka malalamiko yanayotoka kwa wananchi;

3. Serikali, Wizara na Idara ziyafanyie kazi mapendekezo ya Taarifa za Tume kuhusu tafiti, ufuatiliaji na chunguzi mbalimbali zinazowasilishwa kwenye mamlaka husika;

4. Wizara ya Katiba na Sheria kuendelea kuiwezesha THBUB kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; na

5. Wizara ya Habari na Utamaduni ihamasishe vyombo vya habari hususan redio jamii kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

YALIYOMO

VIFUPISHO.....i

MUHTASARI iii

KUTOKA MEZA YA MWENYEKITI WA TUME YA HAKI ZA BINADAMU ix

SURA YA KWANZA 1

1.0 HISTORIA, UONGOZI NA MAJUKUMU YA TUME.....1

1.1. Mapendekezo ya Tume ya Rais ya Mfumo wa Chama Kimoja au Vyama Vingi vya Siasa Tanzania (“Tume ya Nyalali”- 1991).....2

1.2. Mapendekezo ya Kamati Kufanya Mapitio Katika Sekta ya Sheria (“Kamati ya Bomani”- 1996) 3

1.3. Mapendekezo ya Kamati ya Kuratibu Maoni kuhusu Katiba (Kamati ya Kisanga”-1998).....4

1.4. Mapendekezo ya Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali 4

1.5. Muundo wa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi 5

1.6. Hali ya Uongozi na Utawala wa iliyokuwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi 5

1.7. Kuanzishwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora mwaka 2001- Marekebisho ya Kumi na Tatu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 8

1.8. Dira, Dhima na Tunu za Tume 9

1.8.1. Dira 9

1.8.2. Dhima.....9

1.8.3. Tunu za Tume 9

1.9. Muundo wa Tume ya Haki za Binadamu na

Utawala Bora 9
1.10. Maslahi ya Watumishi na Vitendea kazi 12
1.11. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Inavyofanya kazi 12
1.11.1.Kanuni za Paris 12
1.11.2.Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora 13
1.11.3.Majukumu ya Tume.....14
1.11.4.Uwezo na Mamlaka ya Tume 15
1.11.5.Ofisi za Tume 16
1.11.6.Viongozi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora 2002-2022.....18
1.12. Bajeti ya THBUB 22
1.13. Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini 25
1.13.1.Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu 2013 -2017 26
SURA YA PILI 28
2.0. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME TANZANIA BARA KWA KIPINDI CHA MIAKA 20 (2001/2002 - 2021/2022).....28
2.1. Utangulizi 28
2.2. Kazi Zilizotekelezwa na Tume (2001/2002- 2021/2022) .29
2.3. Matumizi ya TEHAMA 2001- 2022 50
2.4. Elimu kwa Umma, Mafunzo, Ufuatiliaji na Tafiti.....52
2.5. Uchunguzi wa Hadharani Kuhusu Migogoro ya Ardhi.....74
2.6. Uandaaji na Uwasilishaji wa Taarifa za Tume 78
2.7. Maktaba ya Tume 80
2.8. Ukaguzi wa Magereza, Vituo vya Polisi, Mahabusu za Watoto na Shule ya Maadilisho 80

2.9. Huduma za Kisheria 87
2.10. Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume ...94
2.11. Ushirikiano na Taasisi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa95
2.12. Tathmini ya Tume Kulingana na Paris Principles *(Accreditation)* 101
2.13. Tathmini ya Kimataifa ya Haki za Binadamu Katika Kipindi Maalum (UPR).....102
Mapendekezo 132
2.12 Ushirikiano wa Tume na Taasisi Nyingine 148
SURA YA TATU 149
HITIMISHO 149

KUTOKA MEZA YA MWENYEKITI WA TUME YA HAKI ZA BINADAMU

Napenda kuchukua fursa hii kushukuru Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake vema katika kipindi cha miaka ishirini (20) tangu Tume ilipoazishwa mwaka 2001. Taarifa hii inaeleza kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Tume katika miaka 20 kwa kuonesha mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizojitokeza na mwelekeo wa Tume kwa miaka ijayo.

Nianze kwa kusema kuwa Serikali ilianzisha Tume hii kwa kutumia misingi ya Kanuni za Paris za mwaka 1993 (Paris Principles of 1993) ambazo ziliridhiwa na Baraza la Umoja wa Mataifa. Pamoja na mambo mengine, kanuni hizo zinapendekeza Tume za namna hii kutekeleza majukumu yake kwa uhuru pia kuwa na majukumu mapana kwenye masuala ya ulinzi, utetezi na uhifadhi haki za binadamu; wajumbe wake kuteuliwa kwa njia ya uwazi na kushirikisha wananchi kwa kuzingatia ushiriki wa jinsia na taaluma mbalimbali. Majukumu ya taasisi za namna hii kulingana na kanuni hizi ni kuishauri Serikali kuhusu hali ya haki za binadamu; kupendekeza marekebisho ya sheria na kushiriki kuandaa programu zinazoweza kusaidia kuingiza haki za binadamu katika elimu; kufanya utafiti na kuongeza uelewa kuhusu haki za binadamu kwa wananchi.

Kuanzishwa kwa Tume kumekidhi matakwa hayo ya Kimataifa na inaonekana wazi kuwa Tume imetekeleza majukumu yake kwa uhuru, kwa mujibu wa sheria na kwa kutilia maanani matarajio ya wananchi. Mafanikio hayo yametokana pia na juhudi za Wizara ya Katiba na Sheria kwa niaba ya Serikali ambayo ndiyo imekuwa mstari wa mbele tangu kuanzishwa Tume hii kwa kuiwezesha kutekeleza majukumu yake.

Uzoefu unaonesha wazi kuwa maendeleo, demokrasia ya kweli na amani vinaimarika zaidi pale ambapo haki za watu zinaheshimiwa na misingi ya utawala bora ikiwemo utawala wa sheria vinafuatwa. Mafanikio yaliyopatikana kwa miaka ishirini (20) ya kuwepo kwa Tume yametokana kwa kiasi kikubwa na mchango na ushirikiano wa wadau mbalimbali. Kipekee napenda kuishukuru Serikali yetu ambayo imekuwa ikiiwezesha Tume kifedha, kimuundo na kiutawala.

Mafanikio ya Tume katika kipindi cha miaka ishirini hayawezi kuelezwa pasipo kutambua michango na misaada iliyotolewa na Wadau wa Maendeleo ambao walichangia Tume kupata vitendea kazi, magari, mafunzo kwa watumishi na kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Natoa shukrani za dhati kwa Ubalozi wa Denmark kupitia Shirika la Maendeleo (DANIDA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP, Jumuiya ya Madola, Ubalozi wa Uholanzi, Ubalozi wa Marekani, Raoul Wallenberg Institute ya Sweden Ubalozi wa Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo (SIDA), IPS, DIGNITY, Legal Services Facility (LSF) na Benki ya Dunia kupitia mradi wa kukuza ufanisi katika sekta ya umma (PIF) kwa misaada waliyotoa.

Kwa ujumla katika kipindi cha miaka ishirini (20) Tume imeweza kutekeleza kazi zake kwa mujibu wa sheria na kuweza kuyafikia

malengo yaliyokusudiwa. Dira ya Tume ni kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa na utamaduni wa kuheshimu na kutetea haki za binadamu na misingi ya utawala bora na kwamba masuala hayo yanahuishwa kuanzia katika ngazi ya familia na katika mipango ya kitaifa.

Ni mategemeo yangu kuwa wadau wote wa haki za binadamu watatumia nafasi walizonazo katika kuhakikisha kuwa Tanzania inabaki kuwa mstari wa mbele katika kukuza, kueneza, kutetea na kutekeleza haki za binadamu na misingi ya utawala bora kama nguzo muhimu ya kudumisha amani na maendeleo nchini.

Nina imani kubwa kwamba Serikali na wadau mbalimbali wataendelea kuiwezesha Tume ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kutoa mchango wake mkubwa katika kujenga umoja, mshikamano na utangamano kwa manufaa ya watanzania wote.

Mathew P. M. Mwaimu (Jaji Mstaafu)

Mwenyekiti

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

SURA YA KWANZA

1.0 HISTORIA, UONGOZI NA MAJUKUMU YA TUME

Historia ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni kuanzia mwaka 1966 ilipoundwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi hadi mwaka 2001 ilipovunjwa. Sehemu ya pili ya historia ya Tume inaanzia miaka ya tisini (1990) pale ambapo Tume na Kamati mbalimbali zilipotoa mapendekezo ya kuanzisha chombo huru kitakachoshughulikia masuala ya haki za binadamu na kupelekea mwaka 2001 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kuundwa na kuanza kazi rasmi mwaka 2002 baada ya kuapishwa Makamishna Saba wa Kwanza wa Tume.

Tume ya Kudumu ya Uchunguzi, au "Ombudsman" ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 25 ya Mwaka 1966 ikiwa ni mwaka mmoja tu baada ya kupitishwa kwa mfumo wa utawala wa chama kimoja cha siasa. Mabadiliko hayo yalifanyika kupitia Katiba ya Muda ya Nchi ya mwaka 1965 (*Interim Constiution*) ambayo ilitaja bayana Tume ya Kudumu ya Uchunguzi na kuipa mamlaka ya kufanya kazi Tanzania Bara na Zanzibar. Hata baada ya Katiba ya Muda kubadilishwa mwaka 1977 na kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Kudumu ya Uchunguzi iliendelea kutajwa katika Katiba hiyo na Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984. Tanzania inajivunia kuwa nchi ya kwanza katika Bara la Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kuanzisha ofisi ya

Ombudsman na kuwa na historia ya kutoa msukumo kuhusu masuala ya utawala na uongozi bora miaka michache tu baada ya kupata uhuru.

Tume hiyo ilifanya kazi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na ilihusika na usimamizi wa misingi ya utawala bora na masuala ya matumizi mabaya ya madaraka kwa kupokea na kuchunguza malalamiko ya wananchi kuhusu utawala katika sekta ya umma na Chama wakati huo. Hatma ya uchunguzi wa Tume hiyo ilikuwa ni kupeleka mapendekezo ya uchunguzi wake kwa Rais. Wanaharakati wa haki za binadamu waliikosoa Tume hiyo kwamba haikuwa huru na wazi. Wakati ikihudumu Tume ya Kudumu ya Uchunguzi ilishughulikia malalamiko zaidi ya 60,000 ambapo malalamiko 2,237 yalirithiwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilipoanzishwa mwaka 2001.

1.1. Mapendekezo ya Tume ya Rais ya Mfumo wa Chama Kimoja au Vyama Vingi vya Siasa Tanzania (“Tume ya Nyalali”- 1991)

Mbegu za kuanzishwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora hapa Tanzania zilioteshwa kwa mara ya kwanza na “Tume ya Nyalali” ya mwaka 1991. Tume hii iliwasilisha mapendekezo yake Serikalini mwaka 1992 ikiwemo pendekezo la kuifanyia marekebisho Tume hiyo ili iweze kuwa na manufaa katika utekelezaji wa majukumu yake na hivyo ilipendekezwa kuwa, huru na kuwajibika kwa Bunge na kwamba ipewe mamlaka ya kuamua kuanzisha uchunguzi yenyewe. Hata hivyo, mabadiliko ya nane ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 yaliyofayika mwaka

1992 ambayo yalirudisha rasmi mfumo wa siasa ya vyama vingi hayakuingiza mabadiliko ya Tume ya Kudumu ya Uchunguzi kama ilivyopendekezwa na Tume ya Nyalali.

1.2. Mapendekezo ya Kamati Kufanya Mapitio Katika Sekta ya Sheria ("Kamati ya Bomani"- 1996)

Jitihada za kuanzishwa kwa Tume huru ya haki za binadamu na usimamizi wa misingi ya utawala bora ziliendelea pale Serikali ilipoteua Kamati ya Kufanya Mapitio Katika Sekta ya Sheria (Legal Task Force) chini ya Mpango wa Kurekebisha Mfumo wa Kitaasisi na Kisheria (FILMUP). Kamati hiyo iliongozwa na Jaji Mark Bomani na katika ripoti yake ya mwaka 1996 ilipendekeza, pamoja na mambo mengine kuanzishwa kwa Tume huru ya Haki za Binadamu na Usimamizi wa Utawala (*Commission for Human Rights and Administrative Justice*). Tume hii ingeunganisha kazi za iliyokuwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi (TKU) ikiwa na sehemu mbili: Sehemu ya kwanza ikijihusisha na haki za binadamu na sehemu ya pili ikijihusisha na usimamizi wa misingi ya utawala bora. Mapendekezo ya Kamati hiyo yalifikiwa baada ya kufanya utafiti na kubainisha katika taarifa yake majukumu nane ya kutekelezwa na Tume ya Haki za Binadamu na Usimamizi wa Utawala, madaraka yake, muundo, vitendea kazi na mpango kazi.

Ripoti ya "Kamati ya Bomani" ilitambua mchango mkubwa wa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi (TKU) katika kushughulikia malalamiko dhidi ya matumizi mabaya ya madaraka katika sekta ya umma. Hata

hivyo Kamati ya Bomani ilibainisha kuwa kulikuwepo na udhaifu wa kisheria wa namna TKU ilivyoundwa. Hivyo kupendekeza Sheria irekebishwe au iundwe Tume Huru ya Haki za Binadamu na Usimamizi wa Utawala.

1.3. Mapendekezo ya Kamati ya Kuratibu Maoni kuhusu Katiba (Kamati ya Kisanga"-1998)

Mwaka 1998 Serikali iliidhinisha Waraka Namba moja wa mwaka 1998 (White Paper No. 1) kwa lengo la kukusanya maoni ya wananchi kuhusu mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Kamati iliongozwa na Jaji Robert Habesh Kisanga ambayo baadaye iliyojulikana kama "Kamati ya Kisanga". Katika ripoti yake ya mwaka 1999, "Kamati ya Kisanga" ilipendekeza, pamoja na mambo mengine, kuwepo kwa Tume huru ya haki za binadamu ambayo ingetekeleza yaliyokuwa majukumu na kazi za Tume ya Kudumu ya Uchunguzi.

1.4. Mapendekezo ya Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali

Sambamba na juhudi za Serikali za kuanzisha Tume Huru ya haki za binadamu, vyama visivyo vya kiserikali navyo vilianzisha mchakato wa kutafuta maoni ya kuanzishwa kwa Tume huru ya haki za binadamu, ambao ulikuwa ukiratibiwa na Muungano wa Umoja wa Kimataifa Tawi la Tanzania (United Nations Association of Tanzania –UNA). Kufuatia semina ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali iliyofanyika Januari 1998, yalitayarishwa mapendekezo kwa ajili ya rasimu ya sheria ya

kuanzisha chombo huru cha haki za binadamu. Mapendekezo hayo yalijadiliwa kwenye mkutano wa wadau ulioandaliwa na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba mwezi Septemba 1999, ambapo ilipendekezwa kuwa iandaliwe rasimu ya sheria ya kuanzishwa kwa chombo huru cha haki za binadamu ambayo iliwasilishwa Serikalini.

1.5. Muundo wa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi

Chini ya Ibara ya 68 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Rais alikuwa na mamlaka ya kuteua Makamishna watatu wenye sifa tofauti, na mmoja kati yao aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa iliyokuwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi.

Mbali na Makamishna, Tume iliundwa na Katibu Mtendaji pamoja na maafisa uchunguzi. Kimsingi, Tume ya Kudumu ya Uchunguzi ilijumuisha:- Mwenyekiti; Makamishna; Katibu Mtendaji; Wakurugenzi; Wakuu wa vitengo; na Maafisa Uchunguzi.

1.6. Hali ya Uongozi na Utawala wa iliyokuwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi

Hali ya uongozi na utawala ilikuwa ikibadilika mara kwa mara tangu mwaka 1966 ilipoanzishwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi hadi ilipofutwa. Kimsingi, Tume ilikuwa ikiongozwa na viongozi mbalimbali kama inavyoonekana katika majedwali yanayobainisha vipindi vya uongozi hapa chini:

Jedwali Na. 1: Wenyeviti 1966 – 2002

NA	JINA	MWAKA
1.	Chifu Erasto A. M. Mang'enya	1966 – 1970
2.	Jaji Mark P. K. Kimicha	1970 – 1972
3.	Chifu Erasto A. M. Mang'enya	1972 – 1973
4.	Col. S.J. Kitundu	1974 – 1978
5.	Nd. Ackland L.S. Mhina	1978 – 1983
6.	Nd. Anthony R. Mbelwa	1984 – 1989
7.	Nd. Abdallah M.R. Nungu	1989 – 1995
8.	Nd. Ibrahim S.A. Kajembo	1995 – 1997
9.	Prof. Joseph Mbwiliza	1998 – 2002

Jedwali Na. 2: Makamishna 1966 – 2002

NA	JINA	MWAKA
1.	Nd. Samson Kishosha Gabba	1966 – 1967
2.	Sheikh M. Ramiyah	1967 – 1968
3.	Nd. K.M. Kikwete	1967 – 1971
4.	Sheikh Abdallah Iddi Chaurembo	1969 – 1973
5.	Nd. Wilson Nkeno Bizuru	1972 – 1976
6.	Nd. Alhaji Mharami Mfaume	1973 – 1977
7.	Nd. John Rwemigira Kibogoyo	1976 – 1978
8.	Bibi. Thekla Grace Mchauru	1976 – 1978
9.	Nd. John Baptist Mwenda	1976 – 1978
10.	Nd. Samson Kishosha Gabba	1978 – 1983
11.	Nd. Ali Ame Chum	1978 – 1983
12.	Nd. Rabia Mohamed Hamdani	1978 – 1983
13.	Nd. Ephraim Kulwa Mvanga	1978 – 1984

14.	Nd. Vincent Magoma Dimoso	1983 – 1984
15.	Bibi. Asia Amour Hassan	1983 – 1989
16.	Nd. Mohamed Khatibu Suleiman Reja	1984 – 1990
17.	Nd. Crispin Tungaraza	1985 – 1991
18.	Bibi. Margreth Lilian Ngude	1985 – 1991
19.	Nd. Mwinyiwesa Idarous	1989 – 1993
20.	Nd. Haji M. Haji	1990 – 1996
21.	Nd. I.S.A. Kajembo	1991 – 1995
22.	Nd. A.S. Kabongo	1993 – 1999
23.	Bibi. Halima Hamisi	1994 – 2000
24.	Nd. Ramadhani Shabani	1997 – 2002

Jedwali Na. 3: Makatibu Watendaji 1966 – 2002

NA	JINA	MWAKA
1.	Nd. Herbert Katua	1966 – 1973
2.	Nd. Anthony R. Mbelwa	1973 – 1977
3.	Nd. Fredrick P.S Malika	1978 – 1993
4.	Nd. Q.J. Mlama	1993 – 1998
5.	Nd. Anastas P. Guvette	1998 – 2002

Jedwali Na. 4: Mkurugenzi 1996 – 2001

NA	JINA	CHEO	MWAKA
1.	Bw. Sabath B. Tetti	Mkurugenzi wa Uchunguzi	1996 - 2001

1.7. Kuanzishwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora mwaka 2001- Marekebisho ya Kumi na Tatu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

Kutokana na maoni ya wananchi yaliyohusu Mabadiliko ya Katiba, Serikali iliandaa na kuwasilisha Bungeni muswada wa Mabadiliko ya Kumi na Tatu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 mwezi Januari, Mwaka 2000. Pamoja na mambo mengine, mabadiliko hayo ya Katiba yaliingiza Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwenye Katiba ya Nchi katika Sehemu ya Kwanza Sura ya Sita[1], na kufuta iliyokuwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi. Pamoja na mabadiliko hayo, Sheria iliyokuwa imeanzisha Tume ya Kudumu ya Uchunguzi ya mwaka 1966 haikufutwa. Sheria hiyo ilifutwa rasmi mwaka 2001 mara baada ya Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Na. 7 ya mwaka 2001 kupitishwa na Bunge.

THBUB ilianzishwa tarehe 01 Julai, 2001 kwa taarifa ya kawaida Na. 311 kwenye Gazeti la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Na. 23 la tarehe 08 Juni 2001. Tume ilianza na watumishi 76 (63 Tanzania Bara, 13 Zanzibar) ambao walikuwa katika Tume ya Kudumu ya Uchunguzi. Aidha, Tume ilizinduliwa rasmi tarehe 15 Machi, 2002 baada ya kuteuliwa na kuapishwa Makamishna wake.THBUB ni taasisi ya Muungano na inafanya kazi zake Tanzania Bara na Zanzibar.

[1] Ibara ya 129 -131 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

1.8. Dira, Dhima na Tunu za Tume

Tume inaongozwa na Dira, Dhima na Tunu kama ifuatavyo:

1.8.1. Dira

Kujenga jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu, misingi ya utawala bora na utu wa mtu.

1.8.2. Dhima

Kusimamia ukuzaji, ulinzi na hifadhi ya haki za binadamu, misingi ya utawala bora kwa watu wote kwa kushirikiana na wadau.

1.8.3. Tunu za Tume

Uadilifu, Uwajibikaji, Usiri na Kutoa huduma bora kwa wakati.

1.9. Muundo wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kwa kipindi cha miaka ishirini (20) Tume imekuwa na miundo miwili. Muundo wa kwanza ni wa mwaka 2002 ambao ulikuwa na Idara sita (6) na vitengo vinne (4), na wa pili ni wa mwaka 2018 ambao unatumika hadi sasa ambao ulileta mabadiliko na kuwa na idara nne (04) na vitengo vitano (05). Muundo huu ulipunguza idara zilizokuwa katika muundo wa awali na kuongeza nafasi za Wakurugenzi Wasaidizi.

Tume inaundwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Makamishna watano (5) na Makamishna Wasaidizi ambao idadi yao haikutajwa kwenye Sheria. Wote huteuliwa na Rais kutokana na

mapendekezo ya Kamati ya Uteuzi ambayo hupokea maoni kutoka kwa wananchi. Tume hufanya kazi kwa kipindi cha miaka mitatu, na Makamishna wake wanaweza kuteuliwa kwa kipindi cha pili kisichozidi miaka mitatu. Chini ya Tume kuna Sekretarieti, yenye jukumu la kutekeleza na kusimamia kazi za kila siku za Tume na inaongozwa na Katibu Mtendaji.

Tangu mwaka 2002 hadi mwaka 2022 Tume imeongozwa na Makamishna kwa vipindi vinne (4) ambavyo ni: kuanzia 2002 – 2008, 2009 – 2013, 2014 -2017, 2019 hadi sasa na kufanya jumla ya Wenyeviti wanne (04), Makamu Wenyeviti wanne (**04)** Makamishna ishirini (**20)** na Makamishna Wasaidizi wawili (**02).** Kwa upande wa nafasi ya Katibu Mtendaji, Tume katika kipindi hiki imeongozwa na Makatibu Watendaji watano (**05*)*** tangu kuanzishwa kwake.

Ikama ya watumishi imeongezeka kutoka watumishi 76 mwaka 2002 hadi watumishi 145 waliopo sasa.

Utendaji kazi wa Tume umegawanywa katika Idara na Vitengo. Wakurugenzi au Wakuu wa Vitengo huongoza Idara na Vitengo mtawalia. Aidha, kila Idara imegawanywa katika sehemu zinazoongozwa na Wakuu wa Sehemu kama inavyojionyesha hapa chini:

MUUNDO WA TUME YA HAKI ZA BNADAMU NA UTAWALA BORA KWA



1.10. Maslahi ya Watumishi na Vitendea kazi

Hali za watumishi zimeendelea kuimarishwa katika maeneo mbalimbali kama vile upandishwaji madaraja sawa na Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na.1 wa 2003; ulipwaji wa nauli na posho za safari za kikazi; posho za kazi ya ziada; huduma za matibabu; na hivyo kuongeza motisha kwa watumishi katika kufanya kazi kwa juhudi na maarifa.

THBUB ilianza utekelezaji wa majukumu yake ikiwa na magari kumi na moja (11) na iliendelea kupokea magari mengine kwa nyakati tofauti ambapo hadi Septemba 2022, Tume inayo jumla ya magari ishirini na mbili (**22**) yanayofanya kazi.

Hata hivyo Tume bado inao uhitaji zaidi wa magari mapya kumi ambayo upatikanaji wake utawezesha kuyaondoa magari yote chakavu kwenye matumizi na kupunguza gharama za matengenezo ya mara kwa mara.

1.11. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Inavyofanya kazi

1.11.1. Kanuni za Paris

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni Taasisi ya haki za binadamu ya kitaifa (*National Human Rights Institution*) ambapo majukumu yake yameainishwa kwenye “Kanuni za Paris za mwaka 1993.” Kanuni hizi kimsingi zinaweka utaratibu wa namna taasisi za kitaifa za haki za binadamu zinavyotekeleza majukumu yake kwa kuzingatia mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu.

1.11.2. Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kuanzishwa kwa Tume kupitia Katiba na Sheria ni mojawapo ya matakwa ya "Kanuni za Paris." Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeanzishwa kupitia Ibara ya 129 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa katika Mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2000 na majukumu yake kutamkwa katika Ibara ya 130 ya Katiba hiyo. Sheria ya Tume Sura ya 391 imerejea majukumu ya Tume yaliyomo katika Ibara ya 130 na pia imeweka mamlaka ya Tume na utaratibu wa kutekeleza majukumu yake. Aidha, Sheria ya Tume, inafafanua majukumu ya Tume na kuipa hadhi ya idara huru ya serikali yenye mamlaka ya kufanya kazi zake Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Tanzania ni mojawapo ya taasisi chache za kitaifa katika Bara la Afrika inayojihusisha katika kutetea na kulinda haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Utetezi na ulinzi huo sio tu katika vyombo vya dola bali pia na watu na taasisi binafsi. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Tume hutoa taarifa ya hali ya haki za binadamu nchini. Kanuni za Paris zinatambua kuwa Serikali inayoanzisha Tume huru ya Haki za bindamu inapaswa kuweka kumbukumbu nzuri ya kushughulikia masuala ya uvunjwaji na

ulinzi wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Tume za Haki za Binadamu zimepewa nafasi ya kutoa taarifa kuhusu hali ya haki za binadamu katika nchi katika Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu.

1.11.3. Majukumu ya Tume

Ibara ya 130 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kifungu cha 6(1) cha Sheria Na.7/2001 zinafafanua majukumu ya Tume kama ifuatavyo:

(i) Kuhamasisha hifadhi ya haki za binadamu nchini na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi;

(ii) Kupokea na kuchunguza malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

(iii) Kutoa ushauri kwa Serikali na vyombo vingine vya umma na vya sekta binafsi kuhusu haki za binadamu na utawala bora;

(iv) Kufanya utafiti, kutoa na kueneza elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora;

(v) Kuchukua hatua zipasazo kwa ajili ya kukuza na kuendeleza usuluhishi na suluhu miongoni mwa taasisi na watu mbalimbali wanaofika au kufikishwa mbele ya Tume;

(vi) Kama ikibidi, kufungua mashauri mahakamani kuzuia vitendo vya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

(vii) Kuishauri Serikali kuridhia au kuingia kwenye mikataba ya kimataifa ya kulinda haki za binadamu;

(viii) Kupendekeza marekebisho katika sheria za nchi, miswaada au taratibu za kiutawala ili kuhakikisha kuwa zinakidhi matakwa ya kanuni za haki za binadamu;

(ix) Kushirikiana na mashirika ya kimataifa, kikanda na mashirika mengine ya kitaifa yenye uzoefu na umahiri katika ukuzaji na utetezi wa haki za binadamu na utawala bora; na

(x) Kutembelea magereza na sehemu nyingine ambazo watu wanazuiliwa au kufungwa, kwa nia ya kukagua hali halisi ya sehemu hizo na watu waliozuiliwa au waliofungiwa, na kutoa mapendekezo yenye lengo la kuboresha hali ya maisha katika sehemu hizo.

1.11.4. Uwezo na Mamlaka ya Tume

Kwa mujibu wa kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume itakuwa ofisi ya umma inayoongozwa na sheria na taratibu zinazohusu idara za Serikali. Tume imetengewa fungu lake la fedha

linalojitegemea (*vote*) kwa ajili ya matumizi yake ya kawaida ya kila mwaka. Kila mwaka wa fedha wa Serikali unapowadia, Tume huandaa bajeti yake kulingana na viwango (*ceilings*) vilivyowekwa na HAZINA. Tume inao uwezo wa kuandaa taratibu za kazi na kuainisha majukumu na uwajibikaji wa wafanyakazi wake kufuatana na muundo wake (*organizational structure*), kuajiri kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kuandaa na kutekeleza mpango wake wa kazi wa muda mfupi na mrefu kulingana na mipango ya maendeleo ya taifa na kimataifa.

1.11.5. Ofisi za Tume

THBUB inatoa huduma kupitia ofisi zake kuu zilizoko Dodoma na Unguja pamoja na ofisi za matawi zilizoko Dar es Salaam, Mwanza, Lindi na Pemba. Ofisi za Tume zinapatikana katika maeneo yafuatayo:

- Dodoma (Makao Makuu)
  Mtaa wa Nyerere, Kitalu Na. 339, Kilimani,
  S.L.P 1049, DODOMA.
  Simu: +255 734 047 775; 734 119 978.
  Barua pepe: info@chragg.go.tz.
  Tovuti: www.chragg.go.tz.

- Zanzíbar (Makao Makuu),
  Jengo la Kamisheni ya Wakfu na Mali za Amana, Mbweni.
  S.L.P 285,
  ZANZIBAR.
  Simu: (024)2230494/2236124.
  Barua pepe:zanzibar@chragg.go.tz

- Dar es Salaam (Kanda ya Mashariki),
  Mtaa wa Luthuli Kitalu Na. 8 Haki House,
  S.L.P 2643,
  11101 DAR ES SALAAM.
  Simu: (022) 2135747/8.
  Barua pepe:dsm@chragg.go.tz

- Wete (Kanda ya Pemba),
  Mtaa Kitutia Mkabala na Posta Wete,
  S.L.P 231,
  PEMBA.
  Simu:(024)2454196
  Barua pepe:pemba@chragg.go.tz

- Mwanza (Kanda ya Ziwa),
  Eneo la Mkolani, Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Nyamagana,
  S.L.P 10430,
  MWANZA.
  Simu (028)2541770,
  Barua pepe:mwanza@chragg.go.tz

- Lindi (Kanda ya Kusini),
  Mtaa wa Wailesi, Jengo la zamani la TTCL,
  Barabara iendayo kwa Mkuu wa Mkoa,
  S.L.P 1050,
  LINDI.
  Simu (023)2202734/2202744
  Barua pepe:lindi@chragg.go.tz

Ofisi ya Tume Zanzibar inaongozwa na Kamishna Mkaazi na Tawi la Dar es Salaam linaongozwa na Kamishna. Aidha, Ofisi nyingine za Matawi, zinaongozwa na Maafisa Wafawidhi.

1.11.6. Viongozi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora 2002-2022

Tangu ilipoanzishwa THBUB imekuwa na viongozi ambao wamehudumu katika nyakati tofauti kama ifuatavyo:-

Jedwali Na.5: Wenyeviti 2002 – 2022

NA	JINA	MWAKA
1.	Mhe. Jaji (mstaafu) Robert Habesh Kisanga	2002 – 2008
2.	Mhe. Jaji (Kiongozi Mstaafu) Amir Ramadhani Manento	2008 – 2014
3.	Mhe. Bahame Tom Nyanduga	2015 - 2018
4.	Mhe. Jaji (Mstaafu) Mathew P.M Mwaimu	2019 hadi sasa

Jedwali Na.6: Makamu Wenyeviti 2002 – 2011

NA	JINA	MWAKA
1.	Mhe. Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa	2002 – 2008
2.	Mhe. Mahfoudha Alley Hamid	2008 – 2014
3.	Mhe. Idd Ramadhani Mapuri	2015 - 2018
4.	Mhe. Mohamed Khamis Hamad	2019 hadi sasa

Jedwali Na.7: Makamishna 2002 – 2022

NA	JINA	MWAKA
1.	Mhe. Catherine Herieth Mbelwa Kivanda	2002 – 2008
2.	Mhe. Stephen Zakaria Mwaduma	2002 – 2008
3.	Mhe. Jecha Salim Jecha	2002 – 2008
4.	Mhe. Robert Vincent Makaramba	2002 – 2006
5.	Mhe. Safia Masoud Khamis	2002 – 2008
6.	Mhe. George Francis Mlawa	2007 – 2010

7.	Mhe. Joaquine Antoinette De-Mello	2008 – 2011
8.	Mhe. Zahor Juma Khamis	2008 – 2011
9.	Mhe. Bernadeta Gambishi	2008 – 2011
10.	Mhe. Ali Hassan Rajabu	2010 – 2013
11.	Mhe. Dkt. Kevin Mandopi	2015-2018
12.	Mhe. Salma Ali Hassan	2015-2018
13.	Mhe. Rehema Ntimizi	2015-2018
14.	Mhe. Mohamed Khamis Hamad	2015-2018
15.	Mhe. Dkt. Fatma Rashid Khalfan	2019 hadi Agosti 2022
16.	Mhe. Dkt. Thomas P. Masanja	2019 hadi sasa
17.	Mhe. Amina Talib Ali	2019 hadi sasa
18.	Mhe. Khatib Mwinyichande	2019 hadi sasa
19.	Mhe. Nyanda Josiah Shuli	2019 hadi sasa

Jedwali Na. 8: Makamishna Wasaidizi 2002 – 2014

NA	JINA	MWAKA
1.	Mhe. Costantine Biseko Luguli Mugusi	2007-2010, 2011-2014
2.	Mhe. Fahamu Hamidu Mtulya	2007-2010, 2011-2014

Jedwali Na. 9: Makatibu Watendaji 2002 – 2022

NA	JINA	MWAKA
1.	Bw. Anastas Pius Guvette	2002 – 2003
2.	Bw. Gad John Kimweri Mjemmas	2004 – 2006
3.	Bibi. Upendo Msuya	2007 – 2008
4.	Bibi. Mary C. Massay	2008 – 2018
5.	Bibi. Fatuma I. Muya	Kaimu Katibu mtendaji 2018

		- Feb, 2021
6.	Bw. Nabor B. Assey	Kaimu Katibu Mtendaji Feb, 2021 hadi Dec 2021
7.	Bw. Patience K. Ntwina	Januari 2022 hadi sasa

Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi 2004 – 2022

Kufuatia mabadiliko ya muundo wa mwaka, 2002 na 2018 Wakurugenzi na wakurugenzi wasaidizi wa Idara na vitengo vifuatavyo waliteuliwa.

Jedwali Na. 10: Wakurugenzi 2004-2022

NA	JINA	IDARA	KIPINDI
1.	Bw. Issa A. Nchasi	Utawala na Utumishi	2004 - 2009
2.	Bibi. Mary C. Massay	Huduma za Sheria	2004 – 2008
3.	Bw. Hamisi J. Mvamba	Utawala Bora	2004 -2013
4.	Bibi .Epiphania H. Mfundo	Utafiti na Nyaraka	2004 -2008
5.	Bibi. Rosemary C. Jairo	Elimu kwa Umma na Mafunzo	2004 -2012
6.	Bw. Francis K. Nzuki	Haki za Binadamu	2004 -2020
7.	Bw. Augustine M. Mudogo	Utawala na Rasilimali watu	2009 -2011
8.	Bibi.Florida Kazora	Utawala na Rasilimali watu	2011-2015
9.	Bibi. Tabu Aron	Utawala na Rasilimali watu	2015-2017
10.	Bw.Bernad P.	Utawala na	2017-2018

	Marceline	Rasilimali watu	
11.	Bw.Orest L. Mushi	Utawala na Rasilimali watu	2018 -2020
12.	Bw.Alexander S. Hassan	Elimu kwa Umma na Mafunzo	2012 – Machi, 2021
13.	Bw. Godlisten Nyange	Kaimu Mkurugenzi-Utafiti na Nyaraka	2013-2019
14.	Bibi.Fatuma I. Muya	Utawala Bora	2013-2018
15.	Bw. Nabor B. Assey	Huduma za Sheria	2010 – Machi, 2021 na Disemba 2021 hadi sasa
16.	Bibi.Suzan N. Paschal	Kaimu Mkurugenzi Malalamiko na Uchunguzi	2021 hadi sasa
17.	Bw.Joshua K. Taramo	Kaimu Mkurugenzi Elimu kwa Umma, Mawasiliano, Utafiti na Nyaraka	Machi, 2021 hadi sasa
18.	Bw.Baraka R. Baraka	Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini	2020 - Juni 2021
19.	Bibi. Caroline N. Shao	Kaimu Mkurgenzi Malalamiko na Uchunguzi	2020 - 2021
20.	Bw. Robert G. Mangowi	Kaimu Mkurugenzi Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini	Juni, 2021 hadi sasa

Jedwali Na.11: Wakurugenzi Wasaidizi 2018 - 2022

NA	**JINA**	**IDARA/SEKSHENI**	**KIPINDI**
1.	Bibi. Portacia G. Benito	Utawala	2019 hadi sasa
2.	Bw. Mbwana M. Mbwana	Utawala Bora	2019 hadi sasa
3.	Bw. Andrew R.	Sheria-Ushauri	2019 hadi

	Samanyi		sasa
4.	Bw. Philipo R. Sungu	Haki za Binadamu	2020 hadi sasa
5.	Bibi. Fides A. Shao	Kaimu Mkurugenzi Utafiti na Nyaraka	2021 hadi sasa
6.	Bw. Gabriel S. Lubyagila	Sheria-Utekelezaji	2019 hadi sasa
7.	Bw. Germanus J. Kyafula	Elimu kwa Umma na Mawasiliano	2019 hadi sasa
8.	Bibi. Caroline N. Shao	Haki za Binadamu	2019 – 2020

1.12. Bajeti ya THBUB

THBUB imekuwa ikitekeleza majukumu yake kutokana na fedha zinazotoka katika Ruzuku ya Serikali na kutoka kwa Wadau wa Maendeleo. Fedha hizi zimekuwa zikitumiwa kupitia mifumo mbalimbali ya kifedha inayotumika kwa ajili ya kupokea fedha kulipa, kuandaa ripoti, kutunza mali na madeni ya Serikali.

Mapato na matumizi ya fedha ya THBUB yanazingatia Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001 na marekebisho yake ya mwaka 2004, na miongozo mbalimbali inayotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa kipindi cha miaka 20 THBUB imefanikiwa kupata hati safi kutoka kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Tafsiri ya hati safi ni kuonesha kuwa THBUB inazingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayotolewa na serikali kuhusu matumizi ya fedha za umma.

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2001, Tume imekuwa ikipokea ruzuku na fedha za maendeleo kutoka Hazina ya Taifa baada ya bajeti yake kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Katika kipindi cha miaka 20 iliyopita hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022, Tume ilipokea jumla ya Tshs. **81,236,400,809.00** badala ya Tshs **93,592,366,651.00** ambayo ni pungufu ya asilimia 13 ya bajeti iliyotengwa.

Jedwali Na 12: Mtiririko wa Bajeti za Ruzuku na Fedha za Maendeleo kwa Miaka 20 ya Tume

Mwaka wa Fedha	Bajeti	Ruzuku
2001/2002	842,600,000	725,697,775
2002/2003	993,268,200	787,296,671
2003/2004	1,680,200,000	1,352,000,000
2004/2005	1,985,000,000	1,780,800,000
2005/2006	2,248,332,396	2,074,732,296
2006/2007	2,982,300,000	2,731,910,000
2007/2008	3,733,630,000	3,424,170,000
2008/2009	4,347,619,235	4,140,481,855
2009/2010	6,321,000,000	6,001,625,290
2010/2011	4,844,021,592	4,523,027,178
2011/2012	4,853,501,105	4,001,739,028
2012/2013	6,315,293,225	5,490,881,912
2013/2014	6,649,267,000	4,498,989,075
2014/2015	4,952,350,000	4,806,155,017
2015/2016	5,388,071,000	3,965,585,899
2016/2017	3,781,088,084	3,416,016,019
2017/2018	4,171,838,694	3,963,937,289
2018/2019	6,757,801,000	6,337,132,740
2019/2020	7,021,437,982	4,325,039,894
2020/2021	6,995,659,000	6,918,773,304
2021/2022	6,728,088,136	5,970,409,561
JUMLA KUU	**93,592,366,649**	**81,236,400,803**



1.13. Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini

Katika kipindi hiki THBUB ilitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia: Mpango Mkakati wa Tume wa mwaka 2005/06 - 2009/10 - 2010/11 2014/15 na 2018/19 - 2022/23; Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu *(National Human Rights Action Plan)* 2013-2017; Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu *(Monitoring and Evaluation Framework of the National Human Rights Action Plan);* Mpango Mkakati wa Mawasiliano (Communication and Visibility Strategy 2018 – 2023); Mkakati wa Ushirikishwaji wa Wadau 2018 – 2022 *(Stakeholders' Engagement Strategy 2018 – 2023);* na Mpango Mkakati wa TEHAMA kwa Mwaka 2019/2020 – 2021/2022.

1.13.1. Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu 2013 -2017

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na THBUB, iliunda Kamati ya Kitaifa ya Uratibu (*National Coordination Committee*). Kamati hiyo kwa msaada wa Umoja wa Mataifa ilitengeneza Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu 2013 - 2017 kwa mara ya kwanza kwenye historia ya Tanzania kama sehemu ya kuimarisha mfumo wa kitaifa wa kukuza na kulinda haki za binadamu nchini. Mpango huo ulijumuisha Wizara, Idara, Taasisi na Serikali za Mitaa zote Tanzania bara na Zanzibar.

Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu 2013-2017 ulilenga kuimarisha masuala ya haki za binadamu Tanzania kwa kukuza mbinu zinazozingatia haki za binadamu katika kuleta maendeleo na kupunguza umaskini. Mpango kazi huo ulikuwa na malengo makuu mawili, ambayo ni:

(i) Kukuza na Kulinda haki zinazoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 na Katiba ya Zanzibar 1984 pamoja na mikataba ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu; na

(ii) Kuimarisha uhusiano wa haki za binadamu na mikakati ya maendeleo ya taifa.

Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki Binadamu 2013 - 17 ulianisha maeneo manne (4), ambayo ni:

(a) Haki za Kiraia na Kisiasa;

(b) Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni;

(c) Haki za Makundi ya Watu wenye Mahitaji Maalum nchini; na

(d) Uimarishwaji wa Taasisi na Masula Mtambuka nchini.

Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu 2013-2017 ulikuwa wa kwanza nchini Tazania. THBUB kama Taasisi ya Haki za Binadamu ya Kitaifa (NHRI) ilishiriki kuandaa na kutekeleza mpango huo kama ifuatavyo:- Kutoa na kueneza elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu:

(i) Kuwajengea uwezo watumishi mbalimbali wa Umma hasa kwenye Sekta ya Utoaji haki (Mahakama, Polisi na Magereza) kuhusu uelewa wa haki za binadamu;

(ii) Kukuza na kulinda haki za Makundi ya Watu wenye Mahitaji Maalum;

(iii) Kuimarisha utoaji huduma kwa wananchi (Service Delivery);

(iv) Kuhamasisha haki za binadamu na biashara nchini na;

(v) Kuongeza mashirikiano na wadau mbalimbali wa haki za binadamu.

SURA YA PILI

2.0. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME TANZANIA BARA KWA KIPINDI CHA MIAKA 20 (2001/2002 - 2021/2022)

2.1. Utangulizi

Majukumu ya Tume yameainishwa katika Ibara ya 130 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Sheria ya Tume Sura ya 391. Katika kipindi cha miaka ishirini (20) (2001/2002- 2021/2022) Tume imetekeleza majukumu yake kwa kuzingatia:- Mipango Mikakati ya Tume ya mwaka 2005/06 - 2009/10, 2010/11 – 2014/15 na 2018/19 - 2022/23; Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (2013-2017), Mipango na Mikakati mbalimbali ya Maendeleo ya Nchi; na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2000/2005-2020-2025. Baadhi ya Kazi zilizofanyika kwa kipindi hicho ni pamoja na:-

(i) Kupokea na kuchunguza malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

(ii) Kukagua Magereza, Vituo vya Polisi, Mahabusu za Watoto na Shule ya Maadilisho;

(iii) Kutoa elimu ya haki za binadamu na utawala bora;

(iv) Kufuatilia masuala mbalimbali ya haki za binadamu na utawala bora nchini;

(v) Kuandaa taarifa za mwaka za hali ya haki za binadamu na utawala bora nchini na utekelezaji wa majukumu ya Tume kila mwaka;

(vi) Kupendekeza marekebisho ya sheria mbalimbali;

(vii) Kutoa ushauri kwa Serikali na taasisi zake kuhusu utekelezaji wa haki za binadamu na utawala bora nchini; na

(viii) Kushirikiana na taasisi nyingine za ndani na nje katika kutekeleza majukumu yake kwa kupitia wahisani na wadau wa maendeleo.

2.2. Kazi Zilizotekelezwa na Tume (2001/2002- 2021/2022)

2.2.1. Malalamiko na Uchunguzi

Ibara ya 130(1) (c), (f) na (g) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na vifungu vya 6 (1) (c), (f), (g) na 15 (1) (a) vya Sheria ya Tume Sura ya 391 vimeipa THBUB mamlaka ya kupokea na kuchunguza malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora nchini.

2.2.2. Utaratibu wa Kupokea na Kuchunguza Malalamiko

Utaratibu wa kupokea na kushughulikia malalamiko umeainishwa katika kanuni na miongozo ifuatayo:

Kanuni za Kushughulikia Malalamiko (Tangazo la Serikali Na. 144/2003), Utaratibu wa Uchunguzi (Tangazo la Serikali Na. 145/2003) na Mwongozo wa Kushughulikia Malalamiko wa mwaka 2005.

Tume hupokea na kuchunguza malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora kwa mujibu wa Ibara ya 130 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na vifungu vya 6(1)(b), 15(1)-(3) (a) na (b) vya Sheria ya Tume Sura ya 391. Malalamiko hayo hupokelewa kutoka kwa mtu mmoja mmoja, kikundi cha watu, jumuiya, taasisi na makampuni. Pia Tume inaweza kuanzisha uchunguzi wa malalamiko yenyewe.

Malalamiko yanaweza kuwasilishwa[2] kwa mtu kufika kwenye mojawapo ya ofisi za Tume; kutuma kwa barua kwa njia ya posta au barua-pepe, kupiga simu, kutuma ujumbe wa simu ya kiganjani "USSD Code", au kwa simu janja (Haki App) na kwa kutumia tovuti ya Tume.[3]

Malalamiko yanayopokelewa hufanyiwa uchambuzi ili kubaini iwapo yapondani ya mamlaka ya Tume kwa kwa mujibu wa sheria . Kwa yale ambayo hubainika kuwa nje ya mamlaka ya Tume, mlalamikaji hushauriwa ipasavyo na au huelekezwa kufanya ufuatiliaji katika mamlaka husika. Malalamiko yanayopokelewa na Tume huingizwa kwenye mfumo wa kushughulikia utekelezaji wa kazi za Tume (*Complaints Management Information System-CMIS*). Yale yatakayobainika kuwa ndani ya mamlaka ya Tume, huchunguzwa kwa kuzingatia Kanuni za Haki za

[2] Kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Tume Sura ya 391.
[3] Email, info@chragg.go.tz, SLP 1049 DODOMA

Asili "*Natural Justice*" kwa kujumuisha mawasiliano ya pande zinazohusika kwa maana ya; mlalamikaji, mlalamikiwa na mashahidi ili kupata taarifa sahihi zitakazosaidia kufikia muafaka wa lalamiko husika.

Baada ya uchunguzi kukamilika na matokeo kuthibitisha kuwa kuna uvunjwaji wa haki za binadamu au ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, THBUB hutoa taarifa ya uchunguzi yenye mapendekezo ambayo huwasilishwa kwa mamlaka husika kwa ajili ya utekelezaji ndani ya siku tisini (90).[4] Endapo mamlaka husika haitatekeleza mapendekezo ya Tume ndani ya muda uliotajwa, Tume imepewa mamlaka ya kufungua shauri mahakamani. Pamoja na kupewa mamlaka hiyo, Tume haizuiliwi kuendelea na usuluhishi baina ya pande zote mbili.[5]

2.2.3. Malalamiko Yaliyopokelewa na Kuchunguzwa na THBUB

Katika kipindi hiki cha miaka 20 Tume ilipokea jumla ya malalamiko **35,900.** Kati ya hayo, malalamiko **2,237** yalirithiwa kutoka Tume ya Kudumu ya Uchunguzi na malalamiko **33,663** yalipokelewa na THBUB. Malalamiko **30,728** yalihitimishwa na **3,648** yalikuwa nje ya mamlaka ya Tume na malalamiko. Aidha, malalamiko **1,524** uchunguzi wake unaendelea.

Idadi ya malalamiko yaliyopokelewa na Tume tangu ilipoanzishwa mwaka 2001/2002 kama inavyoonekana katika Jedwali hapa chini.

[4] Kifungu cha 28 (1) na(2) cha Sheria ya Tume Sura ya 391
[5] Kifungu 28 (3-4) cha Sheria ya Tume Sura ya 391

Jedwali Na. 13: Malalamiko yaliyopokelewa kuanzia Julai 2001 – Juni 2022

Mwaka	Idadi ya malalamiko	Yaliyohitimishwa
Yaliyorithiwa kutoka TKU	2,237	-
2001/2002	1,074	-
2002/2003	2,458	1,595
2003/2004	2,691	1,564
2004/2005	2,789	2,447
2005/2006	3,812	3,021
2006/2007	4,948	3,538
2007/2008	2,660	2,424
2008/2009	2,459	2,731
2009/2010	1,454	1,588
2010/2011	1,355	1,058
2011/2012	965	1,672
2012/2013	1,545	1,250
2013/2014	1,080	1,202
2014/2015	914	1,017
2015/2016	579	1,106
2016/2017	786	1,260
2017/2018	562	482
2018/2019	424	233
2019/2020	333	1,122
2020/2021	518	622
2021/2022	257	796
Jumla	**35,900**	**30,728**

Jedwali hapo juu linaonesha kuwa mwaka 2001/2002 hakuna lalamiko lililohitimishwa na hii ni kutokana na Tume kuanza kazi mwaka 2002 baada ya kuapishwa rasmi kwa makamishna ambao ndiyo wenye mamlaka kisheria kuhitimisha malalamiko.

2.2.4. Chunguzi za Malalamiko ya Uvunjwaji wa Haki za Binadamu na Ukiukwaji wa Misingi ya Utawala Bora

Katika kipindi cha miaka 20 Tume ilifanya chunguzi za malalamiko mbalimbali. Chunguzi hizo zilichangia kupata suluhu ya malalamiko, kuondoa migongano na migogoro baina ya wananchi, au wananchi na taasisi za Serikali, au na sekta binafsi, hivyo kuleta hali ya amani na utulivu ambayo ni mazingira muhimu katika maendeleo ya nchi. Baadhi ya chunguzi zilizofanyika ni kama zifuatazo:-

2.2.4.1. Chunguzi za Migogoro ya Ardhi

THBUB ilichunguza migogoro ya ya ardhi iliyohusu wananchi kuondolewa kwa nguvu kwenye maeneo yao, uchimbaji wa madini na uhifadhi wa mazingira. Miongoni mwa migogoro hiyo ni: Mgogoro wa Ardhi katika Kijiji cha Merera Wilaya ya Kilombero Mkoani Morogoro; mwananchi wa wilaya ya Kiteto kutorejeshewa mifugo yake kwa madai ya kulisha kwenye hifadhi; kusitishwa shughuli zote za uchimbaji wa mawe na udongo wa madini ya “Bauxite” katika machimbo yaliyopo Kata ya Magamba, Wilaya ya Lushoto Mkoani Tanga na Utekelezaji wa mpango wa urejeshaji wa mazingira (*mining closure and rehabilitation program*) katika mgodi wa uchimbaji madini wa Buzwagi katika Wilaya ya Kahama Mkoani Shinyanga.

Migogoro mingine ni madai ya wananchi kuondolewa katika Vijiji vya Ufulaga na Mtakuja Magharibi Kata ya Igagala Wilaya ya

Kaliua kupisha Hifadhi dhidi ya Jumuiya ya Jamii ya Hifadhi ya Wanyamapori Igombe-Sagara "*Igombe - Sagara Wildlife Management Area*" (ISAWIMA) na lalamiko dhidi ya Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Saadani kuhusu Kuingizwa Kwa Kitongoji cha Uvinje Katika Hifadhi ya Taifa ya Saadani.

Masuala yaliyobainika katika chunguzi hizo ni pamoja na:

(i) Wananchi kukosa taarifa sahihi kutoka kwenye mamlaka za Serikali kuhusu kuondolewa katika maeneo yao;

(ii) Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu sheria na taratibu za miliki na matumizi ya ardhi;

(iii) Baadhi ya wananchi kutotekeleza sheria na maagizo ya Serikali ikiwemo kuhama baada ya kulipwa fidia;

(iv) Kutoendelezwa kwa baadhi ya maeneo ya ardhi na mashamba ambayo yamemilikishwa kwa wawekezaji hivyo kuwashawishi wananchi kuingia katika maeneo hayo na kuanzisha makazi, shule, shughuli za kilimo na ufugaji huku wakitambua wazi kuwa maeneohayo yamemilikishwa kisheria kwa Wawekezaji;

(v) Baadhi ya viongozi wa vijiji na Kata kutumia madaraka yao vibaya kwa kugawa eneo moja kwa wamiliki tofauti (double allocation);

(vi) Wananchi kuingia kwenye maeneo ya hifadhi na kufanya shughuli za kibinadamu mathalan ufugaji na kilimo; na

(vii) Askari wa maeneo ya Hifadhi na Mapori ya Akiba kuvunja haki za binadamu na kukiuka misingi ya utawala bora wakati wakitekeleza majukumu yao.

Mapendekezo

Kwa kuzingatia matokeo ya chunguzi hizo, Tume ilitoa mapendekezo yafuatayo:

(i) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakiki mipaka ya Hifadhi, Mapori ya Akiba, na Vijiji vinavyopakana kwa kushirikisha wananchi ili kuweka alama zenye kuonekana na kutambua mashamba na makazi ya wananchi ambayo yameguswa na mipaka ya hifadhi;

(ii) Mamlaka za Serikali zisitishe shughuli mpya za maendeleo ikiwemo shughuli za ujenzi na uzalishaji kwenye maeneo yenye migogoro hadi ufumbuzi upatikane;

(iii) Mamlaka za Serikali zishirikishe kikamilifu wananchi katika hatua mbalimbali zinazochukuliwa katika kutatua migogoro ya ardhi;

(iv) Viongozi wa vijiji wasimamie sheria katika utendaji wao wa kazi;

(v) Elimu kuhusu masuala ya matumizi na umiliki wa ardhi itolewe kwa wananchi ili kuepusha uvamizi wa ardhi na maeneo ya mashamba pori;

(vi) Mamlaka husika zisimamie Wawekezaji wanapotekeleza miradi yao na kuzingatia masharti ya umiliki wa maeneo ya uwekezaji;

(vii) Wananchi wazingatie sheria na taratibu pale ardhi inapotwaliwa;

(viii) *Tanzania Wildlife Authority (TAWA)* ihakikishe Askari wa wanyama pori wanasimamia utekelezaji wa majukumu yao kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa na kuheshimu haki za binadamu.

2.2.4.2. Matumizi Mabaya ya Madaraka na Ofisi

THBUB ilifanya chunguzi kuhusu tuhuma za matumizi mabaya ya madaraka na ofisi. Baadhi ya chunguzi hizo ni kama ifuatavyo:

1. **Lalamiko Na. UB/S/1608/2020/2021/SCO4**

Lalamiko hili lilihusu mwananchi mmoja kusitishiwa biashara yake kinyume na utaratibu, kuharibiwa miundombinu ya shamba lake, kusitishiwa mchakato wa kupata hati miliki ya shamba na kudaiwa rushwa.

Ililalamikiwa kuwa Kiongozi mmoja wa Wilaya alisitisha biashara ya mwananchi huyo kinyume na utaratibu, ambapo aliamuru wananchi waharibu miundombinu katika shamba lake na kuzuia mchakato na nyaraka zake zinazohusu maombi ya hati miliki ya kimila ya shamba lake. Tuhuma nyingine ilikuwa ni madai ya rushwa na kumfanyia vurugu kiasi cha kusababisha usumbufu kwa wateja katika biashara yake.

Uchunguzi ulithibitisha kufanyika kwa vitendo vya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora hususan utawala wa sheria na matumizi mabaya ya madaraka vilivyofanywa na Kiongozi huyo.

Tume ilihitimisha lalamiko hili kwa kutoa mapendekezo kwa mamlaka ya uteuzi wa Kiongozi husika kwamba achukuliwe hatua za kinidhamu na TAKUKURU ifanye

uchunguzi wa madai ya rushwa dhidi ya kiongozi huyo.

2. Lalamiko Na UB/S/1556/2020/2021/SCO1

Lalamiko hili lilihusu kiongozi mmoja wa Serikali kutumia madaraka yake vibaya na kumzuia mwananchi mwenye kampuni ya uwindaji kufanya shughuli zake za uwindaji baada ya kuingia kwenye mgogoro na mshirika mwenzake. Ilidaiwa kwamba Kiongozi huyo alishirikiana na Kiongozi mmoja wa Kata pamoja na Jeshi la Polisi kumkamata mwananchi huyo na kumuweka mahabusu katika kituo kimoja cha Polisi bila ya kumfikisha mahakamani.

Katika uchunguzi huo, Tume ilibaini kuwa kulikuwa na uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora hususan uadilifu, utawala wa sheria, uwazi na uwajibikaji katika tukio hilo.

Tume ilitoa mapendekezo kwa mamlaka ya uteuzi wa kiongozi huyo kwamba imuelekeze kuzingatia misingi ya sheria na utawala bora na kuheshimu mipaka yake katika kutekeleza majukumu aliyopewa. Aidha, Tume ilipendekeza TAKUKURU ifanye uchunguzi juu ya uhusiano uliokuwepo kati ya Kiongozi huyo na aliyekuwa mshirika mwenza wa mlalamikaji.

3. Lalamiko Na.UBS/S/1699/2020/2021/SCO4

Lalamiko hili lilihusu malipo ya fidia ya shamba la ekari 15 kulipwa mtu asiyestahili kinyume na taratibu.

Tume ilichunguza tuhuma dhidi ya Kiongozi wa Jiji kuwa alihusika kulipa fidia ya shamba la ekari 15 kwa mtu asiyestahili kinyume na utaratibu.

Baada ya uchunguzi, Tume ilibaini kuwa madai hayo yalikuwa ya kweli kwani Kiongozi huyo alishindwa kutekeleza uamuzi wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya katika Rufaa iliyompa haki mlalamikaji kuwa mmiliki halali wa eneo hilo na kupuuza pendekezo kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka la kutolipa fidia kwa mtu asiyestahili kufuatia uwepo wa kesi mahakamani.

Tume ilipendekeza kwa Kiongozi wa Jiji kumtambua mlalamikaji kama mmiliki halali wa shamba la ekari 15 lililolipwa fidia kwa mtu asiyestahili kama ilivyoamuliwa na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya. Aidha, ilipendekezwa kuwa kiongozi huyo amlipe mlalamikaji fidia ya fedha yenye thamani ya ardhi ekari 15 kwa kuzingatia thamani ya soko la wakati huo.

4. Lalamiko Na. HB/S/2030/2020/2021/SC19

Lalamiko hili lilihusu wafanyabiashara wa Machinjio mojawapo nchini dhidi ya Mamlaka ya usimamizi wa shughuli hizo Tanzania na Mamlaka ya usimamizi wa sheria. Walalamikiwa walituhumiwa kuendesha zoezi la kuwaondoa wafanyabiashara waliokuwa wakifanya shughuli zao kando ya machinjio hiyo.

Hata hivyo ilidaiwa kuwa zoezi hilo pia lilijumuisha wafanyabiashara waliokuwa ndani ya machinjio kwa kunyang'anywa nyama, kuwatoza faini ya Tsh 100,000/= kila mmoja na Watendaji wa Mamlaka ya usimamizi wa Sheria husika kugawana nyama hiyo. Kufuatia taarifa hizo Tume ilifanya uchunguzi na kubaini yafuatayo:

(i) Zoezi hilo lilifanyika bila kuwashirikisha wadau pamoja na mamlaka nyingine zinazosimamia Sekta ya Nyama kinyume cha Sheria na kanuni;

(ii) Zoezi hilo lilifanyika kwenye eneo ambalo halikulengwa kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Wilaya. Zoezi hilo lililenga kuwaondoa wafanyabiashara wanaouza nyama nje ya machinjio lakini kinyume chake lilijumuisha pia wafanyabiashara waliokuwa wakifanya shughuli zao ndani ya machinjio.

Tume ilitoa mapendekezo yafuatayo:

(i) Hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yawatumishi wa Bodi ya Nyama na Watendaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Sheria wa Kituo cha husika walioshiriki katika zoezi hilo;

(ii) Taasisi za Serikali zinapoendesha zoezi kama hilo zizingatie msingi wa ushirikishwaji wa wadau muhimu wakati wa utekelezaji wa majukumu yake kisheria.

5. Kupigwa, Kuteswa na Vifo Kwenye Mahabusu za Jeshi la Polisi

THBUB ilifanya chunguzi katika maeneo mbalimbali nchini kuhusu tuhuma za wananchi kupigwa, kuteswa kuuawa na wengine kupata ulemavu. Chunguzi hizo zilifanyika kwa lengo la kupata ukweli ili kuthibitisha tuhuma mbalimbali kuhusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Chunguzi hizi zilibaini kuwepo kwa vitendo vya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora vinavyofanywa na Jeshi la Polisi kama ifuatavyo:

(i) Kupiga, kutesa na kuwafanyia vitendo vya kikatili na udhalilishaji watuhumiwa

wakati wa ukamataji na mahojiano ili wakiri makosa;

(ii) Kuwanyima dhamana watuhumiwa hata pale makosa yanayowakabili kustahili kupatiwa dhamana kwa mujibu wa sheria; na

(iii) Kuwabambikiza watuhumiwa kesi, kuchelewesha upelelezi na kutowafikisha watuhumiwa mahakamani kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali.

Mapendekezo yaliyotolewa na Tume ni pamoja na:

(i) Jeshi la Polisi kuchukua hatua za kinidhamu kwa Askari wote waliothibitika kuhusika na tuhuma za kuwapiga na kuwatesa watuhumiwa;

(ii) Jeshi la Polisi kufanya mapitio ya adhabu za kinidhamu zilizotolewa kwa baadhi ya Askari kwa kuzingatia uzito wa makosa waliyofanya Askari Polisi na Maafisa wa Polisi yakihusisha matukio ya uvunjwaji wa haki za binadamu ili Askari hao wapewe adhabu stahiki;

(iii) Makamanda wa Polisi wa Mikoa kusimamia utendaji wa Askari na Maafisa wa Polisi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu

zinazoongoza maadili ya utumishi wa Jeshi la Polisi;

(iv) Serikali iimarishe Jeshi la Polisi kwa kulipatia vitendea kazi, kuongeza idadi ya Askari Polisi na kuimarisha miundombinu;

(v) Wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi ili kusaidia kuzuia na kupambana na vitendo vya uhalifu nchini.

6. Lalamiko Na UB/S/30/11/12/DED/LD

Lalamiko hili lilihusu Mtumishi Mstaafu katika Halmashauri mojawapo katika Wilaya nchini kupunjwa malipo ya kusafirisha mizigo kutoka eneo la kazi hadi Kijijini kwake katika mkoa mmojawapo nchini ambapo alidai kuwa alistahili kulipwa kiasi cha Tshs **11,588,000/=** lakini Halmashauri husika ilimlipa Tshs **6,664,000/=**

Katika uchunguzi wake Tume ilibaini kuwa mlalamikaji alilipwa gharama ndogo za nauli na kusafirisha mizigo kinyume cha taratibu.

Tume iliwasiliana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika na kukiri madhaifu yaliyojitokeza na kumlipa mlalamikaji kiasi cha fedha kilichokuwa kimebaki kwa Hundi Na. 004725 ya tarehe 08/05/2015 na

kufanya jumla ya malipo ya Tshs **11,588,000/=** kama alivyostahili.

7. **Lalamiko Na UB/S/07/14/15/MAG/LD**
   Lalamiko hili lilimhusu Askari Magereza akimtuhumu Kiongozi wake kwa kumnyanyasa. Katika lalamiko hilo, mlalamikaji alilalamikia kutumiwa vibaya madaraka na kumnyanyasa kwa kutompandisha cheo, kutishiwa usalama wa ajira yake na kusemwa vibaya na viongozi.

   Tume ilifuatilia lalamiko hili na uongozi wa Makao Makuu uliingilia kati na kutoa kibali cha kumhamisha mlalamikaji kituo cha kazi na kwenda mkoa mwingine.

8. **Lalamiko: UB/S/28/09/10/NSSF/LINDI**
   Lalamiko hili lilimhusu mwananchi mmoja aliyekuwa mtumishi wa Kampuni ya kutoa huduma ya Usafi. Baada ya kufanya kazi katika kampuni hiyo kwa muda wa miaka miwili (2) mlalamikaji aliamua kubadilisha kazi lakini alipofuatilia malipo ya NSSF alijulishwa kuwa mwajiri alikuwa hapeleki michango yake NSSF.

   Katika uchunguzi wake Tume ilibaini kwamba ni kweli mwajiri alikuwa hapeleki michango yake NSSF na baada ya Tume kumshauri alifanya hivyo na Mlalamikaji kupata haki yake na lalamiko lake kupatiwa ufumbuzi kwa kulipwa madai yake na NSSF.

9. Lalamiko Na. UB/S/502/DSM

Mlalamikaji kwa niaba ya Wanachuo wa Chuo Fulani cha Ualimu alilalamika kwamba uongozi wa Mkuu wa Chuo na wa Mshauri wa wanafunzi (Dean of Students) ni mbaya. Alifafanua kwamba Mkuu wa Chuo hutumia vitisho, hasikilizi matatizo ya wanachuo, amewagawa walimu katika makundi, hataki kupokea ushauri na ana uhusiano wa kimapenzi na wanachuo wa kike. Kuhusu Mshauri wa Wanafunzi, ilidaiwa kuwa huwa na tabia ya kutumia lugha ya matusi kwa wanachuo na hawajali wanachuo.

Uchunguzi ulifanywa na ilithibitika kuwa ulikuwepo upungufu katika uongozi wa chuo na kusabbisha kero za wanachuo zisipatiwe ufumbuzi. Pia Wakufunzi na Mkuu wa Chuo walikuwa na tabia ya ufuska. Tume ilipendekeza kwa mamlaka husika ichukue hatua za haraka kurekebisha matatizo ya uongozi yaliyosababisha malalamiko. Hatimaye baadhi ya Wakufunzi na Mkuu wa Chuo walihamishwa na Mkufunzi mmoja alipewa onyo. Tatizo la uongozi mbaya chuoni lilitatuliwa.

10. Lalamiko Na. 669/1999

Mlalamikaji ni mkazi wa Mbagala Mjini Dar es Salaam, alileta lalamiko lake mbele ya Tume akieleza kuwa alivunjiwa nyumba

yake na mtu ambaye naye aliuziwa kiwanja cha eneo hilo na mfanyabiashara mmoja. Mlalamikaji alifungua kesi ya madai dhidi ya mvunja nyumba katika Mahakama ya Mwanzo. Hakuridhika na hukumu iliyotolewa kuwa alipwe fidia na kiwanja amilikishwe mdaiwa. Aliendelea kukata rufaa hadi Mahakama Kuu ambako hukumu iltolewa kwamba alipwe fidia na arudishiwe kiwanja chake. Fidia ililipwa mara moja lakini kiwanja hakikurejeshewa kwa kuwa Hakimu alikula njama na mdaiwa pia na mfanyabiashara aliyeuziwa kiwanja hicho kukwamisha utekelezaji wa hukumu kuhusu kurudishiwa kiwanja.

Tume ilifanya uchunguzi kuhusu kutotekelezwa sehemu ya hukumu na kufanikisha mlalamikaji kupata haki yake na hatimaye mlalamkaji alikabidhiwa eneo lake.

11. Usikilizaji wa Hadharani Kuhusu wananchi kuchomewa makazi yao Nyamuma

THBUB ilifanya usikilizaji wa hadharani kuhusu kuondolewa kwa nguvu na uharibifu wa mali bila kulipwa fidia kulikofanywa na mamlaka ya Serikali kwa wananchi wakazi wapatao 135 wa eneo la Nyamuma waliokuwa wameamriwa kuondoka eneo hilo. Zoezi la kuondolewa kwa nguvu lilitekelezwa kwa kuchomwa moto nyumba

za watu chini ya usimamizi wa uongozi wa serikali ya Wilaya ya Serengeti

Masuala Yaliyojitokeza Wakati wa Uchunguzi

Usikilizaji wa hadharani wa Nyamuma ulihusisha jumla ya wanakijiji 133 kama mashahidi wa upande wa walalamikaji na watu 33 kama mashahidi kwa upande wa serikali. Shuhuda na maelezo yaliyotolewa yalibaini yafuatayo:

(i) Kijiji cha Nyamuma ambacho walalamikaji walikuwa wanaishi ilikuwa ni sehemu ya kijiji halali cha Nyamuma kilichosajiliwa na Msajili wa Vijiji kwa Hati Na. 7 ya mwaka 1993;

(ii) Zoezi la kuwaondoa kwa nguvu na kuwachomea nyumba zao na mali zingine wananchi wa kijiji cha Nyamuma lilikiuka misingi ya utawala bora;

(iii) Zoezi la kuwaondoa kwa nguvu wananchi hao halikuzingatia sheria na utu wa watu;

(iv) Uondoaji wa watu uliambatana na uvunjwaji wa haki za binadamu kama vile haki ya kumiliki mali, haki ya faragha na haki ya kuishi katika mazingira na maisha bora; na

(v) Matumizi mabaya ya madaraka miongoni mwa watendaji na maafisa wa Serikali.

Mapendekezo

Kutokana na masuala yaliyojitokeza wakati wa uchunguzi, Tume ilipendekeza yafuatayo:-

(i) Waathirika kupewa maeneo mbadala;

(ii) Kuwepo malipo ya fidia halali na stahiki;

(iii) Utoaji wa misaada ya kiutu ikiwemo chakula, makazi, matibabu na huduma ya elimu kwa watoto hadi hapo walalamikaji watakaporejea katika maisha yao ya kawaida; na

(iv) Uzingatiwaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika zoezi kama hili kwa siku zijazo.

Mapendekezo hayo hayakutekelezwa na mamlaka husika na ndipo Asasi isiyo ya Kiserikali ambayo ni Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ilifungua kesi Mahakama Kuu kuomba utekelezaji wa mapendekezo ya Tume

2.2.4.3. Malalamiko Yaliyofanyiwa Usuluhishi na Upatanishi

Tume imepewa mamlaka ya kufanya usuluhishi na upatanishi kuhusu malalamiko yanayowasilishwa mbele yake kama itahitajika kufanyika hivyo kulingana na

kifungu cha 28(4) cha Sheria ya Tume Sura ya 391. Baadhi ya malalamiko yaliyofanyiwa usuluhishi na upatanishi katika kipindi cha miaka 20 ni kama ifuatavyo:-

1. **Lalamiko Na. UB/S/36/07/08/MWZ**

   Lalamiko hili lilihusu mkazi mmoja aliyelalamikia kiwanda fulani kwa kuelekeza mfereji wa maji yaliyokuwa na kemikali kwenye shamba lake na kusababisha uchafuzi wa mazingira.

   Tume ilisuluhisha mgogoro huo kwa kuzikutanisha pande zilizohusika na kumwezesha Mlalamikaji kulipwa fidia ya Tsh **2,500,000/=**

2. **Lalamiko Na. HB/S/1837/2016/2017/GGM**

   Lalamiko hili lilihusu wananchi 71 wa Kitongoji fulani waliolalamikia kutolipwa fidia stahiki za mashamba, nyumba na mazao baada ya maeneo yao kutwaliwa na Kampuni moja ya Uchimbaji Madini.

   Tume kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya husika, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa na Wananchi walikutana kwa pamoja na kufanya usuluhishi na upatanishi. Ilibainika kuwepo kwa uelewa mdogo miongoni mwa Wananchi kuhusu taratibu za umiliki wa ardhi na ulipaji wa fidia pale ardhi inapotwaliwa. Tume ilipendekeza kwa

mamlaka za wilaya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu sheria, kanuni na taratibu za ulipaji fidia na viwango vya fidia kwenye eneo husika.

2.3. Matumizi ya TEHAMA 2001- 2022

Katika kipindi tajwa Tume imeendeleza matumizi ya mifumo mbalimbali ya TEHAMA ikiwemo mifumo ya mawasiliano na utendaji wa shughuli za kila siku za Tume. Ofisi zote za Tume zimeunganishwa katika mtandao wa intaneti ambapo zinatumia huduma ya intanenti kupitia Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL).

Mifumo Mahsusi ilianzishwa na Tume kwa lengo la kutoa huduma ukiwemo Mfumo wa utendaji wa shughuli za kila simu za Tume (*Complaints Management Information System*) ulioanza kutumika kwa mara ya kwanza mwaka 2010. Mnamo mwaka 2012, mfumo huu ulihuishwa kwa kuongeza mfumo mdogo (module) iliyoruhusu upokeaji wa malalamiko kwa njia ujumbe mfupi wa simu (short messages).

Aliyekuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Anne Makinda akizindua rasmi mfumo wa kisasa wa kielektroniki wa utendaji wa shughuli za kila siku za Tume, Viwanja vya Karimjee Desemba 10, 2010, huku aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume, Mhe. Amir Manento akishuhudia.

Hata hivyo, kutokana na teknolojia iliyotumika katika kutengeneza mfumo huo na kuwepo kwa changamoto za matumizi ya mfumo husika, Tume ilitengeneza mfumo mpya unaoitwa *Complaints Management Information System* (CMIS) ambapo mahitaji yalitolewa na Tume kisha usanifu na utengenezaji ulifanywa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA).

Usanifu na utengenezaji wa mfumo wa CMIS ulianza Juni, 2019 na kukamilika Julai, 2020. Mfumo ulifanyiwa majaribio ya kina kwa kipindi cha Disemba 2020 hadi Februari 2021. Aidha, tofauti na mfumo wa zamani na huu mpya ni kuwa, unatumika katika ofisi zote za Tume na unafikika kwa

kutumia mtandao mahali popote, wakati ule wa kwanza ulikuwa unatumika ofisi za makao makuu pekee. Mfumo huu umehifadhiwa katika kituo cha kutunzia kumbukumbu cha Serikali (eGov data centre).

Matumizi ya mifumo yameleta mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo:

a) Kuwawezesha wananchi kuwasilisha na kufuatilia malalamiko masaa 24/7 popote walipo bila kujali aina ya simu walizonazo (smart phone, feature phone and computers);

b) Kurahisisha ufuatiliaji wa malalamiko ambapo mlalamikaji anaweza kupewa taarifa anazohitaji bila kusubiri muda mrefu kwani taarifa zote zinapatikana kwenye mfumo;

c) Kupunguza gharama za uendeshaji na hivyo kuongeza tija katika utoaji wa huduma pamoja na kuwapunguzia wananchi gharama zisizokuwa za lazima za kusafiri kuifuata ofisi ya Tume ilipo;

d) Kuziwezesha ofisi zote za Tume kutumia mfumo na majalada ya malalamiko kupatikana katika mfumo kwenye ofisi zote za Tume; na

e) Kurahisisha upatikanaji wa takwimu.

2.4. Elimu kwa Umma, Mafunzo, Ufuatiliaji na Tafiti

Ibara ya 130(1)(c)(d) na (g) ya Katiba ya Jamhuri ya Muugano wa Tanzania 1977 na Kifungu cha 6(1)(c)(d) na (j) cha Sheria ya Tume Sura ya 391, vinaipa Tume mamlaka ya kufanya utafiti, kutoa elimu kwa umma; na kuishauri Serikali, taasisi nyingine za umma na sekta

binafsi kuhusu masuala yanayohusiana na haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini.

Tume kwa kipindi husika imetekeleza jukumu lake la kukuza, kuhamasisha na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini kwa kutoa elimu kwa umma, mafunzo kwa wadau mbalimbali, na kufanya tafiti na ufuatiliaji kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

2.4.1. Elimu kwa Umma

Katika kipindi chake cha miaka 20 Tume ilitekeleza yafuatayo:-

(i) Kufanya ziara za uhamasishaji katika mikoa na wilaya zote za Tanzania Bara ambapo mikutano ya hadhara ilifanyika katika baadhi ya vijiji; shule za msingi, sekondari na vyuo. Pia elimu ilitolewa kwenye magereza, Mahabusu za Watoto na vituo vya Polisi kwenye mikoa na wilaya iliyotembelewa;

(ii) Kutayarisha na kusambaza bure machapisho mbalimbali ya elimu kwa umma kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora. Jumla ya nakala **2,843,700** za machapisho zilisambazwa ikiwemo: vipeperushi **(2,300,000)**, mabango **(10,500)**, vijitabu **(453,200)**, majarida **(66,000)** na fulana zenye jumbe za haki za binadamu na utawala bora **(14,000)**. Kijitabu cha ***'Mwananchi tambua haki zako na wajibu wako'*** chenye kutoa maelezo mafupi kuhusu

Tume, na haki na wajibu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ***'Mambo 101 Unayohitaji Kuyafahamu Kuhusu Polisi Lakini Unaogopa Kuyauliza'*** kinachoeleza majukumu ya jeshi la polisi, namna Jeshi la Polisi linavyofanya kazi na kuainisha haki za mwananchi anapokutana na Askari Polisi na Kijitabu cha ***'Mwongozo wa Utawala Bora'*** kinachofafanua dhana, misingi na faida za utawala bora pamoja na uhusiano baina yake na haki za binadamu ni baadhi ya mifano ya machapisho ambayo yametolewa na Tume kwa Wananchi kuwezesha kuwapatia elimu kuhusu masuala mbalimbali;

(iii) Kutayarisha na kurusha vipindi mbalimbali vya redio na televisheni vilivyolenga kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu Tume, haki za binadamu na utawala bora na kutoa makala na taarifa kupitia magazeti na mitandao ya kijamii. Katika kipindi hiki takriban vipindi **360** vya redio na **120** vya televisheni viliandaliwa na kurushwa kupitia vyombo vya habari Tanzania Bara;

(iv) Katika kipindi hiki, msisitizo umekuwa kutoa elimu kwa kutumia redio jamii, kwa kuwa wananchi wengi wako vijijini ambako redio hizo zinasikika na kupata taarifa kwa urahisi;

(v) Kushiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa kama vile: Wiki

ya Serikali za Mitaa; Wiki ya Sheria; Biashara ya Kimataifa “Saba Saba”; Wiki ya Wakulima “Nane Nane”; na Wiki ya Utumishi wa Umma. Kupitia ushiriki wa Wiki ya Utumishi wa Umma, Tume mwaka 2009 na 2010 mfululizo ilitunukiwa vyeti vya kutambuliwa kama Taasisi Bora ya Umma katika Uendeshaji na Utoaji Huduma. Tume imetumia fursa za maonesho hayo kupokea malalamiko, kutoa huduma za kisheria na elimu kwa wananchi wanaofika kwenye mabanda yake. Aidha, Tume ilipata zawadi kwa kuwa mshiriki bora katika maonesho ya Kimataifa ya Taasisi za Ombudsman (International Ombudsman Exhibition) yaliyofanyika Abuja Nigeria kuanzia tarehe 28-31 Oktoba 2019

(vi) Kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Elimu ya Haki za Binadamu 2011 – 2016, kuendesha mafunzo ya wawezeshaji wa elimu ya haki za binadamu na utawala bora, na kuanzisha klabu za haki za binadamu katika shule za msingi, sekondari na vyuo. Jumla ya klabu **323** zimeanzishwa katika baadhi ya mikoa Tanzania Bara ambapo Shule za Msingi **(klabu 54)**, Sekondari **(253),** Vyuo vya Ualimu **(12)**, Vyuo vya Kati **(1)** na Vyuo vya Elimu ya Juu **(3)**. Tume imekuwa ikifanya ziara za mara kwa mara kufuatilia uhai wa klabu hizo na kuongea na wanachama, walimu walezi na uongozi wa taasisi hizo.

Aliyekuwa Kamishna Msaidizi wa THBUB, Mhe. Fahamu Mtulya (kushoto) pamoja na Maafisa Waandamizi wa Tume, Bwana Phillip Sungu (katikati) na Bwana Germanus Kyafula wakifurahia tuzo za mshindi wa tatu wa taasisi bora ya umma katika uendeshwaji na utoaji huduma wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma Juni 23, 2010 CCM Kirumba, Mwanza.

Kupitia afua hii Tume inalenga kuongeza uelewa wa wanafunzi na walimu kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora ili wawe chachu ya mabadiliko na mabalozi wazuri wa masuala ya haki za binadamu na utawala bora katika jamii.

(vii) Kuandaa na kutoa matamko juu ya masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika jamii kwa lengo la kufahamisha, kuelimisha, kupongeza, kuonya na kukemea mienendo inayovunja haki za binadamu na kukiuka misingi ya utawala bora, ambapo jumla ya

matamko **120** yalitolewa kupitia vyombo vya habari; na

(viii) Kupitia Tovuti ya Tume (www.chragg.go.tz) na mitandao yake ya kijamii ya twitter (chraggtanzania), facebook (chragg.tanzania), na instagram (chraggtanzania) Tume iliongeza uelewa wa umma kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

2.4.2. Mafunzo kwa Wadau Mbalimbali

Tume ilitoa mafunzo ya haki za binadamu na utawala bora kwa makundi mbalimbali katika jamii wakiwemo:- viongozi na maafisa kutoka Mahakama, Kamati za Bunge, TAMISEMI, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Taasisi za Dini, Vyombo vya Habari na Asasi za Kiraia (AZAKi). Uhamasishaji huo ulifanyika kupitia mikutano, semina na warsha.

Katika kipindi cha miaka ishirini (20) Tume kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendesha mafunzo mbalimbali kwa watumishi wake ili kuwajengea uwezo na weledi katika kutekeleza majukumu yao hasa katika masuala ya utatuzi na usuluhisho wa migogoro, mbinu bora za uchunguzi, uandishi wa taarifa, maarifa ya utafiti, elimu ya kujitambua na UKIMWI, mafunzo ya utawala bora na haki za makundi maalum.

Mafunzo mengine yalihusu matumizi ya mifumo mbalimbali kuwezesha kurahisisha utendaji kazi. Mafunzo hayo yalihusisha mifumo ya taarifa za Kiutumishi na Mishahara kwa Idara ya Utawala na Rasilimali watu; Kitengo cha Uhasibu na Fedha kuhusu mfumo wa MUSE; Kitengo cha Ugavi na Manunuzi kuhusu mfumo wa TANePS, GAMIS, MUSE na GIMIS; na Idara ya Malalamiko na Uchunguzi kuhusu mfumo wa kusimamia utendaji wa shughuli za Tume (CMIS).

Mafunzo hayo yalitolewa kwa kutumia vitini na miongozo **24** kama nyenzo za kutolea elimu na ufuatiliaji wa masuala ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa wawezeshaji, watetezi wa haki za binadamu na watendaji. Baadhi ya vitini na miongozo hiyo ni pamoja na:- Mwongozo wa Ufuatiliaji wa Haki ya Mtoto; Ufuatiliaji wa Haki za Binadamu; Mwongozo kwa Wawezeshaji wa Elimu ya Haki za Binadamu; Elimu ya Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora; Sheria na Kanuni kwa Watekelezaji wa Sheria; Taratibu Rahisishwa za Uzingatiaji wa Haki za Binadamu miongoni mwa Taasisi za Sekta ya Sheria – katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza; na Elimu ya Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora kwa Viongozi wa Serikali za mitaa katika ngazi ya Kata.

Mafunzo hayo yamechangia kuongeza uelewa kwa watumishi wa umma, katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kutatua kero za wananchi kwa kuzingatia haki za binadamu, misingi ya utawala bora, sheria na taratibu. Hali hiyo imechangia

wananchi kufurahia haki zao kutokana na huduma zinazotolewa na Serikali.

Tume inaamini kuwa wanufaika wa mafunzo watakuwa chachu katika kuelimisha umma kuhusu mifumo sahihi ya kutoa taarifa na kudai haki zao wanapobaini kuwa zimevujwa au misingi ya utawala bora imekiukwa.

2.4.3. Tafiti na Ufuatiliaji wa Masuala ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

THBUB, imefanya tafiti mbalimbali kuhusu hali ya haki za binadamu na utawala bora nchini. Kwa ujumla malengo ya tafiti hizo ilikuwa ni kubaini vyanzo vya matukio ya uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora, athari zake na hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika kuboresha changamoto zilizojitokeza. Baadhi ya tafiti na chunguzi za hadharani ni kama ifuatavyo na:-

(i) Utafiti na Uchunguzi wa Hadharani Kuhusu Mauaji dhidi ya Watu wenye Ualbino, Wanawake, Wazee (“Vikongwe”) mwaka 2009;

(ii) Utafiti Kuhusu Vitendo vya Ukatili Vinavyofanywa na Vyombo vya Usimamizi wa Sheria, 2010;

(iii) Utafiti Kuhusu Upatikanaji wa Maji Safi na Salama kwa Makundi Maalum 2020;

(iv) Uchunguzi wa Hadharani Kuhusu Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji Dhidi ya Watoto; 2006

2.4.3.1. Utafiti na Uchunguzi wa Hadharani Kuhusu Mauaji dhidi ya Watu wenye Ualbino na Wanawake Wazee

Tume ilifanya utafiti na uchunguzi huo mwaka 2009 katika wilaya 16 za Tanzania Bara.[6] Utafiti huu ulitokana na hali ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora kuingia dosari baada ya kuibuka wimbi la mauaji ya kikatili dhidi ya watu wenye ualbino na mauaji ya wanawake wazee (waliokuwa wanajulika kama “vikongwe”.

Katika utafiti na uchunguzi huo Tume ilibaini kuwa mauaji hayo yalisababishwa na:- imani za kishirikina; elimu ndogo ya afya; urithi wa mali[7], ukatili wa kijinsia, mila potofu, ramli chonganishi na utekelezaji wa mauaji kama ajira kwa kundi fulani la watu.

Kuhusu mauaji ya watu wenye ualbino, ilibainika kuwa yalichangiwa na muunganiko wa sababu mbalimbali zinazotegemeana na kuwa hakuna sababu moja pekee inayoelezea kiini cha mauaji hayo. Miongoni mwa sababu zilizoainishwa ni pamoja na:- imani za kishirikina; waganga wa jadi; mtazamo hasi wa jamii dhidi ya watu wenye ualbino; umaskini; na uelewa mdogo kuhusu sheria na haki za binadamu.

[6] Wilaya hizo ni Misenyi, Muleba, Biharamulo, Ngara, Geita, Sengerema, Kwimba, Magu, Misungwi, Bukombe, Kahama, Bariadi, Bunda, Musoma, Mbarali na Mbozi

[7] Wengi wa wanawake hawa huwa wamefiwa na waume zao hawana hifadhi ya jamii, kutopata hifadhi na matunzo kutoka kwa watoto wao na wamerithi mali walizochuma na waume zao kama mashamba na mifugo.

Katika ufuatiliaji huo ilibainika kuwepo changamoto mbalimbali katika kushughulikia tatizo hili ikiwemo:- wananchi kutokuwa na uelewa wa sheria na taratibu hasa katika kutoa ushahidi, vyombo vya kutekeleza sheria kama Polisi na Mahakama kuchelewa kuchukua hatua na kukamilisha taratibu za kisheria katika kuifikia haki.

Tume iliandaa taarifa na kutoa mapendekezo ikiwemo kuishauri Serikali, Viongozi wa Dini na wa Kimila, AZAKi na Vyombo vya habari kutoa elimu na vyombo vya kusimamia sheria kukamilisha taratibu za kusimamia haki kwa wakati. Mapendekezo hayo yalisaidia Serikali kuchukua hatua madhubuti kukomesha vitendo vya ukatili na mauaji ya watu wenye ualbino na wanawake wazee ambapo kwa sasa vimepotea.

2.4.3.2. Ufuatiliaji wa Chaguzi 2005 – 2020

Tume imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa Uchaguzi Mkuu, na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa nyakati tofauti kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka 2020.[8] Tume ilifuatilia zoezi la kujiandikisha na uboreshaji wa daftari la kudumu la mpiga kura, mikutano ya kampeni na uangalizi siku ya kupiga, kuhesabu na kujumlisha kura na utangazaji matokeo ya uchaguzi.

Malengo ya ufuatiliaji huo yalikuwa ni kutathmini uzingatiaji wa haki za binadamu na misingi ya

[8] Uchaguzi Mkuu 2005, 2010, 2015 na 2020 na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2019

utawala bora kwenye chaguzi hizo na kutoa mapendekezo kwa mamlaka husika kuhusu changamoto zilizojitokeza katika masuala ya haki za binadamu na utawala bora kwenye chaguzi hizo.

Katika chaguzi hizo changamoto zifuatazo zilibainika:-

(i) Kutokuwepo kwa wataalam wa lugha za alama kwa watu wenye ulemavu wa kusikia katika mikutano ya kampeni;

(ii) Baadhi ya vituo vya kupigia kura kutofikika kwa urahisi kwa watu wenye ulemavu;

(iii) Kuchanwa kwa orodha ya majina ya wapiga kura kwenye baadhi ya vituo na hivyo kusababisha usumbufu kwa baadhi ya wapiga kura;

(iv) Vifaa vya kupigia kura kutokufika kwa wakati katika baadhi ya vituo;

(v) Mwitikio mdogo wa wananchi kushiriki zoezi la kupiga kura hasa uchunguzi wa mwaka 2020;

(vi) Mikutano ya kampeni za uchaguzi kuanza kabla ya rufaa za wagombea kujibiwa;

(vii) Mawakala wa vyama vya siasa kutokuwa na barua za uteuzi na kuchelewesha kuwaapisha kwa wakati;

Taarifa zenye mapendekezo ziliandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika kwa utekelezi. Baadhi ya mapendekezo hayo ni:-

(i) Msajili wa Vyama vya Siasa kuvitaka vyama vya siasa kutumia wataalam wa lugha za alama kwenye mikutano ya kampeni;

(ii) Tume ya Uchaguzi kwa kushirikiana na wadau wengine kufanya utafiti ili kufahamu kinachosababisha wananchi wengi kutopiga kura licha ya kujiandikisha;

(iii) Tume ya Uchaguzi kuwa na mkakati endelevu wa kutoa elimu ya mpiga kura kwa wananchi;

(iv) Tume ya Uchaguzi kuandaa kikao cha wadau kufanya tathmini ya mchakato wa uchaguzi wa mwaka 2020 kwa ajili ya kuboresha chaguzi zijazo; na

(v) Tume ya Uchaguzi kuhakikisha kuwa vifaa vya kupigia kura vinafika vituo vya kupigia kura kwa wakati.

2.4.3.3. Ufuatiliaji wa Haki za Watu Wenye Ulemavu

Tume ilifanya ufuatiliaji wa Haki za Watu Wenye Ulemavu wanaoishi kwenye mazingira magumu mitaani na wanaosoma vyuo vikuu nchini, mwaka 2019. Ufuatiliaji huo ulifanyika katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Wilaya ya Arusha Mjini, Wilaya ya Kinondoni, Kigamboni, Temeke na Ilala. Aidha ufuatiliaji wa hali ya haki ya elimu kwa watu wenye ulemavu kwa

wanafunzi ulifanywa katika vyuo vitano (5)[9] vya elimu ya juu katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Katika ufuatiliaji huo Tume ilibaini yafuatayo:-

(i) Mtazamo na uelewa mdogo wa jamii kuhusu haki za watu wenye ulemavu hali inayosababisha kudharauliwa, kutelekezwa, kutukanwa na kunyanyapaliwa;

(ii) Kufukuzwa na kuondolewa kwa nguvu na viongozi wa serikali, kukamatwa na kuwekwa rumande na Askari Polisi na kulipishwa faini ya shilingi 50,000/=;

(iii) Upungufu wa vifaa saidizi, uhaba wa wahadhiri na walimu wenye ujuzi kwenye taasisi hizo;

(iv) Baadhi ya taasisi kutokuwa na miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu na kutokuwepo kwa uwiano wa ajira kwenye taasisi za umma na binafsi.

Taarifa iliandaliwa pamoja na mapendekezo na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika. Aidha, baadhi ya mapendekezo yaliyowasilishwa yalikuwa:-

(i) Halmashauri ziendelee kutekeleza Sheria ya Watu wenye Ulemavu Sura ya 183 na Sheria ndogondogo kwa ajili ya haki,

[9] Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi ya Dar es Salaam (MDCC), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Chuo Kikuu Arusha (ARU) na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE).

maslahi na wajibu kwa watu wenye ulemavu;

(ii) Serikali iendelee kuliwezesha kifedha Baraza la Ushauri la Taifa la Watu Wenye Ulemavu ili liweze kutekeleza majukumu yake na kuvijengea uwezo kiuchumi vikundi vya watu wenye ulemavu;

(iii) Serikali iendelee kuboresha na kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu ili kuweza kufika kwenye majengo, barabara na kuhuisha mipango endelevu ya kutoa vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu nchini;

(iv) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Taasisi za Elimu ya Juu zichukuwe hatua kuhakikisha kuwa watumishi wanaohusika katika utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu wanapata mafunzo ya kitaalam kwa ajili ya kuwahudumia watumishi na wanafunzi wenye ulemavu;

(v) Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iendelee kusimamia uwiano wa ajira kwa kuzingatia asilimia 3 ya watu wenye ulemavu wanaoajiriwa katika sekta ya umma.

2.4.3.4. Uchunguzi wa Hadharani kuhusu Tatizo la Mimba na Ndoa katika Umri Mdogo

THBUB ilifanya uchunguzi wa hadharani kuhusu tatizo la Mimba na Ndoa katika Umri Mdogo katika Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Lindi mwaka 2018/2019.

Malengo ya uchunguzi yalikuwa ni pamoja na:- kutathmini ukubwa wa tatizo, vyanzo vyake, athari zake na hatua za kuchukua katika kukabiliana nalo.

Tume ilibaini kukinzana kwa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kuhusu umri wa mtoto ambapo sheria inaruhusu mtoto kuolewa katika umri wa miaka 14 na 15. Mifumo ya kisheria inayoridhia ndoa za utotoni ilishatolewa maamuzi katika kesi ya **Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Rebeca Gyumi Rufaa Na. 204 ya 2017**, kuwa kifungu cha 13 na 17 cha Sheria ya Ndoa vinabagua watoto kulingana na jinsia ambapo inavunja kanuni ya usawa kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 12 (1) na 13 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Jedwali Na. 14: Takwimu za Mimba Katika Umri Mdogo Katika Wilaya za Shinyanga Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ya Mji, 2016/2017 - 2019/2020

Halmashauri	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20	Jumla	Hatua
Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga	0	51	73	59	**183**	Mahakamani
Halmashauri ya Mji wa Shinyanga	6	21	25	38	**90**	Mahakamani
Jumla	**6**	**72**	**98**	**97**	**273**	

Chanzo: Taarifa ya Uchunguzi THBUB, 2019

Kati ya mwaka 2016 na 2019, jumla ya wasichana mia mbili sabini na tatu (**273**) ikiwa ni wasichana mia moja themanini na tatu (**183**) kutoka Halmashauri ya Wilaya Shinyanga na wasichana tisini (90) kutoka Halmashauri ya Mji Shinyanga walipata mimba. Hata hivyo, uchunguzi ulibaini kuwa kuanzia Julai 2018 hadi Juni, 2019 jumla ya wanafunzi mia moja na sitini na nane **(168**) walifukuzwa shule kutokana na mimba. Idadi hii ni kubwa ukilinganisha na jumla ya wanafunzi mia moja hamsini na nane (**158**) waliofukuzwa shule kutokana na tatizo hilo kwa kipindi cha mwaka 2016 hadi 2018 katika mkoa wa Shinyanga. Ilielezwa kuwa hatua mbalimbali zilichukuliwa katika kukabiliana na tatizo hili ambapo jumla ya matukio **246** yalifikishwa kwenye vyombo vya dola ikiwemo vituo vya polisi kwa ajili ya sheria kuchukua mkondo wake dhidi ya watuhumiwa.

Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2017 jumla ya wanafunzi **166** walipata mimba katika mkoa wa Lindi na kati ya mwaka 2013 hadi 2017 wanafunzi **239** walipata mimba katika mkoa wa Tabora kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini.

Jedwali Na. 15: Wanafunzi waliopata mimba kwa Shule za Msingi na Sekondari Mkoa wa Lindi 2015 - 2017

Halmashauri	Mimba kwa wanafunzi kuanzia mwaka 2015 - 2017						
	Shule za msingi			Shule za sekondari			Jumla
	2015	2016	2017	2015	2016	2017	
Kilwa	0	5	11	0	1	19	36
Wilaya ya Lindi	3	7	3	6	18	15	52
Lindi Mjini	1	5	2	1	5	5	19
Nachingwea	0	0	0	0	19	3	22
Liwale	0	1	2	5	8	10	26
Ruangwa	0	0	0	0	6	5	11
Jumla	**4**	**18**	**18**	**12**	**57**	**57**	**166**

Chanzo: Afisa Elimu Mkoa wa Lindi (2018).

Dawati la Jinsia na Watoto, Jeshi la Polisi liliendelea kushughulikia tatizo la mimba katika umri mdogo kwa kupeleleza na kufikisha mahakamani kesi za matukio hayo. Katika Mkoa wa Lindi kuanzia mwaka 2014 - 2018 jumla ya kesi **85** ziliripotiwa Polisi**.** Katika Mkoa wa Tabora kuanzia mwaka 2013 – 2017 kesi **239** zinazohusu mimba katika umri mdogo ziliwasilishwa Polisi kama inavyoonekana katika jedwali.

Jedwali Na.16: Mwenendo wa Kesi za Mimba Katika Umri Mdogo Zilivyoshughulikiwa na Jeshi la Polisi na Mahakama katika Mkoa wa Tabora, 2013 – 2017

Mwaka	Kesi zilizo pokelewa	Zilizo Shinda	Zilizoa-chiliwa Polisi	Zinazoendelea na upelelezi	Zilizoachiliwa Mahakamani	Zinazoe-ndelea Mahakamani
2013	5	5	-	-	-	-
2014	7	3	2	-	-	2
2015	9	3	4	-	-	2
2016	64	15	37	-	12	-
2017	154	13	32	84	9	16
JUMLA	**239**	**39**	**75**	**84**	**21**	**20**

Chanzo: Taarifa kutoka Jeshi la Polisi Mkoa wa Tabora mwaka 2018

Takwimu za mwenendo wa kesi zinaonesha kuwa kesi nyingi za mimba katika umri mdogo zinazofikishwa Polisi na Mahakamani hushindwa kuendelea kutokana na changamoto zifuatazo:-

(i) Wazazi kushirikiana na watuhumiwa kuyamaliza masuala hayo kifamilia na kutotoa ushahidi mahakamani;

(ii) Sheria ya Ndoa Sura ya 29 kuwa na vipengele vinavyoruhusu ndoa katika umri wa miaka 14 na 15;

(iii) Jamii kutokuwa na uelewa wa haki za mtoto, sheria na taratibu mbalimbali; na

(iv) Kuendelea kuwepo kwa mila potofu na desturi zinazowakandamiza wanawake na watoto wa kike.

Kupitia uchunguzi huu ilibainika kuwa mimba na ndoa katika umri mdogo husababishwa na umaskini katika ngazi ya familia, mmomonyoko wa maadili, vishawishi, ukatili wa kijinsia, umbali mrefu kati ya nyumbani na shuleni, athari za utandawazi,

mapungufu katika baadhi ya sheria[10], wazazi na walezi kutotimiza majukumu yao, imani za kishirikina[11], mila na desturi ambazo ni kandamizi.

Athari za mimba na ndoa katika umri mdogo ni pamoja na: kuacha shule; kupoteza fursa za maendeleo; kuongezeka kwa idadi ya vifo vya watoto wachanga na matatizo wakati wa kujifungua ikiwemo kupata fistula; kuongezeka kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia; ajira mbaya kwa watoto; unyanyapaa; kutoa mimba na biashara ya ngono; tatizo la mzazi mmoja na kuvunjika kwa familia; matatizo ya ulemavu na kukosekana kwa ulinzi na usalama wa mtoto.

Mapendekezo

Ili kukabiliana na tatizo la mimba za utotoni na ndoa katika umri mdogo, yalitolewa mapendekezo ambayo ni pamoja na:-

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu vyanzo, wahusika, athari na namna ya kukabiliana na tatizo la mimba na ndoa katika umri mdogo;

(ii) Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Jeshi la Polisi, Mahakama na AZAKi kuendeleza ushirikiano katika kukabiliana na tatizo la mimba na ndoa katika umri mdogo;

(iii) Serikali kuendeleza juhudi za kupitia na kurekebisha baadhi ya sheria zenye mapungufu na zinazokinzana na mikataba ya

[10] Kifungu cha 13 na 17 cha Sheria Sheria ya Ndoa ya Mwaka, 1971.
[11] Waganga wa Kienyeji kuwaogesha watoto kike kwa kutumia dawa za kimapenzi maarufu kama "samba" ili wapendwe na wanaume.

Kimataifa na Kikanda hususan kifungu cha 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa Sura ya 29;

(iv) Wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kutimiza majukumu yao katika malezi na makuzi ya watoto ikiwa ni pamoja na kuwafundisha tabia njema na maadili;

(v) Jamii, wazazi na walezi kuelimisha watoto kuhusu elimu ya afya ya uzazi, athari za kujihusisha na mapenzi katika umri mdogo na madhara ya mimba na ndoa za utotoni; na

(vi) Serikali kuendelea kuhamasisha wananchi kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi na Mahakama katika kushughulikia kesi za mimba na ndoa za utotoni.

2.4.3.5. Ufuatiliaji wa Haki za Binadamu na Biashara

Tume ilifanya tathmini ya hali ya haki za binadamu na biashara nchini kwa lengo la kubainisha hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Tanzania katika kutekeleza Mwongozo wa Kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za Binadamu.[12] Tathmini iliainisha mambo yaliyotekelezwa na Serikali na mapungufu yalijitokeza katika utekelezaji huo. Tathmini hii ni sehemu ya uliokuwa Mpango kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (2013 - 2017).

[12] Report on the National Baseline Assessment on Business and Human Rights (NBA on BHR) conducted under the project: "**Implementing the United Nations Guiding Principles on Business and Human Rights in Sub-Sahara Africa"**. CHRAGG, Business Human Rights Tanzania (BHRT) and Centre for Research on Multinational Corporations (SOMO) and the Danish Institute for Human Rights (DIHR). CHRAGG 2017

Katika ufuatiliaji huo Tume ilibaini yafuatayo:-

(i) Tanzania haina Mpango Kazi wa Kitaifa wa kushughulikia masuala ya biashara na haki za binadamu;

(ii) Uelewa mdogo kuhusu masuala ya haki za binadamu na biashara miongoni mwa wadau mbalimbali, wakiwemo Serikali, wafanyabiashara, na wananchi kwa ujumla;

(iii) Kuwepo mkanganyiko katika kuhusisha mifumo ya kisheria, kisera na kitaasisi katika kufuatilia utekelezaji wa Mwongozo wa Kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za Binadamu;

(iv) Serikali kutosaini makubaliano ya Kanuni za Hiari kuhusu Usalama na Haki za Binadamu,[13] na kutotoa msimamo wake kuhusu Kanuni za Kimataifa za Kinidhamu kwa ajili ya watoa huduma wa makampuni binafsi ya ulinzi. Kanuni hizi zinasisitiza uzingatiwaji wa haki za binadamu wakati makampuni binafsi ya ulinzi na vyombo vya ulinzi vya Serikali vinapotekeleza majukumu yake;

(v) Serikali haijachukua hatua kutekeleza Kanuni za Hiari za Shirika la Chakula na Kilimo Duniani za Mwongozo kuhusu Uwajibikaji katika Matumizi ya Ardhi, Uvuvi na Mifugo

[13]Secretariat for the Voluntary Principles on Security and Human Rights (2016), Government and voluntary principles on security and human rights, http://www.voluntaryprinciples.org/for-governments/ (last accessed 25 July 2017)

katika Muktadha wa Usalama wa Chakula[14] na Kanuni za Umoja wa Afrika kuhusu Utwaaji wa Ardhi;

(vi) Serikali kutochukua hatua thabiti kuwahimiza wawekezaji kuzingatia viwango vya kimataifa vilivyowekwa, kwa mfano viwango vya Kimataifa vya Baraza la Uchimbaji Madini na Metali, au Viwango vya Utendaji vya Shirika la Fedha la Kimataifa.

Mapendekezo ya kuboresha haki za binadamu na biashara nchini

(i) Serikali ianze kufanya mchakato wa kuandaa Mpango Kazi kuhusu Haki za Binadamu na Biashara, na kwa kushirikiana na wadau ifanye kampeni ya kuelimisha umma kuhusu masuala hayo;

(ii) Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na THBUB, iainishe, kupitia na kufanyia marejeo sheria na sera zinazohusu masuala ya haki za binadamu na biashara ili ziendane na matakwa ya Miongozo ya Umoja wa Mataifa kuhusu haki za binadamu na biashara;

(iii) Serikali iainishe na kutoa kwa umma taarifa za vipindi maalum vya utekelezaji wa sheria ya uwazi na uwajibikaji ya mwaka 2015;

[14] Food and Agriculture Organization of the United Nations (2012) Responsible governance of tenure of land, fisheries and forests in the context of national food security, http://www.fao.org/docrep/016/i2801e/i2801e.pdf (last accessed 25 July 2017)

(iv) Serikali isaini makubaliano ya Kanuni za Hiari kuhusu Usalama na Haki za Binadamu, Kanuni za Kimataifa za Kinidhamu kwa ajili ya Watoa Huduma wa Makampuni Binafsi ya Ulinzi, Kanuni za Hiari za Shirika la Chakula na Kilimo Duniani na Miongozo kuhusu Uwajibikaji katika Matumizi ya Ardhi, na kuzitekeleza, ikiwa ni pamoja na kutoa miongozo kuhusu utekelezaji wake kwa makampuni ya biashara na kwa wadau wengine muhimu; na

(v) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya na Serikli ya Mapinduzi Zanzibar ziimarishe utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa viwango vya kimataifa, kikanda na kitaifa kwa watu wote wanaotaka kuwekeza hapa nchini. Kwa wawekezaji wa kigeni kutakiwa kuzingatia viwango vya kimataifa kama sharti katika kuwekeza.

2.5. Uchunguzi wa Hadharani Kuhusu Migogoro ya Ardhi

Ibara ya 130(1)(c)(d) na (g) ya Katiba ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6(1)(c)(d) na (j) cha Sheria ya Tume, Sura ya 391, vinaipa Tume mamlaka ya kufanya utafiti, uchunguzi na kuishauri serikali na taasisi nyingine za umma na sekta binafsi kuhusu masuala yanayohusiana na haki za binadamu na misingi ya utawala bora nchini. Katika kipindi cha miaka 20 tangu kuanzishwa kwake Tume ilifanya uchunguzi kuhusu migogoro ya ardhi katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Ruvuma, Iringa, Pwani na Morogoro, Kagera, Mwanza, Geita, Manyara,

Rukwa, Tanga, Shinyanga, Mara, Njombe, Katavi, Pwani, Tabora, Singida na Kigoma.

Uchunguzi wa hadharani ulilenga: kujua sababu za kuwepo kwa migogoro hiyo na athari zake; kutathmini hatua zilizochukuliwa na wananchi, serikali au taasisi zenye mamlaka ya utatuzi wa migogoro; na mapendekezo ya wananchi katika suluhu za migogoro ya ardhi. Aidha, Tume ilitoa pia elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu, misingi ya utawala bora, sera na sheria za umiliki na matumizi ya ardhi na mifumo ya kupokea na kusuluhisha migogoro.

Kamishna wa Tume, Mhe. Mohamed H. Khamis akitoa elimu katika Kijiji cha Sanya Station Wilaya ya Hai Mkoani Kilimanjaro wakati wa uchunguzi wa hadharani uliofanyika kijijini hapo kuhusu migogoro ya ardhi. Chanzo THBUB 2017

2.5.1. Aina ya Migogoro ya Ardhi

Uchunguzi ulibaini aina mbalimbali za migogoro ya ardhi ikiwemo: Migogoro ya Mipaka Migogoro kati ya Hifadhi za Taifa na Wananchi; Migogoro baina ya Taasisi za Serikali na wananchi; Migogoro kati ya Wawekezaji na Wananchi; na Migogoro kati ya Wakulima na Wafugaji.

2.5.2. Vyanzo vya Migogoro ya Ardhi

Tume ilibaini vyanzo vya migogoro hii ni:

(i) Matumizi mabaya ya madaraka;
(ii) Kutokuwepo kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi;
(iii) Mila na desturi kandamizi;
(iv) Ongezeko la idadi ya watu na mifugo;
(v) Upanuzi wa Hifadhi za Taifa, Mapori Tengefu na Mapori ya Akiba;
(vi) Wananchi kutoshirikishwa katika maamuzi ya utwaaji wa maeneo, umiliki na matumizi ya ardhi
(vii) Wawekezaji katika sekta ya ardhi kutoendeleza maeneo yao; na
(viii) Rushwa.

2.5.3. Athari za Migogoro ya Ardhi

Migogoro ya umiliki na matumizi ya ardhi imesababisha athari mbalimbali miongoni mwa jamii hapa nchini. Athari hizo ni pamoja na; vifo, uharibifu wa mali kutokana na uchomaji moto wa nyumba, magari, mashamba, maghala ya mazao; wananchi kuhama makazi yao; uharibifu wa miundo mbinu ya kijamii na kudorora kwa shughuli za uzalishaji mali kama vile ufugaji na kilimo. Athari nyingine ni uharibifu wa mazingira, madhara ya kiakili na kisaikolojia na migongano katika familia, koo na jamii kwa ujumla.

Uharibifu wa mali uliosababishwa na mapigano ya wakulima na wafugaji

Picha hapo juu inaonyesha eneo la Mtanzania wilayani Kiteto ambalo ni moja kati ya maeneo ya makazi yaliyovamiwa na kuchomwa moto na watu wanaodaiwa kuwa wafugaji ambapo watu watatu waliuawa: Chanzo Taarifa ya THBUB ya Ufuatiliaji wa Migogoro ya Ardhi mwaka 2017.

2.5.4. Mapendekezo

2.5.4.1. Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na TAMISEMI

(i) Kuwa na mipango endelevu ya kuelimisha wananchi na viongozi kuhusu Sheria za Ardhi, Sura ya 113 na 114;

(ii) Kuweka kipaumbele katika upimaji wa ardhi yote nchini kwa kuzingatia sheria zilizopo;

(iii) Kuhakikisha Idara za Ardhi katika Halmashauri zote nchini zina watumishi wa kutosha na vitendea kazi bora;

(iv) Kutenga fedha kwa ajili ya kuanzisha mfuko wa fidia ya ardhi;

(v) Kudumisha mahusiano mema ya kiutawala na ujirani mwema kati ya kijiji na

kijiji, wilaya na wilaya na mkoa na mkoa; na

(vi) Vijiji vyenye Mipango ya Matumizi Bora ya ardhi vihimizwe kutekeleza mipango hiyo ili kupunguza migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji na ambavyo havina vihimizwe kuwa na mipango hiyo.

2.5.4.2. Wizara ya Mali Asili na Utalii na Taasisi Zilizo Chini Yake

(i) Kuwashirikisha kikamilifu wananchi katika maamuzi mbalimbali yenye maslahi kwa umma;

(ii) Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009 ifanyiwe mapitio upya kwani maeneo ya Mapori Tengefu mengi yako ndani ya maeneo ya vijiji;

(iii) Kudumisha uhusiano mwema na vijiji vinavyozunguka hifadhi;

(iv) Kulipa fidia stahiki kutokana na madhara yanayosababishwa na wanyama pori.

2.6. Uandaaji na Uwasilishaji wa Taarifa za Tume

THBUB ina jukumu la kuandaa Taarifa ya Mwaka na Taarifa Maalum[15] kuhusu hali ya haki za binadamu na utawala bora nchini. Taarifa hizo zinahusu utekelezaji wa majukumu yake ya kutetea, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu.

[15] Kifungu cha 33 na 34 cha Sheria ya Tume Sura ya 391

Ibara ya 131 (3) (a) na (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, ikisomwa pamoja na kifungu cha 33 (1) (a), (b) na (c) cha Sheria ya Tume Sura ya 391 vinatoa wajibu kwa THBUB kutayarisha na kuwasilisha kwa Mawaziri wenye dhamana ya masuala ya haki za binadamu taarifa kuhusu shughuli za Tume katika mwaka uliotangulia na hali ya utekelezaji wa hifadhi ya haki za binadamu katika Jamhuri ya Muungano. Mawaziri hao huwasilisha taarifa hiyo mbele ya Bunge na Baraza la Wawakilishi mapema iwezekanavyo baada ya kupokelewa.

Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mizengo Pinda, akiangalia Taarifa Maalum ya Miaka 10 (2001 – 2011) ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) mara baada ya kuizindua. Wengine kutoka kushoto ni aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Mathias Chikawe na aliyekuwa Mwenyekiti wa THBUB Jaji Kiongozi Mstaafu, Mhe. Amiri Ramadhan Manento (kulia). (Chanzo: THBUB, 2012)

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2001 Tume imekuwa ikiandaa taarifa za mwaka zenye kuelezea hali ya haki za binadamu na utekelezaji wa majukumu yake. Katika kipindi cha miaka 20 ya THBUB, jumla ya taarifa 10 ziliwasilishwa bungeni ambapo taarifa ya mwisho ilikuwa ni ya mwaka 2010/2011 iliyowasilishwa katika Mkutano

wa Kumi na Moja, Kikao cha Arobaini na Tano tarehe 7 Juni, 2013. Tangu wakati huo taarifa kuhusu shughuli za Tume na hali ya utekelezaji wa hifadhi ya haki za binadamu nchini hazijapata nafasi ya kuwasilishwa Bungeni kama ilivyo matakwa ya Ibara ya 131(3) (a) na (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977. Hali hii imesababisha majukumu na kazi zilizotekelezwa na Tume kutofahamika kwa wananchi (visibility).

2.7. Maktaba ya Tume

Katika kipindi cha miaka 20 THBUB imefanikiwa kuanzisha maktaba yenye machapisho mbalimbali. Maktaba hii inatoa huduma kwa watumishi wa Tume, wanafunzi, watafiti na wananchi kwa ujumla kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

Mengi ya machapisho yaliyopo yalipatikana kutokana na ufadhili wa wadau wa maendeleo - DANIDA, UNICEF na USAID. Maktaba hii ina Kanzi data yake (Library data base) katika mfumo wa HURIDOCS.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, maktaba hii inakabiliwa na changamoto kama vile upungufu wa watumishi, uhaba wa vitendea kazi kama vile kompyuta na nafasi finyu ya kuhifadhia vitabu.

2.8. Ukaguzi wa Magereza, Vituo vya Polisi, Mahabusu za Watoto na Shule ya Maadilisho

Katika kipindi cha miaka 20 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2001, Tume imekuwa ikikagua magereza na sehemu nyingine wanamozuiliwa watu kwa mujibu wa Sheria ili kuona uzingatiwaji wa haki za binadamu na

misingi ya utawala bora katika vizuizi hivyo. Kifungu cha 6 (1) (h) cha Sheria ya Tume Sura ya 391.

THBUB ilifanikiwa kukagua takriban magereza na vituo vyote vya Polisi, Shule ya Maadilisho na Mahabusu za Watoto. Taarifa za Kaguzi hizo zenye mapendekezo zilitayarishwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika kwa utekelezaji. Baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na Tume yalitekelezwa na mengine hayajatekelezwa.

Jedwali Na. 17: Idadi ya magereza, vituo vya polisi, mahabusu za watoto na Shule ya Maadilisho vilivyokaguliwa tangu 2002-2022

NA	MWAKA	MAGEREZA	VITUO VYA POLISI	MAHABUSU ZA WATOTO	SHULE YA MAADILISHO
1.	2002/2003	45	-	-	-
2.	2003/2004	23	38	-	-
3	2004/2005	12	43	0	0
4	2005/2006	24	70	-	-
5	2006/2007	34	44	0	0
6	2007/2008	3	5	-	-
7	2008/2009	75	-	-	-
8	2010/2011	29	30	5	1
9	2012/2013	46	51	4	1
10	2013/2014	37	48	1	
11	2016/2017	41	40	5	1
12	2017/2018	30	32	-	-
13	2019/2020	21	14	1	1
14	2020/2021	14	28	2	-

CHANZO: Taarifa za THBUB

2.8.1. Changamoto Zilizobainika Katika Ukaguzi wa Magereza

Katika kaguzi zilizofanywa na THBUB, changamoto zifuatazo zilibainika:-

(i) Magereza mengi kuwa na idadi kubwa ya wafungwa na mahabusu kuliko uwezo wa majengo yaliyopo;

(ii) Baadhi ya magereza kuwachanganya watoto na watu wazima katika mabweni;

(iii) Matumizi ya mitondoo, uchakavu wa miundombinu, upungufu wa magodoro, mablanketi; na sare za wafungwa;

(iv) Wafungwa na mahabusu kulalamikia Polisi, Mahakama, Mkemia Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuhusu kutotekeleza majukumu yao kwa wakati kwa mujibu wa sheria;

(v) Uelewa mdogo wa wafungwa na mahabusu kuhusu haki za binadamu, utawala bora, Sera, miongozo na Sheria mbalimbali;

(vi) Uchache wa wataalam wa afya na madawa katika baadhi ya magereza; upungufu wa huduma maalum kwa wafungwa na mahabusu wanaoishi na VVU na UKIMWI; na huduma duni kwa watoto wadogo walioambatana na mama zao magerezani;

(vii) Kutokuwepo kwa chumba au sehemu maalum ya mahabusu/wafungwa kukutana

na jamaa na ndugu zao magerezani;

(viii) Wafungwa na mahabusu wanawake kutopata taulo za kike;

(ix) Askari Magereza kutolipwa stahili zao kwa wakati; makazi duni ya Askari; Uhaba na Uchakavu wa Sare za Askari kutopandishwa vyeo kwa muda mrefu kwa baadhi ya Askari;

(x) Askari Magereza kutoingizwa kwenye masharti ya kudumu ya ajira mpaka kukamilisha kipindi cha miaka 12 cha utumishi jeshini; na

(xi) Adhabu kandamizi kwa Askari kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Magereza.

2.8.2. Changamoto Zilizobainika Katika Kaguzi za Vituo vya Polisi ni:

(i) Baadhi ya vituo kutokuwa na vyumba kwa ajili ya mahabusu wanawake na watoto;

(ii) Baadhi ya mahabusu kushindwa kupata dhamana kutokana na kuwepo kwa masharti magumu ya dhamana;

(iii) Kutokuwepo kwa rejesta ya mali za watuhumiwa na hivyo wakati mwingine kusababisha upotevu wa mali za mahabusu;

(iv) Ufinyu wa bajeti kwa chakula cha mahabusu ambapo wakati mwingine Maafisa wa Polisi hulazimika kutumia fedha zao kuwalisha mahabusu;

(v) Kukosekana kwa usafiri wa uhakika na upungufu wa vitendea kazi kama vile samani na kompyuta;

(vi) Uhaba wa maji safi na salama katika baadhi ya vituo, hivyo wakati mwingine kushindwa kufanya usafi katika selo na vyoo vya mahabusu.

(vii) Uhaba wa nyumba za kuishi Askari, kucheleweshewa stahili zao kama vile fedha za likizo, na kutopandishwa vyeo kwa wakati;

(viii) Baadhi ya vipengele katika Kanuni za Kudumu za Polisi (PGO) kukiuka haki za binadamu kwa mfano kosa moja linalofanywa na Askari kuwa na adhabu zaidi ya moja;

(ix) Polisi kubambikizia kesi, kuchelewesha upelelezi, kufanya upekuzi bila kufuata taratibu, kuwanyang'anya mali watuhumiwa na mahabusi kutopelekwa mahakamani kwa wakati.

Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria wa THBUB, Bwana Nabor Assey (Kushoto) akikagua kitabu cha usajili wa mahabusi (detention register) katika Mahabusuya Watoto Moshi Juni, 2011. Kulia ni Mkuu wa kituo hicho.

2.8.3. Mapendekezo yaliyotolewa na Tume katika Kaguzi hizo

(i) Mahakama zichukue hatua za makusudi kupunguza mrundikano wa kesi, kusikiliza rufaa kwa wakati unaofaa, kutoa nakala za hukumu na mienendo ya kesi, wafungwa raia wa kigeni waliomaliza vifungo warejeshwe na kutoa adhabu mbadala kwa lengo la kupunguza msongamano magerezani;

(ii) Wizara ya Mambo ya Ndani iboreshe miundombinu kwenye magereza ikiwemo kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu kama sare, maji tiririka, kutoa taulo za kike, matibabu na usafiri,

(iii) Wizara ya Mambo ya Ndani iboreshe maslahi

ya watumishi wa magereza ikiwemo kulipa shtahili zao kama vile malimbikizo; kuboresha makazi, kuongeza idadi ya Askari, sare na kushughulikia upandishwaji wa vyeo

(iv) Wizara ya Mambo ya Ndani ijenge magereza na vituo vya polisi kwenye Wilaya mpya zinazoanzishwa kwa lengo la kutoa huduma muhimu zinazohusiana na idara hizo;

(v) Maafisa na Askari magereza wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora;

(vi) Idara ya Magereza iweke mikakati na taratibu zitakazohakikisha kuwa Askari wenye taaluma za tiba, ugavi na nyingine wanapewa motisha;

2.8.4. Hatua Zilizochukuliwa na Serikali Kuboresha Haki za Wafungwa na Mahabusu Magerezani

Katika kutekeleza majukumu yake, baadhi ya mapendekezo ambayo yalitolewa na Tume na ambayo yametekelezwa ni:-

(i) Kubadili sare za wafungwa “kaptula na shati” na kutoa sare zinazohifadhi na kusitiri utu na heshima ya binadamu;

(ii) Kuboresha lishe kwa wafungwa na mahabusu;

(iii) Kuboresha haki ya kupata habari kwa kuongeza matumizi ya Luninga na redio magerezani;

(iv) Kuboresha miundombinu kwa baadhi ya magereza kwa kujenga vyoo ndani ya mabweni, matumizi ya magodoro katika

magereza; uwepo wa haki ya burudani na taarifa na haki ya elimu;

(v) Mahakama kuongeza matumizi ya adhabu mbadala kupunguza msongamano magerezani;

(vi) Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kutoa msamaha kwa wafungwa mbalimbali; na

(vii) Kuanzishwa kwa Madawati ya Jinsia na Watoto ndani ya Jeshi la Magereza na Jeshi la Polisi kwa kila Wilaya ili kulinda heshima na utu kwa wanawake na watoto.

2.9. Huduma za Kisheria

2.9.1. Ushauri na Msaada wa Kisheria kwa Walalamikaji na Wananchi

Tume imekuwa ikitoa ushauri wa kisheria kwa wananchi katika maeneo mbalimbali kwa kuzingatia majukumu yake. Tume hutoa ushauri wa kisheria kwa wananchi wenye uhitaji ambao hufika katika ofisi za Tume, kwenye ziara za utendaji kazi zinazofanywa na Tume mfano katika ziara za Magereza na Vituo vya Polisi, ziara za utoaji wa elimu na mafunzo na katika mikutano ya hadhara. Aidha katika mashauri ambayo yapo nje ya mamlaka ya Tume, walalamikaji hushauriwa kuyawasilisha katika taasisi na mamlaka zinazoweza kuwasaidia kuyashughulikia.

Sheria ya Tume, Sura ya 391 katika vifungu vya 6(1) (e), (i), 15(3) na 28(4), vimeipa Tume mamlaka ya kufungua mashauri mahakamani ili

kuwezesha upatikanaji wa haki au kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Tume. Baadhi ya kesi zilizosimamiwa na Tume ni pamoja na:-

1. ***Mwanaisha Mohamed Kondo vs Sembo Hussein Jengo & Others***, ***Petition of Appeal No. 76/2013*** kesi hii ilipelekea lalamiko **Na.UB/S/533/13/14** kufunguliwa Tume. Mlalamikaji aliomba Tume imsaidie kukata rufaa Mahakama ya Wilaya Ilala kupinga maamuzi ya Mahakama ya Mwanzo Buguruni iliyomnyima haki. Rufaa iliwasilishwa na kumalizika kwa Mrufani kushindwa. Tume ilikata rufaa kwenda Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam na kushinda kesi.

2. ***Matrimonial Cause No. 34/2011*** **Tasiana L. Shayo vs Epafras Shayo HB/S/151/10/11/MAH/DSM.** Lalamiko hili liliwasilishwa mbele ya Tume na Bi. Tasiana L. Shayo (Mwombaji) akiomba talaka na mgawanyo wa mali walizochuma pamoja na Bw. Epafras Shayo (Mjibu maombi). Kwenye shauri hili Tume ilimwakilisha mwombaji. Shauri hili lilikwisha baada ya wahusika kufikia makubaliano ya kugawana mali nje ya mahakama, ambapo wahusika walisaini hati ya makubaliano (***Settlement Agreement***) na kuiwasilisha mahakamani na shauri husika likaondolewa Mahakamani.

3. ***Republic vs Ally Masoud***, ***Criminal Case*** **No. 17/2014**

   Shauri hili lilihusu Jalada Na **HBUB/S/00022/13/14/DSM** ambapo Mlalamikaji Aziza Masoud aliiomba Tume iingilie mgogoro baina yake na kaka yake Ally Masoud (Msimamizi wa Mirathi ya Baba yao Mzazi) kuhusu urithi. Katika shauri hili Tume ilikuwa na jukumu la kuwasuluhisha. Hata hivyo Mlalamikiwa alikaidi agizo la Tume lililomtaka kuwasilisha hati za nyumba ya Baba yao Moshi Ramadhani kama alivyotakiwa kufanya. Mlalamikiwa alitoa maneno ya vitisho na kejeli kwa Kamishna wa Tume na Wachunguzi wa Tume waliokuwa wanashughulikia lalamiko hili. Hivyo Tume ilitoa taarifa Polisi na Shauri la Jinai tajwa hapo juu lilifunguliwa dhidi ya Ally Masoud kwa kukiuka kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tume kwa kutoa maneno ya kejeli na kuizuia Tume kufanya kazi. Shauri hili lilimalizika kwa mtuhumiwa kukutwa na hatia.

4. ***Barnabas Amed Tesha vs Theresia Barnabas Tesha***, ***Matrimonial Cause No. 22/2014***
   Lalamiko Na. **UB/S/058/13/14** lilifunguliwa Tume kutokana na Shauri husika la Ndoa. Shauri hili lilipelekwa Mahakamani na Bw. Barnabas kuomba talaka na mgawanyo wa mali. Katika kesi hii Tume ilimtetea mwanamke (mjibu maombi) ambaye naye pia alikuwa akitaka aachane na mume wake na wagawane mali. Mlalamikaji ambaye ni mume wa Theresia

Barnabas Tesha aliomba wasuluhishwe. Tume ilifanya usuluhishi kwa wanandoa hao mara tatu na ilishindikana, iliamuliwa mgogoro uendelee mahakamani. Hata hivyo kabla kesi haijatolewa maamuzi na mahakama Mlalamikaji Theresia Barnabas Tesha alifika mbele ya Tume na kueleza wameelewana na mume wake na kurudiana hivyo haoni sababu ya kuendelea na kesi. Hati ya makubaliano (***Settlement Deed)*** iliandaliwa na kuwasilishwa Mahakamani kuhitimisha shauri hili.

2.9.2. Mapitio ya Sheria

Kifungu cha 6 (1) (k) cha Sheria ya Tume Sura ya 391 kinaipa Tume mamlaka ya kupitia sheria, Kanuni na sera mbalimbali ili kubainisha iwapo zinazingatia haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Sheria zilizopitiwa ni pamoja na:-

1. **Sheria ya Takwimu Na. 9 ya 2015 (The National Statistics Act, No. 9 of 2015)**

   THBUB ilipitia Sheria husika na kubaini kuwa ina vipengele vinavyokinzana na Ibara ya 18 ya Katiba inayoruhusu uhuru wa kutoa maoni, kujieleza na kupata habari. Kifungu cha 20(2) cha Sheria tajwa kinazitaka mamlaka zote kupata kibali cha kutoa takwimu kutoka kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali bila kutoa muda maalum na ukomo wa muda husika.

   THBUB ilibaini kuwa, kukosekana kwa ukomo wa muda wa kutolewa kibali cha kupata takwimu ni kinyume na Katiba na kunasababisha uvunjwaji wa haki ya kutoa

maoni, kujieleza na kupata habari. Hivyo ilipendekezwa kuwa kifungu tajwa kifanyiwe marekebisho kukidhi takwa la kikatiba.

Changamoto ilionekana pia kwenye kifungu cha 37 cha Sheria tajwa kwa kuwa kifungu husika kinatoa adhabu kubwa kwa makosa yaliyoainishwa na sheria hiyo. Aidha, inasabisha kuwepo ugumu kwa vyombo vya habari na wadau wote ambao kwa namna moja au nyingine wangetumia takwimu ambazo zingedaiwa kukosa kibali cha Mtakwimu Mkuu wa Serikali. THBUB ilipendekeza kuboreshwa kwa vifungu husika na kurekebisha adhabu kulingana na kosa lililofanyika.

2. **Sheria ya Hati na Nyaraka za Kusafiria (The Tanzania Passports and Travel Documents Act, No 20 of 2002)**

   THBUB kwa kushirikiana na wadau mbali mbali ilipitia Sheria tajwa na kubainisha changamoto zinazokabili kundi la watu ambao wanahitaji kupewa *Diplomatic Passports* kama ilivyobainishwa kwenye kifungu cha 10(3) na Jedwali la Tatu la Sheria husika. Ilipendekezwa kuongeza wigo wa watu wanaohusika katika kundi hilo kwa kuwa lilionekana ni dogo.

3. **Sheria ya Makosa ya Mtandaoni (The Cyber Crimes Act No. 14 of 2015)**

   Sheria tajwa ilitungwa mahsusi kwa ajili ya kuruhusu ulinzi wa watu wanapotumia mitandao *cyber space* lakini badala yake imekuwa na

vizuizi mbalimbali kukinzana na haki ya kujieleza na kutoa maoni.

Kwa mfano kwenye kifungu cha 31(1)(b) (1) cha Sheria tajwa kinatoa nguvu kubwa kwa Jeshi la Polisi kuwakamata watuhumiwa wa uharamia kwenye *cyber space.*

Ilibainika kwamba kuna uwezekano wa kutumika vibaya mamlaka hayo na kusababisha watu kutokufurahia haki ya uhuru wa kutoa maoni na kujieleza. Aidha, Sheria husika haina kifungu kinachozungumzia ulinzi kwa watoa taarifa kwa namna yeyote ile. THBUB ilipendekeza kuwa mabadiliko yafanyike ili kuweza kuboresha upatikanaji wa haki tajwa na ulinzi wa jamii.

4. **Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura ya 391**

   Sheria hii ilipitiwa na kupendekezwa kufanyiwa maboresho kwenye maeneo yanayohusu nafasi ya Makamu Mwenyekiti kama ilivyobainishwa kwenye kifungu cha 7(1)(b) ambapo ilipendekezwa kuwa sifa za Makamu Mwenyekiti zibainishwe na isiwe sifa za kijiografia bali za kitaaluma na uzoefu. Mfano awe mwenye taaluma ya sheria na hadhi ya kuwa Jaji wa Mahakama Kuu au ya Rufani.

   Kifungu cha 33 (1) cha Sheria tajwa pia kilipendekezwa kufanyiwa maboresho ili kuruhusu Taarifa za Mwaka za Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kuwasilishwa Bungeni.

5. **Sheria ya Watu wenye Ulemavu (The Persons with Disabilities Act, 2010)**
   Sheria ilipitiwa na ilibainika inakidhi vigezo vilivyobainishwa kwenye mikataba ya Kimataifa na kikanda ambayo Tanzania ni mwanachama. Changamoto iliyobainika ni katika utekelezaji wa sheria husika. Hata hivyo kwa tathmini ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, inaitaka Serikali kutenga rasilimali za kutosha kutekeleza sheria hii.

6. **Sheria ya Mtoto Sura ya 13**
   Tume ilipitia sheria husika na kubaini kuwa pamoja na sheria kukidhi matakwa ya mikataba ya kikanda na kimataifa kuhusu haki ya mtoto, bado kuna uchache wa mifumo ya kulinda haki zao hususan kwenye eneo la watoto waliokinzana na sheria. Ilishauriwa na kupendekezwa kuwa kwenye mashauri yote yanayowagusa watoto wanaokinzana na sheria Idara ya Ustawi wa Jamii ishiriki kikamilifu. Pia mahabusu za watoto zijengwe zaidi na zilizopo ziimarishwe na kanuni ya haki na maslahi ya mtoto (***best interest of the child principle)*** ipewe kipaumbele.

7. **Sheria ya Bodi ya Mikopo**
   Sheria hii ilipitiwa na kupendekezwa kufanyiwa maboresho ambayo kimsingi yalikuwa ya utekelezaji wa sheria zaidi. Ilipendekezwa kwa kuwa Sheria imelenga kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu;

mikopo hiyo itolewe bila ubaguzi kwani wanafunzi wote ni watanzania. Aidha, kuweka vigezo ambavyo vitawawezesha watanzania wote wenye ufaulu unaostahiki kupata fursa ya mikopo ili kuendelea na masomo.

2.10. Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume

Kifungu cha 28(2) cha Sheria ya Tume Sura ya 391 kinatoa wajibu kwa taasisi au mlalamikiwa kutekeleza mapendekezo ya Tume ndani ya siku Tisini (90). Katika kutekeleza takwa hili la Kisheria THBUB ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo iliyoyatoa kwa mamlaka mbalimbali kwa ajili ya kuboresha hali ya haki za binadamu na uzingatiwaji wa misingi ya utawala bora kufuatia chunguzi mbalimbali zilizofanywa. Baadhi ya mapendekezo yaliyotekelezwa na mamlaka husika ni pamoja na kuboreshwa kwa miundombinu ya magereza kwa kuondoa mitondoo, kuboreshwa kwa sare za wafungwa, malazi na burudani. Nyingine ni Kutungwa kwa Sheria ya Mtoto Sura ya 13, Kutungwa kwa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Sura ya 183, viongozi wa umma waliotumia vibaya madaraka yao vibaya kuchukuliwa hatua za kinidhamu na malipo ya mafao kwa baadhi ya wastaafu. Katika ufuatiliaji huo, Tume ilibaini kuwa kuna baadhi ya mapendekezo hayajatekelezwa na mamlaka husika ikiwemo kulipwa fidia kwa wananchi wa Nyamuma, Vifo vya mahabusu 17 katika Kituo cha Polisi Mbarali na kutoboreshwa kwa maslahi ya Askari wa Jeshi la Polisi na Magereza.

2.11. Ushirikiano na Taasisi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa

Sheria ya Tume Sura ya 391 katika kifungu cha 6(1) (m) kinaitaka Tume kushirikiana na taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa katika kulinda na kuhamasisha haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Sheria ya Tume inaitaka kushirikiana na taasisi za ndani na kuishauri serikali na vyombo vingine vya umma na taasisi za sekta binafsi juu ya mambo maalum yanayohusiana na haki za binadamu na utawala bora. Pia, Kanuni za Paris zinaitaka Tume kushirikiana na taasisi nyingine katika masuala ya haki za binadamu na utawala bora[16].

2.11.1. Uhusiano na Serikali

Katika kutekeleza majukumu yake Tume imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na Wizara, Idara na Wakala za Serikali (MDAs) pamoja na mamlaka za Serikali za Mitaa. Mahusiano ni katika nyanja za mafunzo, kupata taarifa zinazohusiana na malalamiko yaliyofikishwa Tume, utekelezaji wa mapendekezo, uwasilishaji wa bajeti na taarifa za Tume Bungeni. Baadhi ya MDAs tayari zimeteua maafisa *(Focal persons)* wanaoshughulikia masuala ya haki za binadamu na utawala bora na hivyo kurahisisha mawasiliano katika utendaji kazi.

[16] *Principle 3(e) insist about to cooperate with the United Nations and any other orgnization in the United Nations system, the regional institutions and the national institutions of other countries that are competent in the areas of the protection and promotion of human rights*

2.11.2. Uhusiano na Bunge

Katika kipindi cha miaka 20, Tume imefanya kazi kwa karibu na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. THBUB imenufaika na mijadala na maelekezo kutoka kwa wabunge wakati wa mijadala ya bajeti, semina, na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kisekta.

Pia, THBUB imekuwa ikifanya kazi na Kamati za Bunge kushughulikia masuala mahsusi ya haki za binadamu na utawala bora. Miongoni mwa masuala hayo ni mashauriano kuhusiana na kupitishwa kwa Sheria ya Mtoto 2009 na kubadilishana taarifa kuhusu Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu 2013-2017.

2.11.3. Uhusiano na Mahakama ya Tanzania

Katika kutekeleza jukumu lake la kutoa elimu ya haki za binadamu na utawala bora, Tume imeweza kuendesha programu za uhamasishaji zinazolenga kuongeza uelewa na maarifa kwa kutoa mafunzo kwa Majaji wa Mahakama Kuu, Wasajili wa Mahakama na Mahakimu kuhusu kuzingatia haki za binadamu katika utoaji haki. Vile vile Tume imeshirikiana na Mahakama katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wafungwa na mahabusu wakati wa kaguzi za Magereza na Vituo vya Polisi na ushughulikiaji wa malalamiko yanayowasilishwa Tume yanayoihusu Mahakama ya Tanzania.

Changamoto inayoikabili Tume katika mahusiano yake na mamlaka za Serikali ni

uelewa wa baadhi ya viongozi kuhusu dhana ya ombudsman, mamlaka ya Tume kama taasisi ya kitaifa ya haki za binadamu na mtazamo hasi kuhusu Tume kuingilia kazi za mamlaka nyingine ambao ni wa kinadharia.

2.11.4. Uhusiano na AZAKi

Katika kutekeleza moja ya Kanuni za Paris[17] THBUB imeendelea kushirikiana na Asasi za Kiraia (AZAKi). Tume imekuwa ikifanya kazi pamoja na AZAKi hususan katika kuelimisha umma kuhusu masuala ya haki za binadamu, usambazaji wa taarifa kuhusu haki za binadamu na utawala bora, kuwasaidia wananchi waliovunjiwa haki zao kwa kuwaelekeza kwenda kwenye mojawapo ya ofisi za Tume ili kuwasilisha malalamiko yao, na kufanya ufuatiliaji wa uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Katika kuimarisha uhusiano huo, Tume imetiliana saini Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) na jumla ya AZAKI **31**, nne **(4)** kutoka Zanzibar na **27** kutoka Tanzania Bara. Aidha, Tume imekuwa na mahusiano mazuri ya kiutendaji na AZAKI nyinginezo zinazojihusisha na masuala ya Haki za Binadamu nchini. Kwa

[17] Kanuni ya 3(g) ambayo inasema:- Kwa kuzingatia wajibu muhimu unaofanywa na mashirika yasiyo ya Kiserikali katika kuongeza wigo wa utekelezaji wa kazi za taasisi za kitaifa za haki za binadamu, anzisheni mahusiano na mashirika yasiyo ya Kiserikali yaliyojitoa kukuza na kulinda haki za binadamu, maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kupambana na ubaguzi wa rangi, kulinda hususan makundi yaliyo katika hatari ya kudhuriwa (hasa watoto, wafanyakazi wahamaji, wakimbizi, watu wenye ulemavu wa kimwili na kiakili) au walio katika maeneo maalumu.

mfano, imefanya kazi na Asasi Zisizo za Kiserikali kama vile *Policy Forum* katika kuandaa na kusambaza machapisho mbalimbali ya elimu kwa umma.

Pia, Tume imefanya kazi na taasisi ya Legal Services Facility katika mradi wa "Kuboresha Upatikanaji wa Haki kwa Wote, hususan Wanawake yaani "*Enhancing Access to Justice and Human Rights for All Particularly to Women"*. Mradi huu ulianzishwa ili kuimarisha mahusiano baina ya Tume, Maafisa wa Halmashauri na Wasaidizi wa Sheria kwa kuzingatia utekelezaji wa Sheria ya Kutoa Msaada wa Kisheria kupitia Sheria ya mwaka 2017. Vilevile, Tume imekuwa ikiziratibu kwa mafanikio zaidi ya AZAKI 50 nchini katika kuandaa taarifa zao za pamoja za Tathmini ya Kimataifa ya Haki za Binadamu Katika Kipindi Maalum (Universal Periodic Review) zilizowasilishwa Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa.

Licha ya uwepo wa mafanikio ya wazi katika ukuzaji na ulinzi wa haki za binadamu nchini, ushirikiano uliopo baina ya THBUB na AZAKi umekumbana na changamoto kadhaa, zinazojumuisha: uhaba wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji na ufuatiliaji wa programu za pamoja, ukosefu wa uwajibikaji na mwitikio kwa baadhi ya AZAKi, ukosefu wa ufanisi na matokeo bora katika utekelezaji wa programu

na ukosefu wa ujuzi wa kutosha katika kushughulikia masuala ya haki za binadamu.

2.11.5. Taasisi za Kimataifa

THBUB ni mwanachama wa Mtandao wa Taasisi za Haki za Binadamu za Kitaifa Ulimwenguni (Global *Alliance for National Human Rights Institutions* - GANHRI), Mtandao wa Taasisi za Haki za Binadamu za Kitaifa Afrika (*Network of African National Human Rights Institutions* - NANHRI), Taasisi ya Kimataifa ya Ombudsman *(International Ombudsman Institute* - IOI), Umoja wa *Ombudsman* za Afrika (*African Ombudsman and Mediators Associations* - AOMA). Kupitia uanachama huo, Tume imekuwa ikihudhuria mikutano, kushiriki kwenye mafunzo na kubadilishana uzoefu kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora. Ushirikiano huo umechangia katika kuimarisha utendaji wa Tume na kuendana na viwango na kanuni za uendeshaji wa Taasisi za Haki za Binadamu za Kitaifa na Ombudsman.

Tume imeendelea kuwa na uhusiano na Taasisi mbalimbali za Kikanda na Kimataifa ikiwemo Office of the High Commissioner for Human Rights (OHCHR), United Nations Development Programme (UNDP), United Nations Children's Education Fund (UNICEF), International Labour Organization (ILO), Danish International Development Agency (DANIDA), Danish Insitute for Human Rights (DIHR), International Working

Group on Indigenous Affairs (IWGIA) International Fund for Agricultural Development (IFAD), International Peace Information Service (IPIS), DIGNITY, Public International Law and Policy Group (PILPG), SOMO, Save the Children na HelpAge International.

Mahusiano hayo yalijikita katika kuijengea uwezo Tume katika nyanja mbalimbali ikiwemo fedha, vitendea kazi, miundombinu, mafunzo, utaalam na utekelezaji wa miradi ya haki za binadamu.

Baadhi ya miradi iliyotekelezwa kupitia mahusiano hayo ni ufuatiliaji wa haki za watoto walio katika vizuizi, utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu, kuhamasisha utekelezaji wa haki za Watu Wanaoishi Maisha ya Asili, Haki za Wazee, Haki za Binadamu na Biashara, na kufanya Tathmini ya Tamko la Marrakech.

Picha ya pamoja kati ya Viongozi, Watumishi wa THBUB na Mkurugenzi Mtendaji wa NAHRI alipotembelea ofisi za Tume Kilimani Dodoma. Katikati ni Bw. Gilbert Sebihogo Mkurugenzi Mtendaji wa NAHRI, kushoto kwake ni Mh. Mathew Mwaimu Mwenyekiti wa THBUB; Amina Talib Ali Kamishna; Kulia ni Mohamed Khamis Makamu Mwenyekiti na Dkt. Fatma Khalfan Kamishna. (Chanzo THBUB 2020)

2.12. Tathmini ya Tume Kulingana na Paris Principles *(Accreditation)*

GANHRI kwa kushirikiana na OHCHR hufanya tathmini ya Taasisi za Haki za Binadamu za Kitaifa kila baada ya miaka mitano kwa lengo la kuona namna Taasisi inavyokidhi vigezo vilivyoainishwa kwenye Kanuni za Paris, Mikataba ya Kikanda, Kimataifa na Sheria mbali mbali za nchi.

Tangu kuanzishwa kwa Tume 2001 na kuanza rasmi utekelezaji wa majukumu yake mwaka 2002 Tume imefanyiwa tathmini mwaka 2003, 2006, 2011 na 2017. Kwa mara zote imepata Hadhi ya Daraja A (A status NHRI).

Hadhi ya Daraja A ni kielelezo kinachoonesha kuwa nchi inaheshimu, inalinda, inahifadhi na kutetea haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Tume inatarajia kufanyiwa tathmini inayofuata mwaka 2023.

2.13. Tathmini ya Kimataifa ya Haki za Binadamu Katika Kipindi Maalum (UPR)

Tathmini ya Kimataifa ya haki za binadamu ni mchakato wa kupima utekelezaji wa haki za binadamu inayofanywa kwa nchi kila baada ya miaka minne (4). Tathmini hiyo hufanywa na Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu.

Tanzania imeshafanyiwa tathmini mara tatu 2011, 2016 na 2021. Tathmini hizi zilifanyika baada ya serikali ya Tanzania kuwasilisha taarifa inayoeleza utekelezaji wa haki za binadamu nchini. Katika vipindi hivyo THBUB iliwasilisha taarifa iliyotoa tathmini ya hali ya haki za binadamu. Taarifa hii inapowasilishwa huambatana na mapendekezo Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa na kutoa nafasi kwa Serikali kupitia mifumo yake kubainisha katika sera na mikakati yake ni masuala yapi inayapokea na kuyaingiza katika taratibu za utekelezaji.

Jedwali Na. 18: Mapendekezo ya Universal Periodic Review (UPR) 2011-2021

MWAKA	JUMLA YA MAPENDEKEZO	YALIYOKUBALIWA NA SERIKALI	YALIYOKATALIWA	YASIYOKUBALIKA MOJA KWA MOJA
2011	153	107	33	13
2016	227	129	72	25
2021	252	167	65	20

Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya UPR 2011-2021

Mapendekezo Yaliyokataliwa na Serikali

Baadhi ya mapendekezo ambayo yamekuwa yakikataliwa na Serikali ni kama yafuatayo:-

(i) Kuondolewa adhabu ya kifo;

(ii) Kuondolewa adhabu ya kuchapa viboko shuleni;

(iii) Kutambuliwa kwa watu wanaoishi maisha asili *(recognition of Indigenous people's*);

(iv) Kuongeza umri wa kuolewa kwa wasichana kutoka miaka 15 mpaka miaka 18;

(v) Kuondolewa ndoa za mitala na mahari;

(vi) Suala la ubakaji katika ndoa kufanywa kuwa kosa la jinai;

(vii) Haki za watu wenye mahusiano ya kimapenzi ya jinsia moja (LGBTI);

(viii) Kuridhia Mkataba wa Kimataifa kuhusu Utesaji na Adhabu za kutweza.

Mchakato huu umekuwa chachu katika kutekeleza haki za binadamu nchini kwa kuwaleta pamoja wadau wa haki za binadamu na kujadili masuala muhimu na kupanga mikakati ya kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa; kuibua mijadala kuhusu masuala mbalimbali ya haki za binadamu miongoni mwa wadau kutoka Serikalini; Asasi za Kiraia na wananchi kwa ujumla; kuandaliwa kwa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu 2013-2017; na Serikali kupata fursa ya kutoa ahadi katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa haki za binadamu.

SEHEMU YA PILI

HISTORIA NA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME ZANZIBAR

SURA YA KWANZA

1.0. HISTORIA YA TUME ZANZIBAR

1.1. Utangulizi

Kwa mujibu wa Ibara ya 130 (6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Tume Sura ya 391, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), ni chombo cha Muungano ikiwa na maana kwamba inafanya kazi katika pande zote za Muungano yaani Tanzania Bara na Zanzibar.

Tume ilianza kazi zake rasmi Zanzibar tarehe 30 Aprili 2007 baada ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kutunga Sheria ya kuongeza mamlaka ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa Zanzibar (*Extension Act*) Na. 12/2003. Hatua hii ilifuatiwa na marekebisho ya sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Sura ya 391 yaliyofanywa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (*Miscellaneous Amendments*) Na. 8/2006. Kutokana na marekebisho hayo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba na Utawala Bora Zanzibar kupitia Tangazo katika Gazeti la Serikali Namba 31 la mwaka 2007, alitangaza uamuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuridhia Tume kufanya shughuli zake Zanzibar. Kabla ya marekebisho hayo Tume ilikuwa ikifanya kazi Zanzibar kwa kushughulikia malalamiko yaliyohusu masuala ya Muungano tu.

1.2. Uendeshaji wa ofisi ya Tume Zanzibar

Ofisi ya Tume Zanzibar inatekeleza majukumu yake chini ya usimamizi wa Kamishna Mkaazi, akisaidiwa na Naibu Katibu Mtendaji na watumishi wengine wakiwemo Maafisa Uchunguzi.

Ofisi ya Tume Zanzibar ipo kwenye jengo la Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Mbweni. Katika kusogeza huduma zake karibu na wananchi, Tume ilianzisha Tawi la Pemba tarehe 01 Agosti 2015.

Jedwali Na. 1: Makamishna Waliowahi Kuhudumu Ofisi ya Zanzibar

SN	JINA	MWAKA
1.	Mhe. Safia Masoud Khamis	2007-2008
2.	Mhe. Zahor Khamis Juma	2009-2013
3.	Mhe. Mohamed Khamis Hamad	2014-2017
4.	Mhe. Khatib Mwinyichande Khatib	2019- hadi sasa

Jedwali Na.2: Naibu Katibu Mtendaji

SN	JINA	MWAKA
	Juma Msafiri Karibona	Januari 2022 Hadi Sasa

Jedwali Na.3: Maafisa Wafawidhi (Unguja na Pemba)

SN	JINA	OFISI	MWAKA
1	Joel Mkumbwa	Zanzibar	2001-2007
2.	Mwanyemi Bilal Eliud	Zanzibar	2007-2014
3.	Suleiman Salim Ahmad	Zanzibar	2014-2015
4.	Hussein Khamis Mbarouk	Zanzibar	2015-2021
5.	Saada Ahmed Masoud	Zanzibar	2021 hadi sasa
6.	Suleiman Salim Ahmad	Pemba	2017 hadi sasa

SURA YA PILI

2.0. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MIAKA 20 (2001/2002 -2021/2022)

2.1. Utangulizi

Tume inafanya kazi Zanzibar kwa mujibu wa ibara 130 (6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na kifungu cha 3 cha Sheria ya Tume Sura ya 391 kama ilivyorekebishwa na Sheria Namba 8 ya mwaka 2006. Marekebisho hayo yalitokana na Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora *(Extension) Act* Na. 12/2003 iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

2.2. Utekelezaji wa Kazi za Tume

Katika kipindi cha miaka 20, Ofisi ya Tume Zanzibar ilifanya kazi mbalimbali za kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Baadhi ya kazi hizo ni:- kupokea na kuchunguza malalamiko; kutoa elimu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora; kufanya utafiti na ufuatiliaji wa haki za binadamu; uangalizi wa Uchaguzi Mkuu; na kukagua Vyuo vya Mafunzo na Vituo vya Polisi.

2.3. Kupokea na Kuchunguza Malalamiko

Ibara ya 130 (1) (c), (f), na (g) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 6 (1)(b) na (c) cha Sheria za Tume Sura ya 391 kwa pamoja vinaipa Tume mamlaka ya kupokea na kufanya uchunguzi kuhusu masuala yanayohusu haki za binadamu na

ukiukwaji wa misingi ya utawala bora. Tume inaweza kuanzisha uchunguzi yenyewe au kupokea lalamiko kutoka kwa mtu mmoja, kikundi cha watu, jumuiya, taasisi na kampuni kwa niaba ya wananchi.
Malalamiko yanaweza kuwasilishwa[18] kwa kufika kwenye mojawapo ya ofisi za Tume Unguja na Pemba, kwa mtu kufika kwenye mojawapo ya ofisi za Tume; au kwa kutuma kwa barua, kwa njia ya posta au barua-pepe, kupiga simu, kutuma ujumbe wa simu ya kiganjani "USSD Code", au kwa simu janja (Haki App) na kwa kutumia tovuti ya Tume.[19]

Katika kipindi cha miaka 20 Ofisi ya Tume Zanzibar ilipokea na kushughulikia jumla ya malalamiko **724** kati ya hayo, malalamiko **90** yalirithiwa kutoka iliyokuwa Tume ya Kudumu ya Uchunguzi (TKU). Kati ya malalamiko hayo, jumla ya malalamiko **553** uchunguzi wake ulikamilika na kuhitimishwa. Idadi ya malalamiko yanayoendelea kufanyiwa uchunguzi hadi Juni 30, 2022 ni **171**.

[18] Kifungu cha 22(1) cha Sheria ya Tume Sura ya 391
[19] Email, info@chragg.go.tz, SLP 1049 DODOMA

Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa malalamiko yaliyopokelewa, yaliyohitimishwa na yanayoendelea kuanzia Julai 2001 hadi Juni 2022

Mwaka	Yaliyopokelewa	Yaliyohitimishwa	Yanayoendelea
Yaliyorithiwa kutoka TKU	90	90	-
2001/2002	15	15	-
2002/2003	20	20	
2003/2004	11	11	-
2005/2006	9	9	-
2006/2007	67	65	2
2007/2008	104	99	5
2008/2009	43	40	3
2009/2010	26	21	5
2010/2011	38	31	7
2011/2012	42	36	6
2012/2013	15	14	1
2013/2014	18	9	9
2014/2015	30	21	9
2015/2016	20	12	8
2016/2017	30	16	14
2017/2018	34	18	16
2018/2019	23	5	18
2019/2020	15	1	14
2020/2021	46	15	31
2021/2022	28	5	23
Jumla	**724**	**553**	**171**

2.4. Ufuatiliaji wa Baadhi ya Malalamiko Katika Kipindi cha Mwaka 2001/2002 -2021/2022

1. Lalamiko Na. UB/S/15/2020/2021

Tume ilifuatilia lalamiko la mtoto mmoja mwenye ulemavu wa akili na viungo ambaye alikuwa akifanyiwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji na mama yake. Mama wa mtoto huyo ambaye alitengana na baba wa mtoto alikuwa akimfanyia unyanyasaji mtoto wake kwa kumfungia ndani ya nyumba na wakati mwingine mtoto huyo hujisaidia na kuchezea uchafu ikiwa ni pamoja na kusambaza kwa majirani anapopata nafasi ya kutoka nje. Vilevile kushinda katika hali ya uchafu na bila ya kula chakuka kwa muda mrefu.

Katika uchunguzi wa lalamiko hilo, Tume ilishirikiana na Idara ya Ustawi wa Jamii Wilaya ya Magharibi ‘B,’ Idara ya Watu Wenye Ulemavu na ndugu wa mtoto. Kufuatia uchunguzi huo na kwa kuzingatia maslahi ya mtoto, maamuzi yalifikiwa ambapo baba mzazi aliomba mtoto huyo akaishi na bibi yake ambaye aliridhia kuishi naye na baba huyo kupeleka pesa za matumizi. Kadhalika zilifanyika jitihada za kumuunganisha mtoto huyo katika Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar ili aweze kunufaika na fursa zinazojitokeza na pia kumuandikisha katika skuli za watoto wenye ulemavu wa akili.

2. Lalamiko Na. HB/S/23/2017/2018/ZANZIBAR

Lalamiko hili lilihusu madai ya fidia na matibabu ya mtoto mmoja iliyotokana na uzembe kwenye utekelezaji wa tohara uliosababisha kukatwa uume katika kituo kimoja cha Afya Zanzibar. Tume ilipendekeza Wizara ya Afya

impatie matibabu zaidi mtoto huyo na waliohusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Katika ufuatiliaji wa mapendekezo hayo Tume ilibaini kuwa mtoto huyo alianzishiwa matibabu hapa nchini katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja ambayo yangemsaidia kurefusha uume wake. Mkurugenzi wa Hospitali hiyo aliijulisha Tume kuwa baada ya matibabu ya miezi mitatu mtoto huyo angeangaliwa hali yake kwa hatua zaidi.

2.5. Uchunguzi wa Hadharani Kuhusu Migogoro ya Ardhi

Tume ilifanya uchunguzi wa hadharani kuhusu migogoro ya ardhi kutokana na malalamiko ya wananchi kuhamishwa kutoka katika maeneo yao. Uchunguzi huu ulifanyika katika Mikoa yote mitano (5) ya Zanzibar. Malengo ya Uchunguzi huo yalikuwa ni:-

(i) Kubaini sababu na ukubwa wa tatizo la wananchi kuhamishwa katika ardhi yao;

(ii) Kubaini iwapo utaratibu ulioainishwa na sheria kuhusu kuhamisha wananchi katika ardhi yao ulifuatwa;

(iii) Kubaini madhara waliyopata wananchi waliondolewa katika maeneo yao; na

(iv) Kupata maoni na mapendekezo ya wananchi kuhusu namna ya kuondoa tatizo la migogoro ya ardhi.

Mambo yaliyobainika katika uchunguzi huo ni pamoja na wananchi kutoshirikishwa katika zoezi la kufanya uthamini wa ardhi yao; kutolipwa fidia baada ya kuharibiwa mali zao; na kucheleweshwa kwa malipo ya fidia.

Mapendekezo mbalimbali yalitolewa ikiwa ni pamoja na Serikali kuendelea kuwashirikisha wananchi pale inapofanya uthamini na kulipa fidia kwa wakati.

2.6. Matumizi ya Barabara na Haki za Binadamu

Mwezi Oktoba 2011 Tume kwa kuzingatia umuhimu wa matumizi salama ya barabara katika utekelezaji wa haki za binadamu, ilifanya uchunguzi kuhusu matumizi ya barabara na utekelezaji wa haki za binadamu katika Mikoa ya Mjini Magharibi na Kusini Unguja. Uchunguzi huo ulifanyika kwa madhumuni yafuatayo:-

a) Kubaini jinsi haki za binadamu zinavyozingatiwa katika ujenzi wa barabara na matumizi yake;

b) Kutoa ushauri kwa mamlaka husika namna ya kuimarisha utekelezaji wa haki za binadamu katika matumzi ya barabara; na

c) Kubaini vyanzo mbalimbali vinavyochangia ajali ambazo zimesababisha uvunjwaji wa haki ya kuishi kwa kupoteza maisha ya watu, mali na ulemavu wa maisha.

Katika uchunguzi huo Tume ilibaini kuwa:- baadhi ya barabara hazikuwa na njia za watembea kwa miguu; baadhi ya barabara kutokuwa na vituo vya magari ya abiria; baadhi ya alama za barabarani kutoonekana aidha kwa kufutika au kuondolewa; ujenzi wa majengo kutozingatia kuwepo kwa sehemu za maegesho ya magari; na barabara nyingi kutokuwa na sehemu ya hifadhi ya barabara.

Taarifa yenye mapendekezo iliandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika kwa ajili ya utekelezaji.

2.7. Uchunguzi wa Kifo cha Mahabusu Katika Kituo cha Polisi

Tume ilichunguza tukio lililotokea mwaka 2017 la vijana wawili kupigwa na kujeruhiwa katika Shehia fulani katika Wilaya mojawapo huko Zanzibar. Tume ilichukua hatua hiyo baada ya kupata taarifa kutoka vyombo mbalimbali vya habari, ikiwemo kipindi cha Mawio cha Redio Zanzibar. Ilielezwa kuwa vijana hao wawili wakiwa katika makazi yao walivamiwa kwa silaha za jadi yakiwemo mapanga.

Uchunguzi wa Tume ulibaini kuwa vijana hao walipigwa na kuumizwa na watu waliotambuliwa kuwa ni Polisi Jamii waliokuwa katika doria. Wakiwa na majeraha hayo walifikishwa katika kituo cha Polisi ambako waliwekwa mahabusu bila ya kupatiwa matibabu yoyote na hatimaye mmoja wao alifariki siku iliyofuata akiwa katika mahabusu hiyo.

Kupigwa kwa vijana hao kulitokana na kilichodaiwa na Polisi Jamii kuwa tabia za vijana hao kuwakaribisha katika eneo lao watu wanaosadikiwa kuwa ni hatari. Hata hivyo tuhuma hizo hazikuwahi kutolewa kwa Sheha wala kituo chochote cha Polisi. Aidha, baadhi ya wananchi walidai kuwa marehemu na rafiki yake walikuwa na kawaida ya kufanya mazoezi ya mchezo wa judo na kareti kwa lengo la kujihami, katika eneo tofauti na lile lililotengwa kwa ajili ya shughuli hiyo.

Miguu ya mmoja wa vijana waliopigwa na kujeruhiwa na watu waliotambulika kama Polisi Jamii tarehe 3 Januari, 2017 katika Shehia ya Chuini, Wilaya ya Magharibi A. (Chanzo THBUB 2017)

Katika uchunguzi huu ilibainika kuwa:-

(i) Watekelezaji wa zoezi la ukamataji walijichukulia sheria mikononi badala ya kufuata utaratibu wa sheria.

(ii) Kuwaweka mahabusu watu wenye majeraha bila kuwafikisha katika kituo cha afya kupata matibabu au hata huduma ya kwanza ni kinyume cha maadili na kanuni za utendaji kazi wa Jeshi la Polisi.

(iii) Kutesa, kupiga watu na kusababisha kifo ni ukiukwaji wa haki za binadamu wa kiwango cha juu na kosa la jinai.

(iv) Kitendo cha Jeshi la Polisi kutowachukulia hatua za kisheria Polisi Jamii waliohusika na utekelezaji

wa uovu huo ni kukiuka utawala wa sheria na haki za binadamu.

Mapendekezo yalitolewa kwa Jeshi la Polisi

(i) Kufanya upelelezi na kuwafikisha mahakamani wahusika wa mauaji na vitendo vya kujichukulia sheria mikononi;

(ii) Kuwachukulia hatua za kinidhamu Askari waliokuwa zamu katika kituo cha Polisi Bububu usiku wa tukio kwa kutokutekeleza wajibu wao; na

(iii) Kutoa miongozo ya kiutendaji kwa Polisi Jamii na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miongozo hiyo ili kuepusha uwezekano wa kutumika vibaya kwa Polisi Jamii.

2.8. Uchunguzi wa Malalamiko Juu ya Matokeo ya Mitihani ya Kidato cha Nne Mwaka 2011

Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Ofisi ya Tume Zanzibar ilianzisha uchunguzi juu ya malalamiko ya matokeo ya mtihani wa kidato cha nne wa mwaka 2011 ili kuona kadhia ya uvunjwaji wa haki za binadamu kwa wanafunzi wahitimu wa kidato cha nne mwaka 2011 kulikosababishwa na kufutiwa matokeo ya mtihani wao na Baraza la Mitihani la Taifa. Baraza hilo lilitoa adhabu ya kuwazuia kufanya mitihani ya baraza kwa muda wa miaka mitatu kwa baadhi ya wanafunzi wa skuli za Tanzania Bara na Zanzibar na lilitaja sababu za kuchukuwa uamuzi huo kuwa ni:-

(i) Baadhi ya wanafunzi walikamatwa na karatasi za majibu (booklets) zilizokwishajibiwa maswali;

(ii) Baadhi ya wanafunzi waliandika matusi na mambo ya ajabu ajabu katika karatasi za mitihani;

(iii) Baadhi ya wanafunzi waliandika mashairi ya nyimbo za miziki ya bongo fleva; na

(iv) Wengine walikuwa na majibu ya mfanano usiokuwa wa kawaida

Kufutwa kwa matokeo hayo kuliibua malalamiko ya wananchi na wanafunzi dhidi ya Baraza la Mitihani ya Taifa. Kwa upande wa Zanzibar yalikithiri hadi kufikia hatua ambayo baadhi ya Asasi za Kiraia na baadhi ya wazazi wa wanafunzi waliunda Kamati kufuatilia suala hilo.

Katika ufuatiliaji huo Tume ilibaini mambo mbalimbali yakiwemo:- wananfunzi kukutwa na vijitabu vya majibu vilivyokwishajibiwa na majibu ya mfanano usiokuwa wa kawaida; kasoro zilizojitokeza katika usimamizi wa mitihani ambapo baadhi ya wanafunzi kuingia katika vyumba vya mitihani bila kukaguliwa; kuingia na majibu pamoja na simu za kiganjani katika vyumba vya mitihani: na kwamba Baraza la Mitihani halikuwa chanzo cha udanganyifu kwa kuvujisha mitihani kwa sababu hawakupata taarifa ya kuvuja kwa mitihani hiyo na kwamba udanganyifu ulikithiri katika baadhi ya skuli za Tanzania Bara na Zanzibar.

Baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na Tume katika ufuatiliaji huo ni:-

(i) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iboreshe mazingira ya kusomea na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kuzipatia skuli walimu wenye sifa na vifaa vya kusomea ili kuwajengea uwezo

wanafunzi na kuweza kufanya mitihani yao kwa kujiamini.

(ii) Baraza la Mitihani la Taifa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar lichukue hatua madhubuti kuhakikisha wanateuliwa wasimamizi wenye sifa na uadilifu katika kusimamia mitihani ya Taifa.

(iii) Wazazi na Walimu wahimize wanafunzi kuongeza jitihada katika masomo yao ili kujiepusha na tamaa ya kufaulu kwa njia za udanganyifu

2.9. Uchunguzi wa Zoezi la Kuondoa Wanyama Wanaozurura Katika Shehia ya Tomondo

Tume ilifanya uchunguzi wa tukio la uvunjwaji wa haki za binadamu wakati wa kutekeleza agizo la kuondoa wanyama wanaozurura mitaani katika Shehia ya Tomondo Mkoa wa Mjini Magharibi wakati wa kutekeleza agizo la Rais kudhibiti wanyama wanaozurura mijini. Tume ilifuatilia na kuchunguza tukio hilo kutokana na taarifa za vyombo vya habari ambavyo viliripoti kuhusu watu kupigwa risasi na kujeruhiwa wakati wa zoezi hilo.

Uchunguzi ulibaini kuwa zoezi la kukamata wanyama wanaozagaa katika maeneo yasiyoruhusiwa lilikuwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria na Kanuni mbalimbali za nchi ambazo ni:- Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na. 7/2014; Sheria ya Serikali za Mikoa Na. 8/2014; Sheria ya Udhibiti wa Mifugo Na. 11/1999; Sheria ya Mazingira Na. 3/2015; Sheria ya Makosa ya Jinai Na. 6/2004; Sheria ya Usalama wa Taifa Na. 8/2010; na Kanuni za Sheria hizo na Sheria ndogo ndogo za Serikali za Mitaa husika.

Sheria hizo zinaipa mamlaka Serikali ya Mkoa kuondoa wanyama kama vile ng'ombe, punda, mbuzi na kondoo waliopo katika maeneo ambayo Serikali ya mkoa itaona inafaa waondolewe. Hii ni kutokana na baadhi ya wafugaji kuwaacha holela wanyama wao, uchafuzi na uharibifu wa mazingira, ongezeko la ajali linalosababishwa na wanyama wanaozurura, kukithiri kwa wizi wa vifaa vya ujenzi na uhalifu mwingine unaofanywa na vijana wanaoendesha magari yanayokokotwa na ng'ombe au punda.

Shehia ya Tomondo iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Magharibi 'B' ni moja ya maeneo ambayo yamekatazwa kuwekwa wanyama kabisa na pia magari ya wanyama wakiwemo ya ng'ombe na punda yamepigwa marufuku.

Uchunguzi wa Tume ulibaini kuwa katika zoezi hilo ghasia zilizuka baada ya wananchi kutaka kuwazuia Polisi waliokuwa wanatekeleza jukumu hilo. Hata hivyo, Tume ilibaini kuwa Polisi walitumia nguvu kupita kiasi katika kutekeleza zoezi husika.

Mapendekezo

1. Wizara husika itoe elimu kwa wananchi kufuata sheria za utunzaji wa mazingira na sheria za ardhi ikiwepo kuepuka ufugaji katika bonde la Kwarara;
2. Jeshi la Polisi lizingatie sheria wakati linapotekeleza na kusimamia sheria na kujiepusha na matumizi ya nguvu kupita kiasi na silaha za moto.

2.10. Elimu kwa Umma na Mafunzo

Tume ilitoa elimu kwa mujibu wa Ibara ya 130(1) (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na kifungu cha 6 (1) (d) cha Sheria ya Tume Sura ya 391. Elimu kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora ilitolewa kupitia vyombo vya habari; semina; mikutano; maadhimisho ya kitaifa na kimataifa; na usambazaji wa machapisho mbalimbali.

2.10.1. Mafunzo Kuhusu Haki za Binadamu na UKIMWI

Jumla ya watu 40 (20 Unguja na 20 Pemba) walishiriki mafunzo hayo. Washiriki walikuwa wawakilishi kutoka taasisi mbalimbali za Serikali, viongozi wa dini, Masheha, Madiwani, na wengine kutoka Asasi za Kiraia. Washiriki wengine walikuwa ni wanaoishi na VVU na UKIMWI na walioathirika na Madawa ya Kulevya.

Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuelimisha jamii kuhusu haki za watu wanaoishi na VVU na UKIMWI ili waweze kupambana na vitendo vya unyanyapaa dhidi yao. Mada zilizowasilishwa ni pamoja na:- Haki za Binadamu na watu wanoishi na VVU na UKIMWI, Virusi vya UKIMWI, njia za maambukizi, namna ya kujilinda na athari za VVU na UKIMWI.

Mafunzo hayo yalikuwa ya manufaa kwani yalisaidia kuongeza uelewa wa washiriki kuhusu haki za binadamu na utawala bora na haki za watu wanaoishi na VVU na UKIMWI.

2.10.2. Mafunzo kwa Wahudumu wa Afya

Mafunzo hayo yalihusu Haki za Binadamu na Utawala Bora, Haki ya afya na Haki za Binadamu, na Uzingataji wa Utawala Bora katika Utoaji wa Huduma za Afya. Jumla ya watumishi wa afya[20] 104 (59 Unguja na 45 Pemba) walishiriki katika mafunzo hayo.

Lengo la kutoa mafunzo hayo lilikuwa ni kukuza uelewa wa washiriki juu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora ili kujenga utamaduni wa kuheshimu, kutetea, kukuza na kulinda haki za binadamu pamoja na misingi ya utawala bora wakati wakitekeleza majukumu yao.

Katika mafunzo hayo watumishi waliainisha changamoto mbalimbali wanazokutana nazo kama vile kutokamilika kwa miundo ya utumishi, mazingira ya kazi yasiyoridhisha, uelewa mdogo kuhusu haki za binadamu na uhaba wa vitendea kazi.

Kupitia mafunzo hayo, mapendekezo yafuatayo yalitolewa:

(i) Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto iboreshe miundo ya utumishi ya kada zilizopo katika sekta ya afya;

(ii) Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto iendelee kuweka mazingira

[20]Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya Wilaya ya Mpendae, Hospitali ya Wagonjwa wa Akili ya Kidongo Chekundu, Hospitali ya Wilaya Wete na Hospitali ya Rufaa ya Chake Chake

wezeshi ya kazi kwa watumishi wake ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo watumishi wake na kuhakikisha uwepo wa vitendea kazi vya kutosha; na

(iii) Serikali iendelee kutoa mafunzo ya haki za binadamu kwa watumishi katika sekta ya afya ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia haki za binadamu na utawala bora.

2.10.3. Mafunzo kwa Madiwani

Mafunzo ya haki za binadamu na utawala bora yalitolewa kwa Madiwani 102 (wanaume 53 na wanawake 49) wa Halmashauri sita (6)[21] kutoka Unguja na Pemba. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kukuza uelewa wa washiriki juu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora ili kujenga utamaduni wa kuheshimu, kutetea, kukuza na kulinda haki za binadamu na misingi ya utawala bora katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mada zilizowasilishwa katika mafunzo hayo ni:- Ijue Tume; Haki za binadamu; Utawala bora; Uhusiano wa Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora; Majukumu na Wajibu wa Madiwani.

Changamoto zilizoainishwa ni kama ifuatavyo:

(i) Uwepo wa mwingiliano wa kiutendaji baina ya madiwani na masheha;

[21] Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B, Halmashauri ya Wilaya ya Kati, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini, Baraza la Mji Wete na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni

(ii) Uwepo wa changamoto katika upatikanaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi kwani Sheha amepewa mamlaka makubwa na kwamba baadhi ya Masheha huwanyima wananchi vitambulisho kwa maslahi yao na Madiwani hawana nguvu ya kuwasaidia;

(iii) Posho wanazolipwa madiwani wa Zanzibar ni ndogo;

(iv) Kuendelea kuwepo kwa vitendo vya udhalilishaji wa watoto kutokana na wananchi wengi kutokuwa na elimu ya kutosha na hivyo kutokuwa tayari kutoa ushahidi mahakamani pale wanapohitajika kufanya hivyo; na

(v) Ingawa ugatuzi ni miongoni mwa misingi ya utawala bora, kwa upande wa Zanzibar haujafanikiwa kwa vile Serikali Kuu ilifanya ugatuzi wa rasilimali watu tu lakini rasilimali fedha na vitendea kazi vyengine havikuhamishwa kutoka Serikali Kuu, hatua iliyopelekea kushindwa kufanya kazi kama ilivyotegemewa.

Mapendekezo

(i) Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum ilipe posho kwa usawa au walipwe mishahara Madiwani wote wa Zanzibar;

(ii) Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum iendelee kutoa elimu kwa Madiwani na Masheha kuhusu majukumu yao ili kuepusha mwingiliano katika utendaji wa kazi; na

(iii) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto kwa kushirikiana na wadau wengine, itoe elimu kwa umma kupinga vitendo vya udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto;

(iv) Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ahakikishe zoezi la utoaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi linafanyika kwa ufanisi, ikiwa ni pamoja na kutoa vitambulisho hivyo kwa wahusika au kwa watu wenye sifa za kupatiwa vitambulisho hivyo kwa wakati na bila ya usumbufu.

2.10.4. Mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Wanawake na Watoto

Tume ilitoa mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Wanawake na Watoto na wawakilishi wa AZAKi zinazojihusisha na masuala ya watoto kutoka Unguja na Pemba. Jumla ya watu 45 walishiriki mafunzo hayo. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kujadili mafanikio yaliyopatikana katika jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali, taasisi zisizo za serikali, taasisi za dini na jamii kwa ujumla katika utekelezaji, ulinzi, ukuzaji na uhifadhi wa haki za watoto Zanzibar.

Kupitia mafunzo hayo ilibainika kuwa kuna; uelewa mdogo wa washiriki kuhusu haki za binadamu na misingi ya Utawala bora; baadhi ya wananchi kushindwa kuwasilisha malalamiko yanayohusu vitendo vya ukatili kwa kuamua kumalizana wenyewe; na baadhi ya wananchi kushindwa kutoa ushirikiano kwa vyombo vya dola hususan kutoa ushahidi.

2.10.5. Elimu kwa Wanajumuiya za Vyuo Vikuu

Tume ilitoa elimu kuhusu haki za binadamu na utawala bora katika Vyuo sita (6) vya elimu ya juu Zanzibar kwa wanajumuiya wa vyuo husika na kuimarisha ushirikiano na vyuo hivyo. Elimu hiyo ilitolewa katika Vyuo vifuatavyo:- Chuo Kikuu cha Taifa – SUZA), Chuo Kikuu cha Zanzibar – Tunguu Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu – Chukwani Chuo cha Taaluma ya Sayansi ya Afya – Mbweni Chuo cha Uongozi wa Fedha – Chwaka Chuo cha Ufundi – Karume

2.10.6. Elimu na Mafunzo kwa Vyama vya Wafanyakazi

Tume katika kuhakikisha kuwa haki za wafanyakazi na mazingira ya kazi zinazingatiwa ilitoa mafunzo kuhusu biashara na haki za binadamu kwa shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar pamoja na Vyama shiriki ambavyo ni Chama cha Wafanyakazi wa Utafiti na Taaluma, Chama cha Wafanyakazi wa Viwandani na Wafanyabiashara Zanzibar, Chama cha Walimu Zanzibar, Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi zinazotoa Huduma kwa Jamii, Viwanda, Biashara na Fedha Zanzibar, Chama cha Mabaharia

Zanzibar, Chama cha Wafanyakazi wa Mashambani na Wakulima Zanzibar, Chama cha Wafanyakazi wa Kamisheni ya Kazi, Chama cha Wafanyakazi wa Mahotelini na Majumbani na Chama cha Watumishi wa Umma na Afya, na Chama cha Wafanyakazi wa Mawasiliano na Uchukuzi.

Madhumuni ya mafunzo hayo yalikuwa ni kukuza uelewa wa Viongozi na wafanyakazi kuhusu uzingatiwaji wa haki za binadamu katika masuala ya biashara. Mafunzo hayo yalitolewa kwa kuzingatia Muongozo wa Umoja wa Mataifa kuhusu misingi ya Biashara na Haki za Binadamu ya Mwaka 2011 (*United Nations Guiding Principles on Business and Human Rights* – UNGP – BHR) ambayo ni kulinda, kuheshimu na kutoa nafuu kwa watu ambao haki zao zimeingiliwa.

Katika mafunzo hayo ilibainika kuwa: bado kuna uvunjwaji wa haki za binadamu hususan katika sekta ya biashara na ajira; na baadhi ya wafanyakazi kutokupata fursa ya kujiunga na vyama vya wafanyakazi.

2.10.7. Mafunzo kwa Waandishi wa Habari

Tume ilitoa elimu ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa waandishi wa habari kutoka vyombo mbalimbali vilivyopo Zanzibar. Madhumuni ya mafunzo yalikuwa ni kuwawezesha waandishi wa habari kuelewa haki za binadamu na misingi ya Utawala bora ili wazitekeleze katika utendaji wa kazi zao na kuelimisha wananchi.

Katika mafunzo hayo washiriki waliainisha changamoto mbalimbali wanazokutana nazo ikiwemo, rushwa ya ngono na maslahi duni.

2.10.8. Mafunzo kwa Kamati za Ulinzi na Usalama

Tume ilitoa mafunzo kwa Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa yote ya Zanzibar (Unguja na Pemba) kwa lengo la kuongeza uelewa kwa wajumbe juu ya masuala ya haki za binadamu na utawala bora, majukumu ya Tume na kuimarisha uhusiano na ushirikiano katika utendaji kazi na taasisi hizo.

Mada zilizowasilishwa katika mafunzo hayo zilihusu: Ijue THBUB; Haki za Binadamu na Misingi ya Utawala Bora na Utaratibu wa kuwasilisha malalamiko Tume.

Washiriki katika mafunzo hayo walipendekeza kuwa Tume iandae mpango wa kuanzisha siku maalum ya kuelimisha umma na kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi kupitia shughuli mbalimbali kama vile bonanza, mikutano ya hadhara na maonesho.

2.10.9. Elimu Kupitia Vyombo vya Habari

Tume iliandaa na kurusha hewani vipindi vya redio na luninga Unguja na Pemba kwa lengo la kuelimisha jamii kuhusu Haki za binadamu na UKIMWI; Haki za Binadamu na Biashara; Haki za Binadamu na misingi ya Utawala Bora; na Haki za Binadamu na Uchaguzi. Vyombo vilivyotumika ni:- Coconut FM, Redio Kati FM, Tumbatu FM, Mtegani FM, Chuchu FM, na Redio na Luninga ya Shirika la

Utangazaji Zanzibar (ZBC) na Redio Jamii Micheweni kwa upande wa Pemba.

2.10.10. Ziara za Kimkakati za Tume kwa Viongozi wa Kitaifa na Kikanda

Tume ilifanya ziara na mikutano ya kimkakati kwa viongozi wa ngazi mbalimbali Zanzibar. Lengo la ziara na mikutano hiyo lilikuwa ni kuitambulisha Tume kwa viongozi hao, kuboresha na kuimarisha ushirikiano baina ya Tume na Serikali katika kuwahudumia wananchi na kuimarisha ushirikiano na viongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Tume ilikutana na:- Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Hussein Ali Mwinyi; Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman; Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdallah na Waziri, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar Mhe. Haroun Ali Suleiman. Matokeo ya ziara hizo ni kuendelea kuimarika kwa ushirikiano baina ya Tume, Serikali na mashirika mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa yanayojihusisha na masuala ya haki za binadamu.

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk.Hussein Ali Mwinyi akimsikiliza Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania Mhe. Jaji Mstaafu Mathew P.M.Mwaimu, alipofika Ikulu Zanzibar na Ujumbe wake kwa mazungumzo na kujitambulisha, mazungumzo hayo yaliofanyika katika ukumbi wa Ikulu Jijini Zanzibar na (kushoto kwake) ni Makamu Mwenyekiti wa Tume Mhe.Mohamed Khamis Hamad. (Chanzo THBUB 2021)

2.11. Utafiti, Ufuatiliaji na Uchunguzi wa Hadharani

2.11.1. Utafiti na Uchunguzi wa Hadharani Kuhusu Utekelezaji wa Haki za Watoto Zanzibar (2008)

Tume ilifanya utafiti na uchunguzi wa hadharani kuhusu utekelezaji wa haki za watoto katika Wilaya sita (6)[22] za Zanzibar. Katika utafiti huo Tume ilibaini changamoto mbalimbali wanazokutana nazo watoto ikiwemo kufanyiwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wawapo skuli, majumbani na mitaani.

[22] Wete, Kaskazini 'A', Kaskazini 'B', Mjini, Chake Chake na Wilaya ya Kati

Pamoja na kuwasilisha taarifa yenye mapendekezo kwa mamlaka husika, utafiti na uchunguzi huo ulisaidia katika kukuza uelewa kwa wananchi kuhusu haki za binadamu na misingi ya Utawala bora Zanzibar; kulinda na kukuza haki za watoto; kuhamasisha taasisi za serikali na taasisi zisizo za kiserikali kulinda haki na ustawi wa watoto; na kukemea vitendo vya unyanyasaji na ukatili dhidi ya watoto.

2.11.2. Ufuatiliaji wa Tatizo la Uhaba wa Maji Zanzibar

Zanzibar ilikumbwa na tatizo la kukatika kwa umeme kuanzia tarehe 10 Disemba 2009 hadi mwezi Machi, 2010 hali iliyosababisha uhaba mkubwa wa maji. Kwa kutambua kuwa maji ni hitaji la msingi kwa uhai wa binadamu Tume ilifanya ufuatiliaji wa vyanzo vya maji ili kuona hali halisi ya tatizo hilo. Jumla ya vyanzo 37 vya maji katika mikoa ya Kaskazini (U), Kusini (U) na Mjini Magharibi vilitembelewa na kukaguliwa.

Tume ilibaini, pamoja na mambo mengine, kuwepo kwa uharibifu wa mazingira ya vyanzo vya maji; uchakavu wa mitambo ya maji na vitendea kazi; maeneo ya vyanzo vya maji kutokuwa na hati miliki; uharibifu wa vituo vya maji; kukatika kwa umeme kwa miezi minne (4); na watumishi kutokuwa na ujuzi na utaalam wa kutosha.

Ufuatiliaji huo ulikuwa na mafanikio kwani uliongeza uelewa kuhusu haki za binadamu na

misingi ya Utawala bora na kuhamasisha umuhimu wa utunzaji wa mazingira.

2.11.3. Ufuatiliaji wa Mchakato wa Uchaguzi

Katika kipindi cha mwaka 2015 na 2020 Tume ilifanya ufuatiliaji wa mchakato wa uchaguzi katika hatua za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; kampeni za wagombea na upigaji, kuhesabu, kujumlisha kura na kutangaza matokeo. Chaguzi hizo zilihusu uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, Wawakilishi na Madiwani; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge.

Malengo ya ufuatiliaji huo yalikuwa ni:- kutathmini uzingatiwaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwenye chaguzi hizo; kutathmini uzingatiwaji wa sheria, kanuni na maadili ya uchaguzi; kuangalia ushiriki wa wananchi kwenye mchakato wa uchaguzi; na kutoa mapendekezo kwa mamlaka husika kuhusu masuala ya haki za binadamu, utawala bora na uchaguzi.

Afisa wa THBUB Bi Saada A. Masoud akiwa katika chumba cha kupigia kura akifuatalia Uchaguzi Mkuu wa Oktoba Mwaka 2020 katika Kituo cha uchaguzi Kinuni. [Picha THBUB]

Yaliyojitokeza Katika Zoezi la Ufuatiliaji wa Mchakato wa Uchaguzi Mkuu

(i) Mamlaka ya Usajili wa Matukio ya Kijamii kutowapatia baadhi ya wananchi vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi hivyo kutoandikishwa kwenye daftari la wapiga kura na kushindwa kupiga kura;

(ii) Baadhi ya majina ya wapiga kura kutokuwepo katika orodha ya majina yaliyokuwa yamebandikwa katika vituo vyao vya kuandikishwa;

(iii) Baadhi ya vituo kutokuwa rafiki kwa watu wenye mahitaji maalum kutokana na kuwa kwenye mazingira ya kutofikika kirahisi;

(iv) Uwepo wa mamlaka mbili tofauti ambazo ni Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar na Mamlaka ya Usajili wa Matukio ya Kijamii zinazoshughulikia masuala ya mpiga kura kumesababisha baadhi ya wanaostahili

kupiga kura kutoandikishwa katika daftari la kudumu la wapiga kura kutokana na kutopata kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi kwa wakati;

(v) Kutokuwepo watoa huduma ya afya katika mikutano ya kampeni; na

(vi) Kuwepo kwa tukio la kushambuliana kwa mapanga misikitini katika mji wa Wete kwa imani na itikadi za kisiasa.

Hamisi Nyange Makame maarufu kama Profesa Gogo (63), aliyekatwa mapanga wakati wa swala ya alfajiri katika msikiti wa Kangagani Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba (Chanzo: https://globalpublishers.co.tz/ magufuli-amjulia-hali-aliyekatwa-mapanga-msikitini-video/)

Mapendekezo

Taarifa zenye mapendekezo ziliandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika kwa ajili ya utekelezaji. Mapendekezo hayo ni pamoja na:-

(i) Mamlaka ya Usajili wa Masuala ya Kijamii ishughulikie upatikanaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi kwa wakati ili kuwawezesha wapiga kura kujiandikisha;

(ii) Serikali iweke utaratibu wa kuunganisha taarifa za wapiga kura kwenye vitambulisho vya utaifa ili kupunguza gharama na “duplication” kati ya uandikishwaji unaofanywa na NEC/ZEC na unaofanywa na Ofisi ya Vitambulisho vya Taifa;

(iii) Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Afya iweke mpango madhubuti kuhakikisha huduma ya kwanza inapatikana kwenye mikutano ya kampeni za uchaguzi;

(iv) Viongozi wa vyama vya siasa, wagombea na wadau wengine wa uchaguzi wazingatie sheria na kanuni za uchaguzi katika kipindi chote cha mchakato wa uchaguzi na kutotumia lugha zinazoweza kupelekea uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

(v) ZEC na wadau mbalimbali waendelee kutoa elimu kwa wananchi yakiwemo makundi maalum kuhusu haki ya kushiriki katika mchakato wa uchaguzi.

2.11.4. Ufuatiliaji wa Haki za Watu Wenye Matatizo ya Afya ya Akili

Tume ilifanya ufuatiliaji huo kwa lengo la kutathmini hali za watu hao na kutoa mapendekezo na ushauri kwa mamlaka zinazohusika kwa ajili ya kutatua changamoto

zilizopo kwa kuzingatia haki za binadamu na misingi ya utawala bora.

Changamoto zilizobainika katika ufuatiliaji huo ni pamoja na:

(i) Jamii kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu haki za watu wenye matatizo ya afya ya akili;

(ii) Uchache wa watoa huduma katika hospitali na vituo vya kutolea huduma za afya;

(iii) Ufinyu wa bajeti katika kuwahudumia watu wenye matatizo ya afya ya akili.

Taarifa yenye mapendekezo ya namna ya kuboresha hali na haki za watu wenye matatizo ya afya ya akili iliandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika ambapo pamoja na mambo mengine ilipendekezwa:-

(i) Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau wanaojishughulisha na matatizo ya afya ya akili zitoe elimu kwa jamii kuhusu tatizo hili na namna ya kuwahudumia wagonjwa badala ya kuwanyanyapaa;

(ii) Wizara ya Afya ichukue jitihada kuongeza idadi ya wataalam wa magonjwa ya afya ya akili na kutoa mafunzo ya mara kwa mara ya taaluma ya afya ya akili; na

(iii) Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuboresha huduma ya afya, chakula na

malazi katika hospitali zinazotoa huduma kwa watu wenye matatizo ya afya ya akili.

2.11.5. Ukaguzi wa Vyuo vya Mafunzo na Vituo vya Polisi Zanzibar

Kifungu cha 6(1) (h) cha Sheria ya Tume, Sura ya 391 kinaipa Tume mamlaka ya kukagua magereza, vituo vya polisi na sehemu zingine wanamozuiliwa watu ili kutathmini hali za watu wanaozuiliwa katika sehemu hizo na kutoa mapendekezo ya namna ya kurekebisha matatizo yaliyopo. Tume ilifanya ukaguzi wa vyuo vya mafunzo na vituo vya polisi katika Mikoa yote ya Zanzibar.

Lengo la kaguzi hizo ni kutathmini hali ya utekelezaji wa haki na ustawi wa watu wanaozuiliwa kwa mujibu wa sheria za nchi na viwango vya kimataifa na kikanda vilivyoainishwa katika mikataba ya kimataifa na kikanda ambayo Tanzania imeridhia.

Yaliyobainika Katika Kaguzi za Vituo vya Polisi

(i) Uchakavu wa miundombinu katika baadhi ya vituo vya polisi hali inayohatarisha usalama wa maisha ya Mahabusu na Askari;

(ii) Baadhi ya vituo kuwa na upungufu wa samani na ufinyu wa nafasi kwa mfano Chwaka, Mfenesini na Mkokotoni;

(iii) Baadhi ya vituo kutokuwa na vyumba vya wanawake na watoto hivyo kusababisha

wanawake na watoto kuhifadhiwa katika vyumba ambavyo siyo rasmi kwa matumizi hayo;

(iv) Tatizo la upatikanaji wa chakula kwa mahabusu katika vituo vya polisi kutokana na bajeti ndogo inayotolewa kwa vituo vya polisi kuwalisha watuhumiwa. Hali hii husababisha baadhi ya Wakuu wa Vituo vya Polisi (OCS) na aAskari wa zamu kutumia fedha zao binafsi kuwahudumia watuhumiwa;

(v) Tatizo la usafiri ikizingatiwa baadhi ya vituo vinahudumia maeneo makubwa, kuhamisha na kupeleka watuhumiwa vituoni na Mahakamani;

(vi) Malalamiko ya maslahi ya watumishi ikiwemo kutolipwa posho mbalimbali, kutopandishwa vyeo; kucheleweshwa kwa fidia ya kuumia kazini; kutokuwepo kwa baadhi ya huduma katika hospitali na zahanati; Askari wapya kucheleweshewa mishahara; kutorekebishiwa mishahara yao, na pindi inaporekebishwa kutolipwa malimbikizo;

(vii) Askari kutokuwa wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii; na kupunjwa au kucheleweshewa mafao ya kustaafu.

Yaliyojitokeza Katika Vyuo vya Mafunzo

(i) Uchakavu wa miundombinu katika baadhi ya majengo ya vyuo vya mafunzo;

(ii) Kuendelea kutumika Mitondoo katika baadhi ya vyuo;

(iii) Kukosekana kwa huduma ya usafiri kwa baadhi ya Vyuo vilivyokaguliwa;

(iv) Baadhi ya Vyuo kutokuwa na huduma ya afya, madaktari na madawa;

(v) Baadhi ya nyumba za askari ni mbovu, chakavu na hazikidhi kuishi binadamu;

(vi) Kutokuwepo kwa mabweni kwa ajili ya wafungwa na mahabusu watoto;

(vii) Maji safi, mawasiliano na burudani vyote vinapatikana katika vyuo vilivyokaguliwa;

(viii) Kukosekana kwa vitendea kazi kama vile kinga (mask) na viatu kwa wanafunzi kwenye baadhi ya vyuo;

(ix) Uhaba wa vitendea kazi kwa Askari ili kuboresha utendaji wa kazi;

(x) Madai ya malipo ya posho ya uhamisho na nauli ya likizo kwa baadhi ya askari wa vyuo vya mafunzo;

(xi) Malalamiko ya wanafunzi na mahabusu dhidi ya Jeshi la Polisi ikiwemo:- Ucheleweshaji

upelelezi wa kesi; kudhalilishwa na kupigwa ili kukiri makosa; kubambikizwa kesi; na kuchukua vitu wanavyokutwa navyo na kutorudishiwa wakati wanapoachiwa huru;

(xii) Mahakama kucheleweshа kutoa hukumu pamoja na nakala za hukumu kwa wafungwa na ucheleweshaji wa kusikiliza rufaa;

(xiii) Ufinyu wa bajeti na uhaba wa rasilimali fedha kwa ajili ya huduma za Idara ya vyuo vya mafunzo na wanafunzi na mahabusu;

(xiv) Kutokuwepo utaratibu wa kupatiwa fedha kwa kila chuo moja kwa moja kwa ajili ya huduma za chuo husika, badala yake kila chuo hupata bidhaa za huduma zinazohitajika kutoka Makao Makuu;

(xv) Kutokuwepo usafiri wa kuwapeleka wanafunzi na mahabusu mahakamani siku za kesi zao au rufaa; na

(xvi) Upungufu wa dawa na kutokuwepo daktari mkaazi katika baadhi ya vyuo.

Askari wa Vyuo vya Mafunzo

(i) Tatizo la ubovu wa miundombinu ya maji, vyoo na umeme katika makazi ya askari na ufinyu wa posho ya makazi;

Mojawapo ya nyumba zinazotumiwa na askari na familia zao kwa makaazi katika kambi za idara ya chuo cha mafunzo (Chanzo THBUB 2021)

(ii) Upungufu wa sare, kuwa za daraja la chini, kutopatikana zote na Askari kujinunulia viatu wenyewe;

(iii) Mazingira magumu ya kazi kwa Askari kutokana na mishahara midogo, kutokuwepo kwa muda maalum wa uhamisho kutoka Pemba au Unguja;

(iv) Ugumu wa Askari kupata ruhusa pindi inapotokea tatizo kwani ruhusa ya kusafiri kutoka Pemba kwenda Unguja sharti itoke kwa Kamanda wa Vyuo vya Mafunzo Makao Makuu Unguja;

(v) Uhaba wa vitendea kazi na samani, ubovu na uchakavu wa ofisi za vyuo vya mafunzo;

(vi) Mishahara midogo na isiyokidhi kujikimu kimaisha, kulipwa bila nyongeza ya kila mwaka na kutokuwepo kwa tofauti ya mishahara kati ya waajiriwa wa zamani na wapya;

(vii) Kutokuwepo kwa utaratibu au mpango wa kujiunga na mafunzo kwa Askari asiye au aliye na cheo, na kama upo haufuatwi ipasavyo;

(viii) Kutokuwepo kwa usawa na uwazi katika kuhudhuria au kujiunga na mafunzo na upandishwaji wa vyeo;

(ix) Tatizo la ulipwaji wa nauli ya likizo ambapo baadhi ya Askari wamelipwa mara moja ndani ya miaka kumi na tano;

(x) Uhamisho kutofanyika kwa haki ikilinganishwa na Idara Maalumu zingine za SMZ kwani wakati mwingine unachukuliwa kama ni adhabu kwa Askari, kwani baadhi hupewa uhamisho bila kujali ndoa;

(xi) Idara ya Chuo cha Mafunzo haitoi fidia wala msaada wa tiba kwa Askari anayeumia kazini;

(xii) Matukio ya Askari kupigwa, kutemewa mate, kumwagiwa vinyesi au mikojo na wakati mwingine kutorokwa na wanafunzi au mahabausu wakati wanawasimamia; na

(xiii) Askari kutorejeshwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) na mfuko wa Bima ya Afya.

Mapendekezo ya Kuboresha Changamoto Zilizobainika

(i) Wizara husika iboreshe huduma ya afya katika Vyuo vya mafunzo ikiwemo dawa za kutosha na Daktari mkaazi na wataalam wa afya;

(ii) Vyuo vya mafunzo vihakikishe uwepo wa vitendea kazi kwa wanafunzi wanaofanya kazi za kilimo kama vile kinga (mask) wakati wa kunyunyizia

dawa mashambani na viatu vinavyolingana na mazingira ya kazi;

(iii) Jeshi la Polisi liharakishe upelelezi wa kesi ili kupunguza msongamano wa mahabusu na kupunguza gharama za kuwahudumia;

(iv) Vyuo vya mafunzo vihakikishe upatikanaji wa magodoro, dawa ya mswaki na sabuni zenye dawa ya kinga (medicated soap) ili kusaidia kuondoa maradhi ya ngozi;

(v) Viongozi wa dini wawe na utaratibu endelevu wa kuwatembelea wanafunzi na mahabusu katika vyuo vya mafunzo;

(vi) Maslahi ya Askari wa vyuo vya mafunzo yaboreshwe ikiwemo makazi bora, upandishaji wa vyeo, nyongeza za mishahara, malipo ya posho na likizo;

(vii) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Hifadhi ya Jamii (ZSSF) iandae utaratibu wa kuwapatia bima ya afya na mafao Askari wa Vyuo vya Mafunzo;

(viii) Serikali na wadau kuwa na program ya mafunzo na semina kwa Askari kwa ajili ya kuwajengea uwezo kuhusu haki za binadamu, utawala bora na utendaji wao wa kazi;

(ix) Serikali ifanye maboresho ya miundombinu ya vyuo vya mafunzo ikiwemo ujenzi na ukarabati wa vyoo vya ndani ili kuepuka matumizi ya mitondoo;

(x) Vyuo vya mafunzo viboreshe utendaji kazi wa Askari kwa kuwalipa posho ya mazingira magumu; malipo ya fidia, uzingatiwaji wa haki katika taratibu za uhamisho kwa askari;

(xi) Kamanda wa vyuo vya mafunzo Pemba apewe mamlaka ya kutoa ruhusa kwa Askari aliyepo chini ya uongozi wake badala ya ruhusa kutolewa makao makuu Unguja;

(xii) Jeshi la Polisi liharakishe upelelezi wa kesi, kuzingatia maadili ya kazi, kutowabambikiza kesi na kutowatesa watuhumiwa;

(xiii) Mahakama ziharakishe kutoa hukumu za kesi, nakala za hukumu pamoja na kusikiliza rufaa kwa wakati unaofaa;

(xiv) Vyuo vya mafunzo vizingatie haki na usawa katika fursa za mafunzo na kozi mbalimbali na upandishwaji wa vyeo kwa askari wa vyuo vya mafunzo;

(xv) Wizara ya Mambo ya Ndani iboreshe madawati ya jinsia na watoto kwa kuwapatia vitendea kazi na mafunzo askari husika ili kuongeza ufanisi; na

(xvi) Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, ichukue jitihada za makusudi za kujenga mabweni maalum kwa ajili ya wanafunzi na mahabusu watoto katika Vyuo vya Mafunzo.

2.11.6. Ukaguzi wa Vituo vya Malezi ya Watoto

Kaguzi hizi zilifanyika katika vituo vya malezi ya watoto vya Mazizini na Kijiji cha SOS kilichopo Mombasa Mkoa wa Mjini Magharibi. Malengo ya kaguzi hizo ilikuwa ni kutathmini hali ya utekelezaji wa haki na ustawi wa watoto wanaoishi katika vituo hivyo.

Kamishna wa THBUB, Mhe. Mohamed Khamis Hamad akifurahia jambo na baadhi ya watoto wanaolelewa katika Kituo cha kulelea Watoto cha Mazizini katika Mkoa wa Mjini/Magharibi Ungua. (Chanzo THBUB 2017)

Changamoto Zilizobainika Wakati wa Ukaguzi

(i) Posho ya usafiri na nyumba kwa ajili ya watumishi zimejumuishwa katika mshahara na hazilipwi kwa wakati;

(ii) Katika vituo vyote watumishi walilalamikia kulipwa mishahara midogo isiyokidhi mahitaji yao muhimu;

(iii) Walezi wa watoto kutopewa mafunzo maalumu ya malezi ya watoto.

(iv) Kutokuwepo kwa utaratibu maalum wa kumwandaa mtoto kwa kumpatia ujuzi au shughuli ya kujitegemea baada ya kumaliza muda wa kulelewa kituoni; na

(v) Wazazi/walezi kutotoa ushirikiano kwa walezi wa kituo na pengine watoto hufikia umri wa kuondoka kituoni bila ya mzazi/mlezi kufika kituoni hapo.

Mapendekezo ya Kuboresha Huduma za Watoto katika Vituo

(i) Serikali na wadau wahakikishe utekelezaji wa Sheria ya Mtoto kwa ajili ya haki na maslahi ya watoto;

(ii) Wizara ya Ustawi wa Jamii ichukue hatua kuhakikisha uwepo wa vitendea kazi katika Vituo vya Malezi ya Watoto ikiwemo Kituo cha Mazizini; Wizara ya Maendeleo ya Jamii kuandaa programu endelevu ya kuwajengea uwezo walezi wa vituo vya kulelea watoto ili waweze kukabiliana vyema na changamoto zinazojitokeza katika malezi ya watoto;

(iii) Kuwe na ushirikiano endelevu kati ya vituo vya kulelea watoto na wataalamu wa ushauri nasaha kutoka taasisi nyingine katika kurekebisha tabia za watoto;

(iv) Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto, ishirikiane na Wizara ya Afya kuanzisha Zahanati yenye wataalam wa afya na gari la wagonjwa katika vituo vya watoto;

(v) Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ifanye mapitio ya muundo wa watumishi wa Idara ya Ustawi wa Jamii kwa lengo la kuainisha na kuoanisha taaluma, wajibu na maslahi ya watumishi wa vituo vya kulelea watoto;

(vi) Taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali zinazojihusisha na masuala ya kulea watoto ziimarishwe kitaaluma na miundombinu ili ziwe na mifumo bora na yenye tija kwa malezi ya watoto; na

(vii) Wizara ya Kazi Maendeleo ya Vijana, Wazee, Wanawake na Watoto itoe kipaumbele katika nafasi za ajira kwa watoto waliolelewa katika vituo hivyo kulingana na vyeti vya elimu walivyo navyo.

2.11.7. Ukaguzi wa Vituo vya Makazi ya Wazee Zanzibar

Tume ilifanya ukaguzi wa makazi ya wazee ya Sebuleni (Wilaya ya Mjini) na Welezo (Wilaya ya Magharibi) katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Lengo la ukaguzi huo lilikuwa ni kutathmini utekelezaji wa haki za binadamu za wazee katika vituo hivyo.

Yaliyojitokeza Wakati wa Ukaguzi

Ukaguzi katika vituo hivyo ulibaini yafuatayo:-

(i) Majengo ni machakavu na mazingira yake siyo salama kwa wakazi wake;

(ii) Huduma ya maji safi na salama na vyoo haziridhishi;

(iii) Katika Kituo cha Sebuleni huduma muhimu za chakula, maji, nishati, matandiko na usafiri zinapatikana na wazee hupewa posho ya Shilingi 40,000 kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao;

(iv) Tatizo la upungufu wa madawa na vifaa tiba kwa wazee wanaoishi katika vituo hivyo.

Kamishna wa THBUB, Mhe. Mohamed Khamis Hamad akiburudika kwa kucheza bao na mmoja wa wazee wanaoishi katika kituo cha Welezo kilichoko katika Wilaya ya Magharibi, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja tarehe 18,/01/2017 (Chanzo THBUB 2017)

Katika kuboresha huduma kwa wazee katika vituo hivyo, yalitolewa mapendekezo yafuatayo:

(i) Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ichukue hatua za kukarabati majengo ya makazi ya wazee;

(ii) Wizara husika iboreshe vitendea kazi na mazingira ya makazi hayo kwa kuyaweka katika hali ya usafi wakati wote;

(iii) Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano iweke kivuko cha watembea kwenye barabara kuu katika eneo la makazi ya wazee Sebuleni ili kulinda usalama wa wazee wanapovuka barabara;

(iv) Serikali iimarishe miundombinu, ikiwemo umeme, maji, usafiri na huduma nyingine zinazoendana na mahitaji maalum ya wazee;

(v) Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa kushirikiana na AZAKi itoe elimu kuhusu haki za wazee kwa watendaji wa vituo na wananchi kwa ujumla;

(vi) Wizara ya Afya ichukue hatua za kuimarisha huduma za afya katika makazi ya wazee;

(vii) Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto iboreshe maslahi ya watumishi wanaofanya kazi katika makazi ya wazee;

(viii) Serikali iongeze ruzuku kwa kituo cha Welezo kwani kiasi cha sasa cha Tsh. 3,000,000 kwa mwezi hakitoshelezi mahitaji ya kituo.

2.12 Ushirikiano wa Tume na Taasisi Nyingine

Tume iliendeleza ushirikiano na taasisi za kitaifa, na kimataifa kwa mujibu wa Kanuni za Paris na kifungu cha 6 (1) (m) cha Sheria ya Tume Sura ya 391. Ushirikiano huu ulikuwa katika nyanja za kutetea, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na uzingatiaji wa misingi ya utawala bora. Taasisi ambazo Tume ilishirikiana nazo ni UNICEF na UNDP kwa upande wa Kimataifa.

THBUB ilishirikiana na Wizara na Idara za Serikali ikiwemo:- Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora; Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwezeshaji; Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi; Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali; Mahakama naOfisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Nyingine ni Taasisi za dini na Asasi za Kiraia ikiwemo Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar; Kituo cha Msaada wa Sheria Zanzibar; Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar; Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA); *Legal Service Facilities (LSF)*; Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi.

SURA YA TATU

HITIMISHO

Katika kipindi cha miaka 20 Tume kama Taasisi ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya kitaifa imetekeleza jukumu lake la kulinda, kutetea na kuhifadhi haki za binadamu na uzingatiaji wa misingi ya utawala bora nchini. Mafaniko haya yametokana na ushirikiano mzuri kati na Tume na wadau mbalimbali. Hii ni kutokana na ukweli kwamba utetezi, ulinzi na uhifadhi wa haki za binadamu na uzingatiwaji wa misingi ya utawala bora ni suala mtambuka duniani kote linalohitaji nguvu za pamoja katika utekelezaji wake. Aidha, uhamasishaji wa haki za binadamu na uzingatiwaji wa utawala bora ni kichocheo cha maendeleo ya nchi.

Tume imefanikiwa kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kisheria ya kutoa elimu; kupokea na kushughulikia malalamiko; kufanya tafiti, ufuatiliaji, uchunguzi; usuluhishi na upatanishi; kupitia sheria; kufuatilia mapendekezo ya Tume na kuishauri serikali na taasisi mbalimbali kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

Safari ya miaka 20 ya THBUB katika utekelezaji wa majukumu yake imekabiliwa na changamoto kadha wa kadha. Changamoto hizo ni pamoja na: ufinyu wa bajeti; uelewa mdogo wa wananchi kuhusu haki za binadamu na utawala bora; ushirikiano mdogo kutoka kwa taasisi zinazolalamikiwa; kutotekelezwa kwa mapendekezo ya Tume kwa wakati au kutotekelezwa kabisa; huduma za Tume kuwa mbali na wananchi kutokana na kuwa na ofisi chache; Taarifa za

utekelezaji wa majukumu ya Tume kutoifikia jamii na hivyo Tume kukosa nafasi ya kuonekana na kutofahamika kazi zinazotekelezwa na Tume.

Ushirikiano endelevu kati ya Tume, Serikali na wadau wa ndani na nje wa masuala ya haki za binadamu na utawala bora ni suala lisiloepukika katika kukabiliana na changamoto hizo na kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake. Mafanikio ya Tume katika kutekeleza majukumu yake katika kipindi kijacho yatatokana na imani ya Serikali kwa Tume kama chombo saidizi cha utekelezaji wa shughuli za Serikali ili kuwezesha kujenga jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu, utu wa mtu na misingi ya utawala bora. Uzingatiaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya taifa.

MATUKIO KATIKA PICHA

Aliyekuwa Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Pinda, akipata maelezo kutoka kwa maofisa wa THBUB wakati alipotembelea banda la THBUB, siku ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu na Siku ya Maadili yaliyofanyika kwenye viwanja vya Mnazi mmoja, jijini Dar es Salaam, tarehe 10 Desemba, 2012. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)

Aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Mohamed Gharib Bilali akizundua Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu katika kilele cha maadhimisho ya siku ya haki za binadamu yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja tarehe 10/12/2013.

Uongozi mpya wa Awamu ya Tatu ya THBUB ukiwa katika picha ya pamoja na Mhe. Rais waa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Nne Mhe. Dr Jakaya Mrisho Kikwete mara baada ya kuapishwa Ikulu Jijini Dar es Salaam tarehe 7 Januari 2015. (Chanzo THBUB 2015)

Aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. Mohamed Ali Shein akihutubia taifa siku ya maadhimisho ya Miaka sitini ya tamko la haki za binadamu tarehe 10 Disemba 2008

Ujumbe wa mabalozi 11 wa Jumuiya ya Ulaya na Mkurugenzi wa Idara ya Haki za Binadamu ya THBUB, Bw. Francis Nzuki ulipowatembelea wafungwa waliohukumiwa kunyongwa walioko katika Gereza Kuu la Ukonga, Dar es Salaam katika Kampeni ya siku ya kupinga adhabu ya kifo duniani tarehe. Tarehe 10 Oktoba 2015

Pichani Aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume Bw. Bahame Nyanduga (aliyekaa katikati) na Katibu wa AOMA Bw. Ottiende Amolo (wa pili kulia) alipoitembelea THBUB kufuatilia maandalizi ya Mkutano Mkuu wa AOMA. Mkutano huo ulitarajiwa kufanyika Mwezi, Septemba, 2016 Jijijni Arusha

Aliyekuwa Rais wa Awamu ya nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Jakaya Mrisho Kikwete (wa tano kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa Serikali na Makamishna wa THBUB alipotembelea Ofisi za THBUB mwaka 2015. (Chanzo: THBUB 2015)

Aliyekuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Tulia Ackson (kushoto) akimkabidhi cheti Makamu Mwenyekiti wa THBUB Mhe. Mohamed Khamis Hamad kwa kutambua mchango wa THBUB kwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani. Mei 15, 2020, katika viwanja vya hospitali hiyo: (Chanzo THBUB 2020)

Maandamano ni miongoni mwa shughuli zinazofanywa kila mwaka wakati wa maadhimisho ya Siku ya haki za binadamu duniani. Pichani ni waandamanaji, baadhi yao wakiwa na mabango yenye jumbe mbalimbali wakipita katika mitaa ya jiji la Dar es Salaam wakielekea viwanja vya Mnazi Mmoja Desemba 10, 2013.

Viongozi na wageni mashuhuri waliohudhuria maadhimisho ya miaka 50 ya iliyokuwa TKU wakiongozwa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili wa Jamhuriya Muungano wa Tanzania, Mhe. Alhaj Ali Hassan Mwinyi (katikati) wakiwa katika picha ya pamoja. Kutoka kushoto waliokaa ni: Mwenyekiti wa THBUB, Mhe. Bahame Tom Nyanduga, Mwanasheria Mkuu mstaafu, Mhe. Jaji Mark Bomani, Mawaziri Wakuu wastaafu, Wahe. Fredrick Sumaye na Jaji Mstaafu Joseph Warioba, Waziri wa Nchi Ofisi Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Angelah Kairuki, (Mb), Mwenyekiti Tume ya Uchaguzi, Mhe. Jaji Mstaafu Damian Lubuva, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere,Mhe. Joseph Butiku na Makamu Mwenyekiti wa THBUB, Mhe. Iddi Ramadhani Mapuri. Ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam, Oktoba 21, 2016.

Aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (katikati) na mtoto wa Mwenyekiti wa kwanza wa TKU, Hayati Chifu Erasto Mang'enya, Bwana Stanley Erasto Mang'enya (wa tatu kushoto) wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa THBUB na watumishi wa TKU waliopewa tuzo, mara baada ya Mhe. Waziri kukabidhi tuzo zilizotolewa na Muungano wa Taasisi za Uchunguzi na Usuluhishi Afrika (AOMA) kutambua mchango uliotukuka wa Hayati Mang'enya katika masuala ya uwajibikaji barani Afrika. Tuzo hizo zilitolewa Novemba 2016 huko Durban Afrika Kusini na kupokelewa kwa niaba ya familia na Mwenyekiti wa THBUB, Mhe. Bahame Tom Nyanduga.